

**UCHANGANUZI WA KIPRAGMATIKI WA MAANA YA MAWASILIANO
KATIKA JUKWAA LA FACEBOOK**

SIMON PETER KATUI

**Tasnifu hii imewasilishwa Kwa ajili ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya
uzamili katika masomo ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi**


2020

UNGAMO

Nakiri kuwa tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa katika chuo chochote kwa minajili ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili.


Simon Peter Katui

C50/5899/2017

Sahihi.  Tarehe. 14/11/2021

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa Kwa idhini yetu wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

PROF. JOHN HAMU HABWE

Sahihi.  Tarehe. 15/11/2021

MWALIMU ANDREW WATUHA

Sahihi.  Tarehe. 17/11/2021

TABARUKU

Kwa wazazi wangu wpendwa: Samwel Katui Na mama yangu mpendwa Sara Ombiso Katui pamoja na ndugu zangu na dada zangu.

SHUKRANI

Shukrani zangu za kipekee zimwendee Mwenyezi Mungu aliyeniumba kwa mfano wake kwa kunipa pumzi na uhai pamoja na idili kama kauli mbiu maishani mwangu.

Ningependa kuwashukuru wasimamizi wangu prof. John Habwe na Dkt, Andrew Watuha kwa mawaidha yao ya busara na kwa kujitolea kusoma kazi hii na kunikosoa na kuweza kunipa mwelekeo unaofaa. Shukrani za dhati na Mungu awabariki. Shukrani ya kipekee naitoa Kwa Dkt. James Nyachai Michira aliyekuwa msimamizi wangu mtangulizi kwa kuweza kuisoma kazi yangu na kunipa ushauri ulionifaa katika kufanikisha kazi hii pia. Mungu akaweze kumbariki.

Nawashukuru pia wahadhiri wote katika chuo kikuu cha Nairobi, Idara ya Kiswahili Kwa mafunzo na ushauri wenu mwema ambao umeniwezesha kuiona ndoto yangu ya kiakademia. Shukrani zangu ziwafikie Prof. Iribe Mwangi, Prof. Rayya Timammy, Prof. Mwenda Mbatia, Prof. Kineene Wamutiso, Prof. Kyalo Wadi Wamitila, Prof. Evans Mbuthia, Prof, Tom Mboya Olali, Prof. Kithaka Wamberia, Dkt. Prisca Jerono, Dkt. Basilio Mungania, Dkt, Ayubu Mukhwana, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Amir Swaleh, Dkt. Mwaliwa, Dkt. Ongarora na Mwalimu Leo sanja.

Shukrani zingine ziwafikie wanafunzi wenzangu tuliosoma pamoja. Hawa ni Oliver Onyango Ogutu, Yunny Amisi, Kirui Simon Kipkoech, Deon Musau Muia, Joseph Peter Kang'ethe, Susa Agatha Twili, Kithure Misheck, Mulati Benard, Mwebesa Alex na Purity Kathomi Mutegi. Mwisho siwezi kuwasahau wale ambao Kwa njia moja au nyingine wamechangia kufanikisha utafiti huu. Kwenu nyote nasema shukrani.

IKSIRI

Tasnifu hii imeshughulikia uchanganuzi wa maana ya kipragmatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza suala la maana ya kipramatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook na malengo maalum yakiwa ni; kubainisha maana ya kipragmatiki katika mawasiliano ya Facebook, kujadili mikakati ya usimbwaji na upanuzi wa maana na kujadili mikakati ya ubanaji wa lugha inavyotumika katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook. Data iliyoweza kufanikisha malengo ya utafiti huu ilitolewa kutoka intaneti kwa makundi ya wanafunzi wa chuo kikuu ambao huwasiliana kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika jukwaa la Facebook. Makundi ambayo yaliteuliwa kutumika katika utafiti huu ni; Kenyan university students, K.U. comrades forum na Kenya university organization. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya pragmatiki leksika ya Blutner (1990), ambapo matokeo ya utafiti huu yamebainika kuwa , wanafunzi wa chuo kikuu huwasiliana kwenye jukwaa la Facebook kwa matumizi ya michakato ya kipragmatiki ambayo ni; upanuzi wa maana, ubanaji wa maana na kisio la maana. Isitoshe, imebainika kwamba asilimia kubwa ya wanafunzi wa chuo kikuu huwasiliana katika jukwaa la Facebook kwa kutumia mchakato wa upanuzi wa kimaana, ikifuatwa na mchakato wa ubanaji wa maana huku asilimia ndogo zaidi ya wanafunzi wa chuo kikuu ikiwasiliana kwa matumizi ya mchakato wa kipragmatiki wa kisio la maana.

**MAELEZO YA ISTILAHU MUHIMU KAMA ZILIVYOTUMIKA KATIKA
UTAFITI**

- Michakato** - Mfululizo wa shughuli ambazo husababisha kitu Fulani kufanyika au malengo fulani kuafikiwa.
- Michakato ya kileksika** - Mikondo ambayo leksimu hujukuwa kwa minajili ya kuleta fahiwa mpya jinsi inavyowasilishwa katika mawasiliano.
- Pragmatiki leksika** - Nadharia inayoshughulikia maana za leksimu kulingana na muktadha wa kimawasiliano.
- Semantiki leksika** - Aina ya semantiki inayojishughulisha na maana za kileksika za maneno.
- Mawasiliano** - Ni utaratibu wa maongezi baina ya pande mbili au ni namna ambayo pande mbili za watu hutoa kauli hivi kwamba, kila kauli inatolewa na mwasilianaji kwa wakati wake.
- Mikakati ya kipragmatiki** - Mbinu mbalimbali ambazo zinatumiwa na wanafunzi wa chuo kikuu katika mawasiliano yao ili kuusitiri ujumbe kwa wanakikundi na kusababisha ufafanuzi wa maana ya usemi kimuktadha.
- Mikakati ya upanuzi wa maana-** Mbinu mbalimbali ambazo zinatumiwa na wanafunzi wa chuo kikuu katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook ili kuleta upanuzi wa maana ya neno.
- Mikakati ya ubanaji lugha** - Mbinu mbalimbali zinazotumiwa na wanafunzi wa chuo kikuu katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook ili kuweza kuufinya ujumbe fulani kwa maana moja kusudiwa.
- Usemi** - Ni maneno ambayo yanatolewa na wanafunzi wa chuo kikuu katika maandishi na yanawakilisha maoni au fikra za mwasilianaji kuhusu mtazamo wake kwa jambo fulani.

YALIYOMO

UNGAMO.....	ii
TABARUKU	iii
SHUKRANI.....	iv
IKSIRI.....	v
SURA YA KWANZA : MSINGI WA UTAFITI	1
1.0 Utangulizi.....	1
1.1 Tatizo la Utafiti	3
1.2 Malengo ya Utafiti	3
1.3 Maswali ya Utafiti.....	3
1.4 Upeo na Mipaka.....	3
1.5 Umuhimu wa Utafiti	4
1.6 Msingi wa Nadharia	4
1.7 Nadharia ya Pragmatiki leksika ya Blutner Reinhard.....	5
1.8 Mihimili ya Nadharia ya Pragmatiki Leksika	5
1.8.1 Semantiki Leksika	5
1.8.2 Michakato ya Pragmatiki leksika	6
1.9 Ubanaji wa kileksika.....	6
1.10 Upanuzi wa Kileksika	7
1.11 Kisio la maana.....	7
1.12 Kwa nini Pragmatiki Leksika?.....	8
1.13 Yaliyoandikwa	9
1.13.1 Yaliyoandikwa kuhusu Nadharia ya Utafiti	9
1.13.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ya Utafiti.....	15
1.14 Mbinu za Utafiti.....	20
1.14.1 Mbinu za Kukusanya Data	20
1.15 Uteuzi wa Sampuli.....	20
1.16 Uchanganuzi na uwasilishaji wa Data	21
1.17 Muhtasari wa Sura	21

SURA YA PILI : MITAZAMO YA KIPRAGMATIKI NA MIFUMO YA FACEBOOK... 23

2.0 Utangulizi.....	23
2.1 Historia na Mifumo ya Mawasiliano ya Jukwaa la Facebook	23
2.2 Sifa za Lugha ya Jukwaa la Facebook	25
2.2.1 Usilabishaji.....	25
2.3 Sifa za mkutano duara au kikongamano	26
2.4 Matumizi ya lugha ya Kiswahili.....	27
2.5 Kuchanganya Msimbo	27
2.6 Matumizi ya vifupisho	29
2.7 Matumizi ya Ikonihisi na picha.....	30
2.8 Msimulizi wa hadithi Anayeonekana.....	31
2.9 Dhana ya pragmatiki.....	33
2.10 Kubanika kwa maana ya neno	34
2.11 Kupanuka kwa maana ya neno	36
2.12 Semantiki leksika	38
2.13 Lugha na mawasiliano	38
2.13.1 Mtungaji ujumbe	39
2.13.2 Njia ya mawasiliano	39
2.13.3 Mpokeaji ujumbe.....	39
2.13.4 Muktaadha.....	39
2.13.5 Lugha na muktaadha	39
2.14 Hitimisho.....	41

SURA YA TATU : UPANUZI WA MAANA KATIKA MAWASILIANO YA FACEBOOK..... 42

3.0 Utangulizi.....	42
3.1 Upanuzi wa kileksika katika mawasiliano	43
3.2 Hitimisho.....	63

SURA YA NNE : UBANAJI WA MAANA NA KISIO LA MAANA KATIKA MAWASILIANO YA JUKWAA LA FACEBOOK..... 64

4.0 Utangulizi.....	64
4.1 Ubanaji wa kileksika na kisio la maana katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook	64
4.2 Hitimisho.....	89

SURA YA TANO : HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....	90
5.0 Utangulizi.....	90
5.1 Kutathmini Ufanisi wa Malengo ya Utafiti	90
5.2 Changamoto za Utafiti	94
5.3 Mapendekezo	95
MAREJELEO	96
VIAMBATANISHO	99
Kiambatanisho cha kwanza.....	99
Kiambatanisho cha pili	112
Kiambatanisho cha tatu.....	115

SURA YA KWANZA

MSINGI WA UTAFITI

1.0 Utangulizi

Mawasiliano ni kiungo muhimu sana katika jamii yoyote ile, ambapo lugha ni kiungo cha muhimu sana katika mawasiliano. Binadamu ameweza kubuni mbinu kadha wa kadha za kumwezesha kukidhi mahitaji yake ya kimawasiliano. Miongoni mwa njia za mawasiliano ni pamoja na kuzungumza moja kwa moja kwa matumizi ya mdomo, kuwasiliana kwa matumizi ya ishara na kuwasiliana kwa lugha ya kimaandishi. Utafiti huu umelenga mawasiliano ya kimaandishi ambapo teknolojia imekuwa kiungo muhimu cha mawasiliano. Watafiti watangulizi wameweza kufanya tafiti mbalimbali katika uwanja huu wa mawasiliano ikiwemo tafiti kuhusu sifa na sajili za lugha ya Kiswahili katika mitandao ya kijamii kama vile: Twita, Facebook na WhatsApp. Katika utafiti huu tunalenga kufanya uchanganuzi kuhusu suala la maana ya kipragmatiki ya mawasiliano katika jukwaa la Facebook. yaani, maandishi ya jukwaa la Facebook kwa kujikita kwa nadharia ya pragmatiki leksika, ambapo Kwa ufahamu wetu hakujakuwa na utafiti ambao umefanywa katika lugha ya Kiswahili kwa matumizi ya nadharia ya pragmatiki leksika ya Reinhard Blutner (1990) Kwa kuchunguza suala la maana ya kipragmatiki ya mawasiliano ya jukwaa la Facebook.

Facebook Kama nyenzo ya mawasiliano inaafiki malengo ya wanajamii katika kudumisha haja zao za kila siku za kimawasiliano kwani, Ni mtandao ambao umefaulu katika kuunganisha walimwengu kote duniani. Hata hivyo, mtandao huu una athari chanya pamoja na athari hasi kwa watumizi wake.

Suali la kujiuliza hapa ni kuwa, lugha ambayo inatumika katika nyenzo hii ya kimawasiliano ina maana gani kipragmatiki? Na iwapo ina maana ya kipragmatiki ni jinsi gani lugha inayotumika katika jukwaa la Facebook husimbwa.

Kwingineko tunazidi kujiuliza kuwa, iwapo kuna usimbwaji wa lugha katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook, wawasilianaji huisimba lugha yao ya kimawasiliano kwa matumizi ya mikakati ipi? Masuala haya yataweza kupata ufafanuzi kupitia Kwa utafiti huu ambapo nadharia ya pragmatiki leksika itatuongoza.

Blutner ambaye ndiye mwasisi wa nadharia ya pragmatiki leksika (1990), anatupa michakato inayotumika kufafanua maana ya kipragmatiki kama vile: ubanaji na usimbwaji wa kimaana, kisio la maana na upanuzi wa maana. Lugha inayotumika katika jukwaa la Facebook huibua matumizi ya miundo mbalimbali ambapo kutokana na miundo hiyo maana mpya huweza kuibuka.

Wamitila (2003), anatupatia ufafanuzi wake kuhusu muundo kuwa, ni umbo la kitu kuhusiana na namna kilivyotengenezwa. Anaendelea kuongezea kwamba, muundo tena ni jinsi ya kutengeneza kitu. Nayo maana ni ufafanuzi wa neno ama wa jambo fulani. Pia ni maelezo yanayoweka wazi tafsiri au ufafanuzi, isitoshe maana tena ni faida au manufaa ya kitu au jambo. Hivyo basi utafiti huu unalenga kujishughulisha na maana kama ufafanuzi wa neno au jambo fulani jinsi limetumika kimawasiliano. Kundi mahsusi kama vile vijana wana mazoea ya kuwasiliana kutumia sentensi fupifupi na vifupisho lakini wazee hujikita kwa matumizi ya sentensi ndefu zilizokamilika ili kuweza kuziba mianya ya kiimplikecha katika ujumbe wanaokusudia kuupasha kwa hadhira lengwa, kwingineko jamii ya wasomi nayo huweza kuwasiliana kwa kujikita kwenye miundo ya lugha ya kiusomi huku wakilenga kuibua maana iliyopanuliwa katika kufasiri ujumbe uliowasilishwa kimawasiliano. Hii ndio maana utafiti huu umechochewa kuuziba mwanya huu wa kiusomi kwa kufanya uchanganuzi na uchanganuaji wa maana ya kipragmatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook kwani, ni nyenzo ya kimawasiliano iliyovutia mahuluki luluki chungu nzima kote ulimwenguni.

1.1 Tatizo la Utafiti

Jukwaa la Facebook limeweza kuvutia watafiti wengi ambao wameweza kufanya utafiti wao kuhusu sifa za mazungumzo ya jukwaa hili, athari ya Facebook kwa jamii husika haswa vijana na umuhimu wa lugha ya jukwaa hili katika jamii. Haswa, tafiti zao zikiegemea umaanisho kwa matumizi ya nadharia ya Umaanisho ya Grice (1975) ambayo inasisitiza ushirikiano katika kuleta mwamana katika mawasiliano, kwa kutumia kanuni za mawasiliano kama masharti ya mawasiliano. Uwanja wa Facebook ungali unahitaji kueleweka Suala la maana ya kipragmatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook hata Zaidi kuhusiana na namna watumizi wake husimba maana. Ni tafiti chache sana ambazo zimegusia suala la maana ya mawasiliano ya jukwaa la Facebook hasa tafiti hizi zikijikita katika lugha ya Kiingereza. Mpaka sasa hakuna utafiti wa kutosha ambao umefanywa kuhusu suala la maana ya kipragmatiki katika mawasiliano ya lugha ya Kiswahili katika jukwaa la Facebook. Ni kutokana na kuwepo kwa mwanya huu wa ukosefu wa utafiti kuhusu maana ya kipragmatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook ambapo utafiti huu unapata msingi wake.

1.2 Malengo ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza suala la maana ya kipragmatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook. Malengo maalum ni,

- i) Kubainisha maana ya kipragmatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook.
- ii) Kujadili mikakati ya usimbwaji na upanuzi wa maana
- iii) Kujadili mikakati ya ubanaji wa maana ya lugha inavyotumika katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook.

1.3 Maswali ya Utafiti

- i) Je, lugha inayotumika katika jukwaa la Facebook inatumika kwa maana gani kipragmatiki?
- ii) Je mikakati ya ubanaji hudhihirika vipi?
- iii) Mikakati ya upanuzi hudhihirika vipi?

1.4 Upeo na Mipaka

Utafiti huu unatazamiwa kujikita katika maandishi ya jukwaa la Facebook pekee wala si mitandao mingine ya kijamii kama vile Twita na WhatsApp. Pia, utafiti wetu utajikita kwenye uchanganuzi wa maana ya kipragmatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook wala si

masuala mengine kama vile; iktisadi ya maneno na mengineyo. Mtafiti atazuru kurasa za wanafunzi wa chuo kikuu ambao huwasiliana kupitia jukwaa la Facebook wala si kurasa za watu wote. Isitoshe, wanafunzi ambao tutazuru kurasa zao ni wale wanaotumia lugha ya Kiswahili kama lugha ya mawasiliano pekee na pia wale ambao tutakuwa tumepata idhini kutoka kwao wala si wanafunzi wowote tu wa chuo kikuu. Isitoshe, habari zilizochapishwa na tasnifu ambazo zimeweza kuchapishwa na zile ambazo hazijachapishwa zitakazotumika katika utafiti huu ni zile zinazo jihusisha na masuala kuhusu mitandao ya kijamii na pia kazi zinazojihusisha na nadharia yetu ya utafiti ambayo ni nadharia ya pragmatiki leksika ya mwanaisimu Reinhard Blutner (1990) pekee.

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utaweza kuwarahisishia kazi wasomi wa isimu ya lugha katika somasoma zao kwa kuwapa makala ya urejelezi wa maana ya kipragmatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook. Kwingineko, utafiti huu utafungua ukurasa mpya wa tafiti za maana inayoibuliwa na waandishi wa makala katika mitandao mingine ya kijamii kama vile: Twita na WhatsApp kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili kwani, utafiti huu umekuwa kama msingi wa tafiti zinginezo. Pia, utafiti huu utawafaa watafiti wengine na wanajamii kwa ujumla kwa kutoa maana ya kipragmatiki ya lugha inayotumika kimawasiliano katika jukwaa la Facebook. Kwingineko, mawasiliano yanapochukua mwelekeo wa matumizi ya lugha kulingana na masiala mbalimbali kama vile; jamii, masiala ya vyeo, masiala ya kitaaluma, masiala ya mbari na miko na masiala ya umri.

Wawasilianaji huweza kutumia lugha kwa njia tofauti kimuundo. Hivyo basi utafiti huu utaweza kuleta mwanga na kufafanua ni kwa nini mawasiliano ya jukwaa la Facebook huweza kuchukua miundo hiyo na kuweza kuleta maana tofauti ambayo ni lazima iweze kufasiriwa kimuktadha ndiposa maana hiyo iweze kueleweka sawasawa.

1.6 Msingi wa Nadharia

Utafiti huu utaendelezwa na Nadharia ya Pragmatiki leksika ya Reinhard Blutner (1990) ambayo iliasisiwa katika Jarida la Semantiki. Nadharia hii inazungumzia mpangilio na ufafanuzi wa fenomena za kipragmatiki ambazo zinaambatanishwa na semantiki chini ya vipashio vya kileksika. *Reinhard Blutner* anatoa mtazamo wake kuhusu lugha kuwa vipashio vya lugha vinachanganuliwa Kwa njia maalum kulingana Na muktadha wa matumizi ya lugha.

Lugha yaweza kupanuliwa au kusimbwa. Pia, lugha yaweza kuwa na miundo ya sentensi sahili, lugha yaweza kuwa na vifupisho au michoro ambayo inaashiria ishara ya ujumbe fulani. Ni Kwa msingi huu ambapo utafiti huu unajikita kwa Nadharia hii ya Pragmatiki lekiska ya *Blutner*. Nadharia hii ilipata msingi kupitia Kwa nadharia ya Umaanisho ambayo iliasisiwa na Grice (1975) ambaye aliweza kuzua utaratibu wa ushirikiano katika mawasiliano katika nadharia yake ya Umaanisho. Mawazo ambayo pia yatakuwa na mchango mkuu katika utafiti huu.

1.7 Nadharia ya Pragmatiki leksika ya Blutner Reinhard

Nadharia hii iliasisiwa na Blutner Reinhard mwaka wa (1990) na baadaye ikaendelezwa na Wilson (2003) kwenye mihadhara yake katika chuo kikuu cha Havard lakini pia iliendelezwa na Wilson akiwa pamoja na Carson (2007) katika miaka ya baadaye. Nadharia hii inajikita katika uchanganuzi wa mageuzi ya maana katika muktadha. Yaani maana za maneno kusimbwa, kubanika, kupanuliwa na kukisiwa. Kulingana na majukumu haya kinadharia, nadharia hii ni faafu katika utafiti huu wa kuchanganua maana ya kipragmatiki ya lugha katika jukwaa la Facebook.

Pragmatiki leksika inatutolea maelezo kuwa, faridi za kileksika za lugha zinachanganuliwa kiutaratibu na kufasiriwa kulingana na muktadha mahususi wa kimawasiliano.

Mchango wa Semantiki katika ufasiri wa maana ya kijumla ya neno unabanwa kuliko ilivyodhaniwa awali kwani pragmatiki leksika inafafanua na kuelezea fenomena za kipragmatiki ambazo zimeshikamana na semantiki chini ya elementi za kileksika.

1.8 Mihimili ya Nadharia ya Pragmatiki Leksika

1.8.1 Semantiki Leksika

Semantiki leksika inashughulika na dhana ya neno haswa fahiwa ya kimsingi.

Maneno huweza kuchukuliwa kwa minajili ya kuonyesha kitu Fulani kutegemea mtazamo mahususi wa semantiki leksika. Tetezi za Mmbawanga (2010), ni kuwa, vitengo fahiwa katika semantiki leksika ni vitengo vya kileksika ambavyo kwavyo mzungumzaji huweza kuongezea kwa mfululizo katika maisha pamoja na ujifunzaji wa dhana ya maneno mapya na fahiwa yake.

Mhimili huu utakuwa wa msaada mkuu kwa utafiti huu kisa na maana ni kuwa utatuwezesha kupata maana msingi ya neno ndiposa tuweze kuangazia maana iliyosimbwa kisemantiki, maana

iliyobanwa, maana iliyopanuliwa na maana inayoweza kukadiriwa kulingana na muktadha wa mazungumzo na pia kuchunguza muundo unaotumika katika lugha kimawasiliano.

1.8.2 Michakato ya Pragmatiki leksika

Tukimrejelea Blutner (2011), mambo ya kimsingi yanayoshughulikiwa katika pragmatiki leksika akiwarejelea Wilson (2003) na Carson (2002), yanaweza kugawika katika mambo matatu ambayo ni ya kimsingi yatakayotumika katika uchanganuzi wa fahiwa ya kipragmatiki ya lugha inayotumika katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook ni kama yafuatayo:

- a. Usimbwaji wa maana,
- b. Upanuzi wa maana,
- c. Kukisia kwa maana.

1.9 Ubanaji wa kileksika

Kolaiti na Wilson (2012), wanatupasha habari kuwa, ubanaji wa kileksika ni mchakato ambao unajihusisha na matumizi ya neno au kirai katika kuonyesha dhana mahususi zaidi ya maana iliyosimbwa kiisimu. Utafiti huu unakubaliana na ufafanuzi huu na kushadidia kuwa maana pana ya neno ndiyo iliyosimbwa kiisimu kwani wakati ubanaji wa maneno kimuundo na kimaana unafanywa, tunapata dhana ndogo katika muktadha wa mazungumzo.

Maana inayojitokeza hususan ni sehemu ya maana ya maana pana iliyosimbwa.

Horn na Ward (2004), wanafafanua dhana ya ubanaji wa kileksika kwa kutupa mwanga kuwa ubanaji ni wa kiwango kikubwa kwani, ni mchakato ambao unaweza kusawasishwa na hutegemea muktadha unaohusika. Maana iliyosimbwa inaweza kubanwa katika fahiwa tofauti kutegemea muktadha wa kimawasiliano

Mfano ni; Katui ana Kiswahili. Neno Kiswahili lina maana pana kwani laweza kumaanisha kuwa mtu huyu ni mzungumzaji mwema wa lugha ya Kiswahili, ni mjanja au ana ufasaha katika somo la Kiswahili pia ni mjuzi wa masuala Fulani kwa hivyo ni lazima maana iliyosimbwa katika mawasiliano iweze kufasiriwa kimuktadha. Katika upanuzi wa maana vipashio vya leksimu vyaweza pia kuongezewa au kufupishwa kwa kuondoa leksimu zingine hivyo basi mchakato huu huweza kubadili miundo na maana ya lugha husika inayotumiwa katika mawasiliano. Kulingana na Blutner (1998), ubanaji ni hali ya mzungumzaji kutumia faridi za kileksika kupitisha maana ambayo imebanwa kuliko ile maana ambayo imesimbwa kisemantiki. kwa mfano kisemantiki, Kiswahili ni lugha mojawapo kati ya lugha nyinginezo ulimwenguni na

pia Kiswahili ni neno ambalo lina maana ya somo mojawapo katika mtalaa wa kielimu ulimwenguni. Mawazo haya yatakuwa muhimu sana katika kuchanganua maana ya kipragmatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook.

1.10 Upanuzi wa Kileksika

Fromkin na Rodman (1978), wanatujaza kuwa, upanuzi wa kileksika ni mchakato ambao kwao dhana ya neno hupanuka kwani, neno linamaanisha kila kitu kilichokuwa kikimaanishwa na kuweza kuongeza fahiwa nyingine kwa hiyo; fahiwa ya neno hupanuka. Kwani, neno linamaanisha kila kitu kinachokuwa kikimaanishwa na kuongeza maana nyingine.

Utafiti huu unakubaliana na maelezo haya na pia kuleta mchango wake kuwa kando na kupanuka kimaana kwa neno, miundo na maana ya maneno katika lugha ya kimawasiliano huweza kufasiriwa kivingine kwani miundo hii huweza kuleta mageuzi ya kisintaksia, na kimofolojia kwa minajili ya kuleta maana pana ambayo mwasilishaji wa ujumbe huwa amekusudia katika muktadha wa kimatumizi. Kwa mfano, matumizi ya neno shingo yaweza kupanuliwa kumaanisha naibu wa mkuu katika taasisi au idara Fulani kimamulaka au katika mazingira ya usimamizi wa kazi Fulani.

Hapa panahitaji matumizi ya sentensi changamano ili kuweza kueleza ufahamu wa matumizi ya neno hili. Pia, neno hili shingo laweza kutumika kimuktadha kumaanisha kitu kinachoshikilia kingine. Mfano katika sentensi ni kama vile: John na Amos ni shingo langu.

Kumaanisha kuwa mzungumzaji huwa anashikiliwa na John pamoja na Amos, kwani bila wao hawezi kusimama. Lakini matumizi ya neno hili kisemantiki leksika ni kuwa maana yake ni sehemu ya mwili inayoshikilia kichwa.

Jeffers na Lehiste (1979), wanafafanua upanuzi wa dhana kuwa, upanuzi wa fahiwa ya maneno huwa unatokana na kujumuisha hali mahususi inaoshiriki. Hii ni kwa sababu, majina ya kipekee huwa yanajitokeza kwa kurejelea jamii ya kijumla ya ile fenomena.

1.11 Kisio la maana

Haya ni aina ya mageuzi ya maana ambayo kwayo leksimu zilizo thabiti kwa njia fulani hupanuliwa mwishoni na kujumuisha mawanda ya makundi ambayo kwa yakini yanapatikana nje ya maana yake kamilifu kiisimu. Wilson (2003), katika tetezi zake anatumieza kuwa, mifano mizuri ni kama vile: matumizi ya kilegevu ya takwimu za kukadiria, maneno yanayokadiria kimaeneo na msamiati ambao unafanuliwa kwa njia ambayo ni ya ukanusho. Kimsingi, fahiwa

ambazo zinapanuliwa ndizo zinawasilishwa na wasemaji katika usemi huku dhana thabiti za leksimu zikiwa ndizo ambazo zimesimbwa kisemantiki na neno lilo hilo.

Marisya (2017), naye anatuelezea kwamba, ukadiriaji wa fahiwa ni hali ambayo ufasiri wa neno ambalo lina dhana finyu hupanuliwa ili kuhusiana na dhana ya kitu ambacho kina maana tofauti na maana halisi ya neno hilo kiisimu. Kwa mfano, neno sindano jinsi linavyotumiwa kurejelea ugonjwa wa ukosefu wa kinga mwilini kwa mojawapo ya mawasiliano katika kikundi cha wanafunzi wa chuo kikuu cha Facebook. Hii ni kwa sababu binadamu ambaye anaugua uwele huu wa ukimwi huwa anakonda na kukondeana mithili ya ng'onda na kuwa mwembamba mithili ya sindano.

Katika mageuzi haya, dhana ambayo inawasilishwa na neno Fulani huwa inajitenga zaidi kutoka kwa ile fahiwa ambayo imesimbwa kama ambayo inapatikana katika upanuzi wa kiistiari.

Mfano: staftahi imeletwa kuchelewa, leo asubuhi ni siku nzima, inaonekana siku hii si kama siku nyingine. Asubuhi ni wakati thabiti lakini hapa mzungumzaji anachukulia kuwa wakati wowote chai ikiandaliwa ni asubuhi.

Hivyo basi maana hii imejitenga na maana ya neno asubuhi kisemantiki kwani, neno asubuhi limetumiwa hapa kwa njia ambayo ni tepetevu.

Michakato hii ni ya muhimu kwa utafiti huu kisa na maana ni kuwa inatupa mwafaka bayana kuhusu maana ya kipragmatiki ambayo tunakusudia kuchanganua katika lugha inaotumiwa katika Facebook ikiwa ni nyenzo mojawapo ya mawasiliano.

1.12 Kwa nini Pragmatiki Leksika?

Nadharia hii ni faafu kwa utafiti huu kwa sababu, itaweza kutuonyesha jinsi msemaji ana uhuru wa kutumia maneno kwa jinsi mbalimbali kutegemea muktadha kwani, mnenaji anaweza kutumia upanuzi wa leksimu, ubanaji au ukadiriaji wa maana. Pia nadharia hii itatuwezesha kufanya ugunduzi kuwa msemaji anaweza kusetiri ujumbe wa mawasiliano ili uwafikie wasikilizaji ambao ni wa lengwa tu. Isitoshe, kupitia kwa nadharia hii, tutaweza kupata utambuzi kuwa mzungumzaji huweza kuficha ukali wa maneno kama vile katika matumizi ya maneno ya lugha mwiko.

1.13 Yaliyoandikwa

1.13.1 Yaliyoandikwa kuhusu Nadharia ya Utafiti

Katika somasoma zetu, tuliweza kubainisha kuwa wasomi mbalimbali wameweza kutoa mawazo mzomzo kuhusu lugha ya kimawasiliano ambayo yanaenda sambamba na nadharia hii ya pragmatiki leksika ya Reinhard Blutner (1990), ambayo ni nadharia inayotuongoza kwa utafiti wetu kama ifuatavyo; Bloomfield (1930), anajadili aina mbalimbali za mageuzi katika fahiwa. Katika maelezo yake, anataja upanuzi wa kimaana, upanuzi wa kiistiari na upanuzi wa chuku miongoni mwa mabadiliko mengine.

Mwanazuoni huyu anaendelea kwa kudai kuwa, kila mageuzi ya kidhana huwa yanaathiri maneno mengine katika vikoa vya maana. Mawazo haya yatakuwa na msaada mkuu kwa utafiti huu kwani yatatupa mwanga kuhusu maana ya kipragmatiki katika lugha itumikayo katika mawasiliano ya mtandao wa kijamii wa Facebook ambayo ni mojawapo ya nyenzo za mawasiliano katika jamii ya kisasa iliyopata mwanga wa teknolojia.

Tofauti na utafiti wetu ni kuwa, Bloomfield alishughulikia aina mbalimbali za mabadiliko katika maana lakini utafiti huu nao unajikita kwa maana ya kipragmatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook.

Carson, (2002), alifafanua mihimili ya nadharia ya pragmatiki leksika ambapo mihili ndiyo nguzo za kinadharia. Haswa namna msikilizaji anavyojenga dhana ya dharura. Kuongezea, aliweza kufafanua michakato ya pragmatiki leksika kama vile: ubanaji wa kileksika, upanuzi wa kileksika. Bila kusita amefafanua upanuzi wa kiistiari kwa kuonyesha namna fahiwa ya maneno inavyosimbwa na jinsi ambavyo sitiari huweza kusimbuliwa na msikilizaji wa ujumbe huo kimawasiliano.

Mawazo ya Carson (2002) ni ya muhimu katika utafiti huu maadamu yatatuwezesha kupata uelewa wa michakato ya pragmatiki leksika. Kwingineko, mawazo haya yatatuwezesha kuitumia michakato ya pragmatiki leksika katika uchanganuzi wa maana ya kipragmatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook.

Kolaiti na Wilson (2012), wanafafanua dhana ya ubanaji wa kileksika kuwa ni mchakato ambao unahusu matumizi ya neno au kipashio cha sentensi kiitwacho kirai katika kuonyesha dhana mahsusi zaidi ya fahiwa iliyosimbwa ya kiisimu. Mchango wa wanazuo hawa unakubaliana na mawazo ya Blutner ambaye ndiye mwasisi wa nadharia tunayojikita kwayo katika utafiti huu.

Hivyo basi, utafiti huu unakubaliana na kushadidia kuwa maana pana ya neno ndiyo iliyosimbwa kiisimu kwani, wakati ubanaji wa maneno kimuundo na kimaana unatekelezwa, ambapo tunapata dhana ndogo katika muktadha wa mazungumzo au mawasiliano. Maana inayojitokeza hususan ni sehemu ya maana pana iliyosimbwa.

Horn na Ward (2004), wanatoa mchango wao wa kiisimu kuwa, ubanaji ni mchakato wa kiwango kikubwa kwani ni mchakato ambao unaweza kusawasishwa kutegemea na muktadha wa matumizi lugha. Mawazo haya yanashabiana na mawazo ya Blutner katika nadharia yake ya Pragmatiki leksika ambayo ni nadharia inayotuongoza katika utafiti huu kwa hivyo ni mawazo yaliyo na faida kuu katika utafiti huu wa maana ya kipragmatiki ya mawasiliano katika jukwaa la Facebook.

Jeffers na Lehiste (1979), wanatoa madai kuhusu upanuzi wa fahiwa kileksika kuwa, upanuzi wa dhana mara nyingi huwa unatokana na kujumuisha hali mahsusi hadi katika jamii ambayo ile hali mahsusi hushiriki. Hii ni kwa sababu nomino za kipekee mara nyingi huwa zinajitokeza jamii husika inaporejelewa kwa kijumla kwazo hizo fenomena.

Japo wataalam hawa walitoa kauli zao kuhusu upanuzi wa kimaana kwa mtazamo mwingine, lakini yanakubaliana na mawazo ya Rein Hard Blutner kwa hivyo mawazo ya wanaisimu hawa wawili ni ya muhimu sana katika utafiti wetu wa uchanganuzi wa maana ya kipragmatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook.

Kulingana na tetezi za Yule (2003), nadharia ya Umaanisho inatupaa maelezo yafuatayo kuhusu masuala ya kimsingi yanayohusu Pragmatiki leksika.

Nadharia hii inasema kuwa, michakato ya kipragmatiki unasababishwa na utafutaji wa umaanisho katika matamshi ya kimawasiliano pamoja na maneno ya lugha yaliyotumika, michakato hiyo hujukua njia ya mikakati michache na hutekeleza majumu yake kupitia kwa uelewano wa kijamii kimuktadha au kimandhari na viathirifu vya kiutambuzi na hukatzwa wakati matarajio yaliyoleta umaanisho katika mazungumzo yametimizwa au yametupiliwa mbali. Mawazo haya ni ya faida kwetu katika utafiti huu, kwani yatatupa mwangaza kuhusu michakato ya kipragmatiki na kisha kutuwezesha kupata uelewa wa matumizi ya nadharia ya utafiti wetu.

Yule (1996) anaendelea kwa kutoa maelezo kuwa, lugha huchanganuliwa ikiwa kwenye muktadha wa mawasiliano. Kulingana na mawazo yake, muktadha ni hali ya kimaandhari ambapo usemi wa kimawasiliano umetolewa.

Mawazo ya Yule (1996), yanamuwala na mawazo ya Blutner (1990) ambayo yanahusu maana ya kipragmatiki kwa hivyo, ni ya muhimu sana katika kufanikisha utafiti wetu wa maana ya kipragmatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook.

Ohly (1977), aliweza kutoa baadhi ya ruwaza za kuanzisha misamiati mipya katika lugha ya Kiswahili. Kwa kutanguliza, alitoa ufafanuzi wa ukopaji wa maneno halafu akaangazia uundaji wa maana geni ambayo inaweza kuwa uundaji wa maneno mapya kikamilifu au kwingineko maneno ambayo yalikuwepo kuidhinishwa kwa maana mpya na kupewa mawanda ya kisemantiki ya kipekee au kutumia makundi ya kisintaksia ambayo yana kijalizo, Mawazo haya yanaleta mshikamano na mawazo ya mwasisi wa nadharia ya pragmatiki leksika ambaye ni Reinhard Blutner. Hata hivyo utafiti wetu pia unakubaliana na ufafanuzi huu madhali nyakati hizi leksimu ambazo zinaundwa hupata maana mpya na miundo mipya kimofolojia na kifonolojia. Hivyo basi mawazo ya mtalaamu huyu ni ya muhimu kwa utafiti wetu wa maana ya kipragmatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook.

Jefwa. M. (2010) anatoa madai kuwa uundaji wa maneno ni uambatanishaji wa mofimu moja au zaidi kufikia kiwango cha mofimu hizo kwa pamoja, huweza kuleta maana kwa pamoja kileksika katika lugha yoyote ile. Utafiti huu unakubaliana na mawazo ya msomi huyu kwani, lugha ya mtandao huwa inachukua miundo mipya ya maneno na kuleta maana mpya kileksika.

Ingawaje wataalam hawa wanauangalia upanuzi wa maana na matumizi ya lugha kimuktadha kwa kutumia mitazamo tofauti tofauti, inajitokeza kuwa wote wanajifunga na mkabala wa kiufafanuzi na kikaida katika kulikabili suala la miundo na maana ya lugha.

Wa aidha mitazamo yao ni tofauti lakini wote wanaelekea kukubaliana kuhusu suala moja kuwa, miundo na maana ya lugha hujitokeza kulingana na hali mbalimbali katika mawasiliano au matumizi lugha. Kuna watafiti ambao wametumia nadharia ya pragmatiki leksika ya Blutner (1990) kuchunguza suala la maana ya lugha katika kuchanganua matini mbalimbali. Kwa mfano,

Wambugu (2010), katika uchanganuzi wake anaangazia mageuzi ya kidhana katika leksimu za jamii ya Akikuyu kwa kutumia mtazamo wa Pragmatiki leksika kwa kutoa ufafanuzi wa dhana ya ziada ambapo kwazo leksimu hizi zimepokea.

Utafiti huu ni wa muhimu katika utafiti wetu kwa sababu, msomi huyu aliweza kutafiti kwa kujikita kwa nadharia ya pragmatiki leksika ambayo ndiyo nadharia itakayotumika kwa utafiti wetu wa maana ya kipragmatiki katika lugha ya mtandao wa kijamii wa Facebook. Tofauti kati ya utafiti wetu na utafiti wa msomi huyu (Wambugu) ni kwamba, yeye aliangazia mabadiliko ya kidhana katika leksimu ya lugha ya kikuyu nasi tunachanganua fahiwa ya kipragmatiki katika lugha ya jukwaa la Facebook. Isitoshe wambugu aliweza kujikita tu kwa lugha ya jamii ya Akikuyu suala ambalo haliendi sambamba na utafiti wetu kwani sisi tunaangazia maana ya kipragmatiki ya lugha inayotumika katika mawasiliano ya mtandao wa kijamii wa Facebook bila kuzingatia jamii yoyote. Pia utafiti wa Wambugu ulihusu lugha ya kimazungumzo bali si lugha ya kimaandishi.

Blank (1998) naye alitafiti kuhusu hali mbalimbali zinazosababisha mageuzi ya maana katika maneno. Katika tafiti zake aliweza kubaini kuwa, mageuzi ya kimaana yanaweza kusababishwa na masuala ya kiisimu katika lugha inayohusika.

Anaendelea kudai kuwa, maneno yanaweza kutumika katika miktadha mbalimbali ili kuibua maana tofauti ambayo msemaji ananua kuwasilisha.

Kuongezea, Blank anatoa ufafanuzi kuwa, hali za kimawazo au kiakili ambazo huweza kuvuruga namna ambavyo, watu au binadamu huwa wameteua na kutumia maneno katika lugha na kutegemea chukulizi zao kuhusu maneno hayo kwani, mzungumzaji anapona kuwa neno Fulani ni kunyume cha maadili ya kijamii atatumia lugha ya upole katika kuwasilisha ujumbe wake.

Utafiti huu wa Blank ni wa msaada mkuu kwa utafiti wetu mbao unahusu maana ya kipramatiki ya lugha katika jukwaa la Facebook kwa sababu utatupa mwongozo jinsi nadharia ya pragmatiki leksika inavyotumika katika ufasiri wa miundo na maana katika lugha ya kimawasiliano.

Tofauti na utafiti wetu ni kuwa, Msomi huyu alitafiti kuhusu hali ambazo husababisha mageuzi ya kimaana katika maneno ya lugha lakini utafiti wetu unahusu maana ya kipragmatiki ya lugha inayotumika katika mawasiliano ya mtandao wa kijamii wa Facebook bali si hali zinazosababisha mabadiliko katika maana ya lugha.

Habwe (1999) alitafiti kuhusu diskosi ya hotuba za kisiasa kwa kujikita katika nadharia ya Grice (1975) miongoni mwa nadharia nyinginezo.

Msomi huyu aliweza kuchunguza na kufanya uchanganuzi jinsi ambavyo implikecha hukarabatiwa kwa kufasiri dhana iliyokitwa kwenye matamshi ya wanasiasa.

Japo Habwe hakuongozwa na nadharia ya pragmatiki leksika, tumeweza kusoma kazi yake na kuiona kuwa ni ya manufaa kwa utafiti huu kwani, nadharia ya umaanisho ya Grice ndiyo iliwekea nadharia yetu ya utafiti jiwe la msingi. Isitoshe, utafiti huu ni wa muhimu katika utafiti wetu kwani utatuwezesha kutambua maana ya kipragmatiki iliyokitwa katika mawasiliano kimuktadha na pia ni kwa nini maana hiyo katika mawasiliano hayo? Utafiti huu wa Habwe (1999), ni tofauti na utafiti wetu yamkini kwa sababu Habwe aliweza kutafiti kuhusu diskosi ya mazungumzo ya siasa kwa mtazamo wa nadharia ya Grice ya implikecha (1975), miongoni mwa nadharia nyinginezo ilhali utafiti wetu unachunguza maana ya kipragmatiki ya lugha inayotumika katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook kwa mtazamo wa nadharia ya pragmatiki leksika ya Blutner (1990).

Mkude (1995) anafanya uchanganuzi wa dhana ya maneno ambayo yana fahiwa sawa kwa kuisitiza haja ya kuangalia muktadha, anadai kuwa muktadha waweza kuunganisha maneno au vipashio vya sentensi vinavyoitwa virai ambavyo huwezi kutegemea kuwa vinaweza kuwa visawe vya aina moja.

Mkude anaendelea kwa kutoa mfano mzuri wa kutoka sentensi “Aliingia kwa tabasamu iliyong’aa wajihini” fahiwa ya neno iliyong’aa wajihini ni kama ifuatavyo: iliyometameta usoni, iliyoangaza usoni, iliyomulika usoni, iliyowaka usoni, iliyovutia usoni au iliyowaa usoni.

Hivyo basi bila muktadha ni vigumu kuweza kubaini visawe vya neno ng'aa jinsi lilivyotumika katika mawasiliano.

Utafiti wa Mkude utakuwa wa msaada mkuu kwa utafiti wetu kwa sababu utatupatia mwangaza kuhusu matumizi ya maneno kimuktadha.

Muyuku (2009) alifanya utafiti kuhusu jinsi uchanganyaji lugha hujitokeza katika matangazo ya benki ya Commercial pamoja na mawasiliano ya simu tamba au rukono kwa matumizi ya nadharia ya pragmatiki leksika ambapo aliweza kufua dafu kwa ufafanuzi wake ambao ulihusu kusimbwa na kusimbuliwa kwa dhana ili kuwavutia na kuwashawishi wateja. Mtafiti huyu aliweza pia kubaini au kutambua kuwa lugha ya Kiswahili ilikuwa kati ya lugha zilizotumiwa kwa wingi. Utafiti huu ni wa muhimu kwetu kwani, utaweza kutupa ufafanuzi jinsi maneno ya lugha ya kimawasiliano huweza kusimbwa na kusimbuliwa na pia kazi hii ya Muyuku itatupa mwongozo jinsi ya kuendesha utafiti kwa mtazamo wa nadharia ya pragmatiki leksika.

Utofauti uliyopo kati ya utafiti wetu na utafiti wa Muyuku ni kuwa, mtafiti huyu aliweza kutafiti kuhusu namna uchanganyaji lugha hujitokeza katika matangazo ya benki ya Commercial na mawasiliano ya simu tamba kwa kujikita katika nadharia ya pragmatiki leksika lakini utafiti wetu nao unahusu maana ya kipragmatiki ya lugha katika jukwaa la Facebook.

Ochoki (2010) alifanya utafiti wake kuhusu usimbwaji wa fahiwa katika nyimbo za Hip hop zinazoimbwa nchini Kenya kwa kutumia michakato ya upanuzi na ubanaji wa fahiwa katika kufafanua usimbwaji wa kimaana. Utafiti huu ni wa msaada katika tafiti zetu kwa sababu utatuwezesha kutoa mwongozo kuhusu lugha inavyosimbwa katika mawasiliano. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa, utafiti wa msomi huyu ulichunguza namna dhana zinavyosimbwa katika nyimbo za Hip hop nao utafiti wetu utaweza kuchanganua maana ya kipragmatiki ya lugha katika jukwaa la Facebook.

Ochichi (2013) alitafiti kuhusu usimbwaji na umaanisho wa dhana kimazungumzo katika lugha ya Egegusi na lugha ya Kiswahili kwa mtazamo wa nadharia ya pragmatiki leksika na kategoria za miktadha, pia aliweza kutafiti kuhusu uwazi na umaanisho wa kauli za Egegusi na lugha ya Kiswahili. Utafiti huu wa Ochichi (2013) ni wa msaada kwetu kwani utatuwezesha kupata ufahamu jinsi dhana zinavyosimbwa kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili.

Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti na utafiti wetu kwa sababu, Ochichi (2013) aliweza kutafiti kuhusu umaanisho na usimbwaji wa maana katika lugha ya kimazungumzo nasisi tunatafiti kuhusu maana ya kipragmatiki ya lugha katika jukwaa la Facebook kwa ujumla ikiwa ni mojawapo ya nyenzo za kimawasiliano.

Okuku (2012) anaangalia uchanganuzi wa kiisimu katika baadhi ya matini ya lugha ya Kiswahili akitumia nadharia ya pragmatiki leksika ambapo amejikita katika kuchanganua tamathali za usemi akirejelea riwaya ya Kiswahili. utafiti wa Okuku ni wa manufaa kwetu kwa sababu kupitia kwayo tutaweza kuelewa matumizi ya nadharia ya pragmatiki leksika. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa, Okuku aliweza kupambanua tamathali za usemi akirijelea riwaya ya kiwahili lakini utafiti wetu nao unahusu maana ya kipragmatiki ya lugha katika jukwaa la Facebook. Pia utafiti wa Okuku unahusu masuala ya kifasihi kinyume na utafiti wetu ambao ni wa masuala ya kiisimu.

Ogutu, P. O. (2018) alitafiti suala la uchanganuzi wa matumizi ya agoti miongoni mwa wafungwa. Hali ya magereza teule katika jimbo la Kisumu nchini Kenya kwa mtazamo wa nadharia ya pragmatiki leksika ya Blutner (1990). Mtafiti aliweza kupata kuwa agoti za wafungwa zilipitia mabadiliko ya kimaana na kupata miktadha kutokana na michakato ya pragmatiki leksika kwani aina zote za mabadiliko zilijitokeza katika agoti ambazo zinatumiwa na wafungwa wa magereza ya Kisumu. Utafiti wa Ogutu ni wa muhimu katika utafiti wetu kwa sababu utaweza kutupa mwelekeo kuhusu michakato ya kipragmatiki kama vile: upanuzi wa kimaana, kubana kwa maana na kisio la maana. Pia utafiti huu utaweza kutupa mwongozo jinsi nadharia ya pragmatiki leksika inavyotumika katika kuchanganua masuala ya utafiti. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa, Ogutu alitafiti kuhusu suala la agoti za wafungwa katika magereza ya kisumu nchini Kenya na utafiti wetu nao unajihusiha na suala la maana ya kipragmatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook ambapo ni miongoni mwa nyenzo za kimawasiliano katika himaya ya mawasiliano.

1.13.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ya Utafiti

Mawasiliano ni njia mojawapo ya kuleta mshikamano na mwamana katika jamii. Katika jidihada za mawasiliano, lugha ni kiungo muhimu mno katika harakati hizi za kimawasiliano kwani, binadamu hutumia ujuzi aliyonao katika mawanda ya lugha kwa minajili ya kuyakidhi mahitaji yake ya kila siku maishani.

Kuibuka kwa mitandao ya kijamii kama nyenzo ya mawasiliano, kuliwapa afueni adinasi wa Rabana kwa sababu mitandao ya kijamii kama nyenzo ya kimawasiliano iliweza kuleta afueni katika uchanjaa wa kupitisha ujumbe.

Jambo la kusikitisha ni kuwa suala la mitandao ya kijamii halijashughulikiwa sana katika isimu japo kuna tafiti chache ambazo zimeshughulikia masiala haya. Tafiti hizi ni kama zifuatazo:

Mwaringa, D. K. (2002), alishughulikia suala la mitandao ya kijamii katika mada “**Globalization and cultural impact of the media: aweb analysis of the Facebook social network.**”

Maina.W. Rachel anaangalia jinsi lugha ya Kiswahili inavyotumika katika mitandao ndani ya makala yanayowasilisha ujumbe wa kimawasiliano. **Kiswahili kwenye mtandao** katika Chimera R. na wengine (2011) (ed.) **Kiswahili research and development in East Africa.**

Shawcraft,(2014). **Gender differences in texts messaging: Birmigham Young University,** ameangalia namna jinsia inavyoathiri matumizi ya lugha ya kimawasiliano katika ujumbe mfupi wa simu.

Msomi huyu anasema kuwa, simu imeathiri sana jinsi vijana wa Marekani wanavyotumia lugha ya kiingereza.

Utafiti huu ni wa muhimu kwetu kwani, utatupa mwanga kuhusu matumizi ya lugha katika jukwaa la Facebook pia tutaweza kupata mwamana kuhusu maana ya kipragmatiki ya lugha inayotumiwa katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook.

Tofauti na utafiti wetu ni kuwa mtafiti huyu alifanya utafiti wake kwa kutumia lugha ya kiingereza nasi tunatafiti kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Pia msomi huyu aliweza kutafiti namna jinsia inavyoathiri matumizi ya lugha katika ujumbe mfupi wa simu tofauti na utafiti wetu ambao unahusu maana ya kipragmatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook.

Mohammed, N.A (2013). Katika tasnifu yake, amefua dafu kwa kutafiti athari za lugha tandawazi katika simu tamba. Msomi huyu anadai kuwa rukono zimeathiri jinsi ambavyo watu huzungumza kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Anaendelea kwa madai kuwa, lugha ya Kiswahili imegeuzwa kwa kiwango kikubwa na simu za mkononi.

Utafiti wa Msomi huyu ni wa msaada mkuu katika utafiti wetu kwa sababu utatuwezesha kuelewa mageuzi ya maana katika lugha ya mitandao ya kijamii. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa Mohammed aliweza kutafiti kuhusu suala la athari za lugha tandawazi katika simu za mkononi ilhali utafiti wetu nao unahusu suala la maana ya kipragmatiki katika lugha ya jukwaa la Facebook.

Mtembei (2011) naye katika utafiti wake wa kiusomi, aliweza kutafiti juu ya matumizi ya simu za mkononi katika mawasiliano. Alizamia matumizi ya rukono katika kuandika ujumbe mfupi. Kulingana na utafiti wa mtafiti huyu, ujumbe mfupi wa simu umerahisisha mawasiliano.

Hata hivyo, anaongezea kuwa ujumbe mfupi wa simu umevuruga matumizi ya sarufi ya lugha ya Kiswahili kwa kiwango kikubwa.

Utafiti wa Mtembei (2011) ni wa msaada mkuu katika utafiti wetu kwa sababu utaweza kutupa mwanga wa miundo na maana katika ujumbe mfupi unaotumika katika jukwaa la Facebook.

Tofauti na utafiti wetu ni kuwa mtafiti huyu aliweza kutafiti kuhusu matumizi ya simu za mkono katika kuandika ujumbe mfupi ilhali utafiti wetu unahusu maana ya kipragmatiki ya lugha inayotumika katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook.

Taga Caroline (2009), katika utafiti wake wa kiakademia, alifanikiwa kutafiti kuhusu suala la; **Acopus linguistics study of sms texts messaging**, ambayo iliwasilishwa katika chuo kikuu cha Birmingham, anadai kuwa kuna mshabaha mkubwa baina ya lugha ya ujumbe mfupi wa simu na lugha ya kimawasiliano ya mitandao.

Anaendelea na madai kuwa matumizi ya simu za mkononi hutawaliwa na matumizi ya vifupisho, akronimu na matumizi ya nambari baina ya maneno.

Wazo ambalo hujitokeza sana katika lugha ya mitandao. Utafiti huu ni wa muhimu katika utafiti wetu kwani tutaweza kubainisha miundo na maana ya lugha inayotumika katika mawasiliano ya mtandao wa kijamii wa Facebook. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa Taga alishughulikia masuala ya ujumbe mfupi kinyume na utafiti wetu ambao unahusu maana ya kipramatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook, isitoshe, Taga alifanya utafiti wake kwa lugha ya kiingereza ilhali utafiti wetu ni wa lugha ya Kiswahili.

Mohammed, M. R. (2012) anatoa madai kuwa kuna uwiano mkuu kati ya lugha ya barua pepe na lugha ya mazungumzo ya kawaida. Msomi huyu anaendelea kudai kwa kupachika jina lugha kama vile lugha ya barua pepe, teknousemi yaani usemi wa kiteknolojia. Utafiti huu ni wa msaada mkuu katika utafiti wetu kwani utatuwezesha kupata ufahamu juu ya lugha ya mtandao.

Tofauti kati ya utafiti wa Mohammed na utafiti wetu ni kuwa, yeye alitafiti kuhusu mfanano uliyopo kati ya lugha ya barua pepe na lugha ya mazungumzo ya kawaida lakini utafiti wetu nao

unahusu mi maana ya kipragmatiki ya lugha katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook kama nyenzo mojawapo ya kimawasiliano.

Brenda, D. (2002) anachanganua sifa za lugha ya barua pepe. Ingawa anatoa madai kuwa uchunguzi wa barua pepe una changamoto nyingi kwa kuwa mazungumzo ya barua pepe ni mazungumzo ambayo hutekelezwa faraghani na binadamu huyatumia katika shughuli za kibinafsi.

Utafiti huu wa Brenda ni wa muhimu kwa sababu utatupa mwanga kuhusu uchanganuzi wa lugha. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa, yeye alichunguza sifa za lugha ya barua pepe kilicho kinyume na utafiti wetu ambao unachunguza maana ya kipragmatiki ya lugha itumikayo katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook.

Pinker (1994) anadai katika mandishi yake kuwa, mfumo wa mawasiliano ya viumbe wasio wanadamu yana muundo wa aina tatu.

Miundo hiyo ni kama ifuatayo: Milio yenye ukomo, ishara zenye kuendelea ambazo zinaonyesha namna na jinsi hali ilivyo na seti isiyo na utaratibu wa mabadiliko ya mada wakati lugha ya adinasi ina miundo tofauti kabisa ambapo tabia ya mfumo wa muungano uitwao sarufi huifanya lugha ya mwanadamu kuwa iso ukomo na yenye kuherufika na kutungika. Mawazo ya Pinker ni wa muhimu kwa utafiti huu kwani utafiti huu umelenga kuchunguza na kuchanganua lugha ya binadamu ambao huwasiliana kupitia mtandao wa kijamii wa Facebook kimuundo na kimaana .

Tofauti na utafiti wetu ni kuwa Pinker alijikita katika kubainisha tofauti zilizopo kati ya lugha za wanyama na lugha za mahuluki lakini utafiti wetu nao unalishughulikia suala la maana ya kipragmatiki katika lugha ya mawasiliano katika jukwaa la Facebook kama mojawapo ya nyenzo za kimawasiliano.

Rita, N. (2013) alifua dafu kwa kutafiti kuhusu athari za mitandao ya kijamii kwa vijana. Alifanya utafiti wake kwa kutumia sampuli ya vijana wa vyuo vya Nairobi ambao ni wanafunzi, msomi huyu aliweza kubaini kuwa vijana huwa wanatumia muda mwingi katika kudurusu mitandao ya kijamii miongoni mwa gango zingine. Hata hivyo, utafiti wake Rita pia ulipata kuwa vijana wengi hutumia mitandao ya kijamii katika mawasiliano ikilinganishwa na mbinu zingine za mawasiliano kuongezea, mitandao ya kijamii ina athari chanya pamoja na athari hasi katika maisha ya vijana katika jamii ya utandawazi na utandarithi.

Utafiti wa Rita ni wa muhimu kwani utaweza kutupatia mwelekeo kuhusu lugha ya mitandao ndiposa nasi tuchukulie pale kwa kutafiti kuhusu maana ya kipragmatiki ya lugha ya mtandao wa kijamii wa Facebook kama nyenzo ya kimawasiliano.

Tofauti iliyopo kati ya utafiti wa Rita na utafiti wetu ni kuwa, alitafiti kuhusu athari za mitandao ya kijamii kwa vijana ilhali utafiti wetu nao unahusu maana kipragmatiki ya lugha ya mawasiliano katika jukwaa la Facebook.

Kiunga (2016) alitafiti kuhusu maana ya usemi na mazungumzo katika mitandao ya kijamii hususan Facebook na Twitter. Mtafiti huyu aliweza kubainisha kuwa lugha katika mitandao ya kijamii ina sifa na majukumu yake maalum, pia mitandao ya kijamii ina nafasi kubwa katika jamii kwa sababu inawaunganisha watu wa matabaka mbalimbali katika jamii.

Isitoshe mazungumzo katika mitandao ya kijamii hupuuza kanuni za ushirikiano, Kwa mujibu wa Grice (1975) na mojawapo ya sababu za kupuuza kanuni za ushirikiano hizi ni wingi wa watu ambao hutumia mitandao ya kijamii kwani mitandao ya kijamii hutumiwa na watu wengi kote ulimwenguni kwa minajili ya kukidhi mahitaji yao ya kimawasiliano. Utafiti huu wa Kiunga (2016), ni wa muhimu katika utafiti wetu kwa sababu, utaweza kutumulikia kurunzi kuhusu maana ya baadhi ya istilahi za lugha zinazotumiwa na mahuluki luluki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook.

Tofauti na utafiti wetu ni kuwa, Kiunga alifanya utafiti unaohusu maana ya usemi katika mazungumzo ya mitandao ya kijamii ambayo ni Facebook na Twitter lakini utafiti wetu nao unajihusiha na masuala ya maana ya kipragmatiki ya lugha inayotumika katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook pekee wala si mitandao mingine yoyote ile. Tofauti nyingine ni kuwa Kiunga alitafiti kwa kujikita katika nadharia ya Umaanisho ya Grice (1975) nao utafiti wetu unaongozwa na nadharia ya pragmatiki leksika ambayo mwasisi wake ni Reinhard Blutner.

1.14 Mbinu za Utafiti

1.14.1 Mbinu za Kukusanya Data

Utafiti wetu utashughulikiwa katika mtandao wa intaneti. Tutazuru kurasa za wanafuzi wa chuo kikuu ambao huwasiliana kupitia jukwaa la Facebook kwa lugha ya Kiswahili, data ya utafiti huu itatoka kwenye majukwaa ya makundi yafuatayo; kundi la Kenyan university students, Kenya universities organization na Kenyatta university comrades. kwa sababu ya masuala ya mbeko, wanafunzi ambao tutazuru kurasa zao, watakuwa wanafunzi ambao wametupa idhini yao, Kisha kufanya uchanganuzi wa data ambayo tutakuwa tumepata. Tumechagua kuyatumia makundi matatu kwa sababu ya upanuzi wa mawanda ya utafiti na pia makundi haya yatawezesha kubaini ni mchakato upi unaotumika kwa wingi na wawasilianaji wa Facebook.

Isitoshe, tutaweza kuwarejelea wataalam mbalimbali katika uwanja huu wa utandawazi na utandarithi wakiwemo wandishi. Ili kuona na kufahamu jinsi lugha inavyotumika kimuundo na kimaana. Uchanganuzi wetu wa maana ya kipragmatiki ya lugha katika jukwaa la Facebook, utakuwa wa kiuwezi pamoja na matumizi ya takwimu.

1.15 Uteuzi wa Sampuli

Maana ya lugha ambayo itateuliwa kufanikisha utafiti huu itatolewa katika jukwaa la Facebook. Mbinu itakayotumika ni mbinu ya kuteua sampuli ambayo ni mbinu ya kuteua madhumuni maalum.

Mbinu hii ni mojawapo ya mbinu za utafiti ambayo ni mbinu ambayo mtafiti anaamua mwenyewe kwa hiari yake kuteua kundi la watu au vitu anavyoamini vinaweza kumpatia data inayoweza kufanikisha malengo yake ya utafiti.

Mtafiti atatumia matini lengwa na makundi ya watu aliyowataja hapo juu kama mbinu za kukusanya data. Kwa sababu mawasiliano ya jukwaa la Facebook ni ya lugha ya kimaandishi na kimazungumzo, Hii itakuwa afueni kwa mtafiti kuweza kuchanganua maana ya kipragmatiki ya lugha ya mtandao wa kijamii wa Facebook.

1.16 Uchanganuzi na uwasilishaji wa Data

Baada ya kunakili maana ya kipragmatiki ya lugha katika jukwaa la Facebook, tutaweza kuainisha lugha kulingana na maana yake na pia kulingana na michakato ya pragmatiki leksika kama vile; upanuzi wa maana, ubanaji wa maana na kisio la maana. Halafu, tutaweza kuifafanua miundo na maana ya lugha tumizi katika kategoria husika kulingana na nadharia ya pragmatiki leksika iliyoasisiwa na Reinhard Blutner (1990).

Vilevile, tutaonyesha jinsi michakato ya kileksika ilivyotumika kubaini maana ya lugha katika jukwaa la Facebook na kubainisha ni mchakato upi wa kileksika unaotumiwa na wawasilianaji kwa wingi katika jukwaa la Facebook.

1.17 Muhtasari wa Sura

Sura ya kwanza ya tasnifu hii imeweka msingi wa utafiti kwa kueleza usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, msingi wa nadharia ya utafiti, mbinu za kukusanya data na uwasilishaji wa data.

Sura ya pili nayo inajadili mitazamo ya kipragmatiki, mifumo ya mawasiliano ya jukwaa la Facebook ambapo tumeweza kutoa maelezo kuhusu historia fupi ya Facebook, sifa za lugha ya kimawasiliano katika jukwaa la Facebook kwa kutoa maelezo na mifano kutoka makundi yaliyoteuliwa kwa utafiti ya jukwaa la Facebook, dhana ya pragmatiki, muktadha na mawasiliano katika jukwaa la Facebook kwa kujikita katika mitazamo ya wataalamu mbalimbali. Vilevile, jinsi ambavyo lugha huhusiana na mawasiliano.

Isitoshe, tumeweza kushughulikia dhana ya maana kwa kuzingatia nadharia yetu ya utafiti ambayo ni nadharia ya Pragmatiki leksika ya Blutner (1990). Ambapo tumejadili michakato ya kileksika kama vile, ubanaji wa maana, upanuzi wa maana na kisio la maana jinsi yanavyojitokeza katika mawasiliano kwa kujikita kwenye jukwaa la Facebook ambapo utafiti huu unahusika.

Sura ya tatu ya tasnifu hii inajadili jinsi mawasiliano ya Facebook yanavyoibua maana kisemantiki na kipragmatiki kulingana na nadharia ya pragmatiki leksika ambayo mwasisi wake ni Reinherd Blutner. Nadharia ambayo iliasisiwa mnamo mwaka wa (1990).

Isitoshe, Sura hii inaangazia jinsi ambavyo wanafunzi wa chuo kikuu wanavyoibua maana katika mawasiliano yao kwenye makundi katika Facebook kwa kiipanua maana ya maneno kimawasiliano kwa mujibu wa pragmatiki leksika.

Mifano mbalimbali inatolewa jinsi wanafunzi wa chuo kikuu katika mawasiliano yao, hulenga kukidhi mahitaji ya kimawasiliano baina ya wanakikundi kupitia Facebook.

Sura ya nne ya tasnifu hii inajadili namna mawasiliano ya Facebook huchukua mtazamo wa ubanaji wa maana na ukadiriaji wa maana kwa mujibu wa pragmatiki leksika. Sura ya tano ya tasnifu hii inajadili matokeo ya utafiti, changamoto za utafiti pamoja na kutoa mapendekezo ya tafiti za siku za usoni.

SURA YA PILI

MITAZAMO YA KIPRAGMATIKI NA MIFUMO YA JUKWAA LA FACEBOOK

2.0 Utangulizi

Katika sura hii tutajadili historia na mifumo ya Facebook, Sifa za lugha ya kimawasiliano katika jukwaa la Facebook, dhana ya pragmatiki, muktadha, na mawasiliano katika jukwaa la Facebook. Isitoshe tutajadili mitazamo ya kipragmatiki na jinsi ambavyo lugha huhusiana na mawasiliano. Vilevile, tutaweza kushughulikia dhana ya maana kwa kuzingatia nadharia yetu ya utafiti ambayo ni pragmatiki leksika ya Blutner(1990), ambapo tutajadili michakato ya kileksika kama vile: Ubanaji wa maana, upanuzi wa maana na kisio la maana katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook ambapo utafiti huu unahusika. Mawazo haya katika sura hii ni kulingana na mchango wa wataalamu mbalimbali wa lugha na matumizi yake kwa minajili ya kukidhi haja ya kimawasiliano.

2.1 Historia na Mifumo ya Mawasiliano ya Jukwaa la Facebook

Mtandao wa Facebook ulianzishwa na Mark Zuckerberg ambaye alikuwa mwanafunzi wa chuo kikuu cha Havard pamoja na wanafunzi wenzake. Tukiwataja; Edwardo Saverin, Dustin Moskovitz bila kumsahau Chris Hughes. Wakati huo huo, nomino iliyokuwa ikitumika ilikuwa Thefacebook ambapo neno Facebook lilitokana na neno la kimsimu ambalo lilikuwa likitumika sana katika chuo kicho hicho kwa urejelezi wa kitabu ambacho kilikuwa na paspoti za wanafunzi wa chuo hicho cha Havard. Yakiwemo maelezo mengine kama vile majina ya vyumba vya kulala ndiposa kitabu chenyewe kikapata kujulikana kwa nomino kuu Facebook.

Zuckerberg na wenzake, walidakua wavuti ambao ulimilikiwa na idara ya mtandao katika chuo kikuu cha Havard walifua dafu kuiba picha za wanafunzi wenzao pamoja na makala ya maelezo mengine ya kimsingi kama vile: Kitivo, jina na mengineyo, na kisha kuyaweka maelezo hayo pamoja na picha kwenye mtandao wao mpya.

Picha ambazo ziliweza kupata watazamaji wengi sana baada ya muda usiyo mrefu. ([htt://venturebeat.com/2008/12/18-history and growth of Facebook](http://venturebeat.com/2008/12/18-history-and-growth-of-facebook))

Mnamo Juni mwaka wa (2004), makao makuu ya Facebook yaliamishwa hadi pale Alto California.

Isitoshe, kufikia Oktoba 2005, matumizi ya jukwaa la Facebook yalikuwa yamepata mawanda mapana kwa kuenea takribani vuo 21 Uingereza na kuzindua aina ambayo iliweza kutumika katika shule za upili. Mbeleni, Facebook iliweza kuwaruhusu watenda kazi wa kampuni mbalimbali kama vile; Microsoft kujiunga na mtandao wao.

Hivyo basi, kufikia mwaka wa (2006), Facebook iliwaruhusu watu wote ambao walikuwa na hirimu ya miaka kumi na mitatu kujiunga na jukwaa la Facebook mradi wawe na anwani ya barua pepe iliyohalalishwa. Mnamo Oktoba (2008), matangazo yalitolewa katika jukwaa la Facebook kuhusu mpango wa kuhamisha makao makuu yake hadi Dublin, Ireland.

Kufikia (2010), Facebook ilikuwa imepanuka kwa kiwango cha juu mno ambapo mwaka uliyofuata February, Facebook ilikuwa mtandao ambao ulikuwa na matumizi mengi.

April (2012), Facebook ilikuwa na watumiaji wa kukadiria million mia tisa. Mtumizi wa jukwaa la Facebook, anapoingia kwenye kivinjari cha Tarakilishi au kipakatalishi kilichounganihwa na intaneti, hubonyeza anwani ya jukwaa la Facebook ambayo ni; [http: // wwwfacebook.com](http://www.facebook.com). Huingia kwenye wavuti wa jukwaa la Facebook ambako anapaswa tu iwapo yeye ni mumiliki wa akaunti ya jukwaa la Facebook.

Facebook ni jukwaa ambalo hupatikana katika takribani lugha Sabini ulimwenguni lugha ya Kiswahili ikiwa miongoni mwa lugha hizo. Kuongezea, katika Facebook kuna eneo la kuingia katika kurasa zake katika lugha ya Kiswahili ambapo msamiati maalumu wa jukwaa hili la Facebook pamoja na msamiati wa kiteknolojia umefasiriwa.

Msamiati huu ni kama vile;

- Ingia -log in
- Nywilia –password
- Toka nje –log out
- Jisajili -log up

Kwa muhtasari, ukurasa wa nyumbani ambao ndio ukurasa wa kwanza mtu anapofungua jukwaa hili la Facebook katika lugha ya Kiswahili, makaribisho ni **‘sasisha hali yako’** au swali **‘unafikiria nini?’** hapa mtumiaji wa Facebook anahitajika kuandika chochote ambacho kiko akilini mwake hususan habari ambazo angependa ziweifike watumiaji wengine wa jukwaa la Facebook.

Maraa kadha wa kadha anachoandika hutegemea hali ya kimuktadha. Yaani, kitu ambacho kinatawala mazungumzo au mawasiliano ya wanajamii kwa wakati huo kama vile; hali ya mtihani chuoni, mazungumzo ya baadhi ya wanasiasa, hali ya kidini, uchaguzi na mengineyo.

Manufaa ya jukwaa hili la Facebook ni mengi kwani, athari chanya ni kuwa jukwaa la Facebook huleta utengamano kwa watumiaji wake. Pia, Facebook huwezesha lugha ya Kiswahili kupata maenezi kote ulimwenguni.

Ujio wa Facebook una athari hasi kwa jamii hivi kwamba vijana wengi hubananga mwida mwingi katika jukwaa la Facebook na kusahau shughuli za ujenzi wa taifa. Haya ni kwa mujibu wa utafiti wa Rita (2013).

2.2 Sifa za Lugha ya Jukwaa la Facebook

2.2.1 Usilabishaji

Mawasiliano katika jukwaa la Facebook kimsingi huchukua mwelekeo wa mazungumzo ya moja kwa moja yaani mtu anatuma ujumbe kisha ujumbe huo unachangiwa kimawasiliano na wengine. Jukwaa la Facebook huwapa binadamu fursa ya kujuliana hali, kutengeneza urafiki na kuweza kuendeleza urafiki kwa mawasiliano kwenye jukwaa.

Massamba D.P.B (1994) usilabishaji ni ugawaji wa maneno katika silabi, ugeuzaji wa vitamkwa ambavyo awali havikuwa silabi ili viwe kama silabi. Katika jukwaa la Facebook, ugeuzaji wa silabi ni suala la kawaida sana kwani, watumiaji wa jukwaa la Facebook, hugawa silabi na kugeza vitamkwa ili vitamkike kwa njia ambayo kwao matamshi yake ni rahisi. Suala hili hasa hutokea baina ya watumiaji wa Facebook. Katika kufanya hivi wawasilianaji wa Facebook huwasiliana kwa matumizi ya herufi na nambari ambazo hutamkika katika usilabi wa sauti na maneno ambayo ni maneno lengwa ya kimawasiliano. Mfano wa maneno ni; 2kutane kesho. Katika usemi huu tunaona matumizi ya herufi pamoja na nambari. Tazama mifano mingine hapa chini kutoka jukwaa la Facebook.

Maasai Lekishon

Imagine it's only 100 bob guys na hutawai kosa kamaziwa kamtoi 😊😊😊 on this platform I earn between 400-600 daily 😊😊 si mambo ya kuchochana ati 10k daily zii!! Hii ni legit kapunch kako na unasonga 😊😊 join smartpay today. You earn in 5 ways

1. Watch videos for 30 seconds only and get paid 50 bob 😊

2. Easy questions survey questions. 5 questions@50 😊

3. Lucky spin win upto 4000 🤑
4. Clicking ads and you get paid 😊
5. Referral (optional) 50 bob for every referral made 🎉
6. Welcome spin free for all new users. 🤗

Minimum withdrawal ni 200 paid directly to your mpesa number. With these utakosaje kapunch (500) daily 🧑 hio ni enough, considering unalipa tu Soo(100) kujoin alafu hutawai lipa dooh ingine tena 😱😱 it's a lifetime investment 😊😊 tafuta kamia tuomoke kimoja na Mia moja 🙌

<https://www.smartpaykenya.com/signup.php?ref=Eagle>

SMARTPAYKENYA.COM

Register to Smartpay

Mawasiliano haya ya Maasai Lekishon yanatupa idhibati kuwa katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook, kuna matumizi ya mfumo wa usilabishaji ambapo tunaona matumizi ya herufi pamoja na nambari.

Prince Johnty

Ameshiriki chapisho lake la kwanza.



· **16 Aprili saa 09:30** ·

Kirinyaga University watuu wa financial engineering mko wapii,,,,,,course inawapeka aje 🤔🤔

Katika kijejezi hiki cha mawasiliano, Prince Johnty anatumia usilabishaji ambapo tunaona neno 'watu' limeongezwa silabi 'u' na kuwa **watuu**. Hata hivyo idadi ya silabi katika neno watu imeongezeka kwa maana ya kuleta msisitizo wa kimaana katika mawasiliano.

2.3 Sifa za mkutano duara au kikongamano

Jukwaa la Facebook ni kama ukumbi wa mawasiliano ambako watu hujadili masuala ya aina nyingi. Hapa watu huhadithiana kwa kutoa hoja halafu wengine huchangia kwa kutoa maoni. Kutoa mchango mara nyingine kunalingana na iwapo yanayojadiliwa yanakuhusu au kivingine. Mawasiliano ya Facebook yanachukua mwelekeo wa rafiki wa mfuasi kutuma ujumbe. Kongamano duara ni mkutano wa watu ambao wanalenga kuwasiliana au kutafuta suluhisho kuhusu masuala mbalimbali ambayo yanawaathiri katika ulimwengu wa sasa.

Masuala hayo huweza kuwa rasmi au masuala ya kikawaida.

Wahusika katika mawasiliano ya Facebook ni mfano wa kongamano duara kwani, wafuasi wa mja Fulani katika Facebook ambao pia huitwa marafiki, ni mfano wa washiriki katika kongamano kwani, wanaweza kutazama na kusoma hoja ambazo zimetolewa na wenzao ama washiriki kwa kutoa maoni yao. Ukurasa wa Facebook hapa hujukuliwa kama jukwaa la mawasiliano.

2.4 Matumizi ya lugha ya Kiswahili.

Lugha katika Facebook ni lugha ya kiteknolojia. Hivyo basi, kuna uwezekano wa lugha ya Kiswahili kutumika. Sababu kuu ni kwamba lugha ambayo inatumika zaidi kiteknolojia ni lugha ya kiingereza kwani, kiingereza ndiyo lingua franca kote ulimwenguni. Tukizingatia maelezo hayo, tutaweza kubaini kuwa msamiati mwingi ambao unahusu teknolojia umetafsiriwa na mwingine kubakia vivyo hivyo japo umetoholewa ili kuunadhibisha na lugha ya Kiswahili pasipo uchunguzi wa misingi ambao uliwekwa kwenye utohosi huo wa maneno.

Kwa mfano katika matumizi ya neno 'Buku' pia matumizi ya neno outocomplete.

- Buku -Book
- Kamilisha kiotomati - outocomplete

Isitoshe, wawasilianaji katika jukwaa la Facebook hutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano yao bila kuzingatia sheria za kisarufi.

Mfano ni katika matumizi ya neno xaxa badala ya sasa. Sote tunafahamu fika kwamba sauti /x/ haitambuliki katika mfumo wa sauti mahsuszi za lugha ya Kiswahili yaani fonolojia ya lugha ya Kiswahili. Lakini wawasilianaji wa Facebook wana mazoa ya kutumia sauti hiyo kwa nafasi ya sauti /s/ ambapo ni ukiushi wa mfumo wa kisarufi. Pia, katika sentensi; Home naenda badala ya kusema ninaenda nyumbani. Tunaona kuwa mpangilio wa vipashio vya kisarufi umevurugwa ambayo ni mazoea ya vijana katika mawasiliano yao katika Facebook.

2.5 Kuchanganya Msimbo

Dhana ya uchanganyaji msimbo imeshughulikiwa na wataalam mbalimbali kama vile; Massamba D.P.B (1994) anatoa ufafanuzi wake kuhusu suala la msimbo kuwa, kuchanganya msimbo ni matumizi ya lugha mbili tofauti katika harakati za kupitisha ujumbe wa kimawasiliano. Massamba (1994) anaendelea kutufahamisha kuwa, lugha hizi zinaweza kuwa kiingereza na Kiswahili, au lugha nyinginezo katika mazingira ya mawasiliano.

Wei (1998) anatoa fafanuzi kuhusu suala la kuchanganya msimbo kwamba, kuchanyanya msimbo ni kutumia lugha mbili katika mkabala wa mawasiliano kwa kiwango ambacho kipo chini ya kishazi kimawasiliano na kiuelezi.

Bokamba (1989) naye anafafanua dhana ya kuchanganya msimbo kuwa ni hali ya kuingiza vipashio vya kiisimu kama vile; mofimu, kirai, neno na kishazi vya sentensi kwenye vipashio ambavyo hujitokeza katika lugha nyingine.

Buliba na wenzake (2009), nao wanadokeza kuwa uchanganyaji msimbo ni hali ya msemaji kutumia vipashio vya lugha mbalimbali katika hali moja ya kimazungumzo kwa minajili ya kuafiki lengo la kimawasiliano.

Tukizingatia fafanuzi za wataalam hawa, tunapata uelewa wa dhana ya uchanganyaji msimbo kuwa ni hali ya kutumia sarufi za lugha mbili tofauti katika muktadha mmoja wa mazungumzo.

Mawasiliano ya jukwaa la Facebook yanaibua matumizi ya uchanganyaji msimbo hivi kwamba maana kusudiwa ni sharti iweze kufasiriwa kwa kujikita kwa muktadha wa mazungumzo. Kama vile katika usemi huu:

Eli Masete

Na we we sura heri stivo simple boy umeparara huna luku msee Wa kunyonga

- Penda

‘mko sawa sana bro nitakam kuwasalamia’, ‘Happy birthday mbotswa, may you enjoy this auspicious day zeeka uone na ujionee’ Katika kifungu cha kwanza hatuwezi kufahamu mwasilianaji anamaanisha nini kwa kusema mko sawa. Hata hivyo, amechanganya lugha ya Kiswahili na kifupisho cha lugha ya kiingereza brother.

Kifungu cha pili nacho kimechukua mkondo wa kuchanganya lugha zaidi ya mbili yaani;

Happy birthday - kiingereza

Mbotswa - kiluhya

Zeeka uone na ujionee - Kiswahili.



Aligura E.A.

Kenya Universities Student Organization



· Saa 14 ·

Dem Wa Campo, Two Minutes Into A Relationship Anatek "Beb Sijakula Lunch"

189189

Maoni 68

Penda

Maoni

Mawasiliano ya Aligura E.A , yanashamiri mfumo wa uchanganyaji msimbo ambapo tunaona matumizi ya maneno ya lugha ya Kiswahili na maneno ya lugha ya kiingereza ambayo ni idhibati kwamba mawasiliano ya jukwaa la Facebook hujukua mfumo wa kuchanganya msimbo.



Mathew Musyoki

Ameshiriki chapisho lake la kwanza.



· 17 Aprili saa 21:58 ·

Ni course gani ukifanya campus wanakijiji wanaona unawaste fee ya parents?

533533

Maoni 309

Tukitazama kijezezi hiki cha mawasiliano, tunaona kwamba kuna matumizi ya lugha ya Kiswahili kimawasiliano na pia matumizi ya lugha ya kiingereza. Hii ni idhibati kuwa mawasiliano ya jukwaa la Facebook hujukua mfumo wa uchanganyaji msimbo.

2.6 Matumizi ya vifupisho

Lugha inayotumika katika jukwaa la Facebook wakati mwingine huchukua mwelekeo wa matumizi ya vifupisho. Hii ndiyo sababu mojawapo ambayo inamhitaji mfasiri wa maana ya mawasiliano katika jukwaa la Facebook kuhitaji uelewa wa muktadha wa jumbe zilivyotolewa.

Matumizi ya vifupisho kama vile:

NKT - kumaanisha vyema, ni sawa au nimekubali. Kuelewa maana kusudiwa hapa lazima mfasiri wa maana ya mazungumzo ambayo vifupisho kama hivi vimetumika ni sharti awe na uelewa wa mazingira ya kimawasiliano.

Vifupisho vingine ni kama vile:

Fb - Facebook
Bf - boy friend
Hw - home work
Pliz - please
Thx - thanks
Dec - december.



Mwanachama Mgeni

· Saa 7 ·

Kama uko kwa Hii group na Ukona 20 years and above comment HI then uangalie inbox yako after 5 minutes for an opportunity.

Katika usemi huu, mwasilishaji wa ujumbe huu anatumia nambari badala ya maneno. Hii ni idhibati kuwa mawasiliano ya Facebook huchukua mtazamo wa matumizi ya vifupisho. Isitoshe, kuna matumizi ya kunchanganya msimbo kama sifa ya lugha ya jukwaa la Facebook.

2.7 Matumizi ya Ikonihisi na picha

Neno ikonihisi ni neno ambalo limetafsiriwa kutoka kwa neno la kiingereza emotion pamoja na neno icon.

Ferdinand De Saussure alitoa fafanuzi kuhusu dhana ya lugha kama mfumo wa ishara na sauti nasibu kwa maana kuwa, jamii hukubaliana kuhusu maana ya ishara mbalimbali ambazo jamii hiyo hutumia kimawasiliano kwani, kulingana na mwanaisimu huyu 'De saussure' hakuna uhusiano baina ya kiashiria na kiashiriwa. Hivyo basi, ishara zitumikazo ni kwa misingi ya makubaliano katika jamii.

Mawasiliano ya Facebook, hujukua mtazamo wa matumizi ya ishara ambazo zinawasilisha hisia za binadamu katika mawasiliano hayo. Mara nyingi uso wa mtoa ujumbe au mwasilianaji kwa mlengwa wa mawasiliano, atausoma ujumbe huo na kuufasiri kulingana na ishara ambazo


zimetumika (ikonihisi). Kwani ikonihisi huweza kuwa za msaada mkubwa katika ufasiri wa maana ya mawasiliano. Tazama ujumbe huu hapa chini:

Travis KE



2.8 Msimulizi wa hadithi Anayeonekana

· Saa 1 ·



3232

Maoni 15

Penda

Maoni

🤣🤣🤣🤣 hii hapa mifano ya ikonihisi za kuonyesha hisia ya furaha.



Mbulah Musyoka

Saa 2 ·

Kampuni yetu inatafuta form4leavers, students, jobseakers na graduates. Malipo (13k-21k). in Nairobi, Mombasa, Kisumu, Nakuru and Eldoret. Comment MI.

Penda

Maoni

Shiriki

Maoni

Andika maoni ya umma...

Bonyeza Ingiza ili kuchapisha.



Brilly Mum Gifty Ukipigana na maisha afu maisha yakushinde 🧡🧡 plz unaenda kushtaki

wapii 😞😞😞

Tukitazama ujumbe huu, tunaweza kubaini kuwa mawasiliano ya jukwaa la Facebook yanachukua mwelekeo wa matumizi ya ikonihisi, picha, uchanganyaji wa msimbo, kutumia lugha ya Kiswahili kilegevu pamoja na usilabishaji.



Çëë Thëë Çlĩñtõñ
Kenya Universities Student Organization
15 Aprili saa 23:24 ·

Unaringa na uko Embarambara university (kisii university) 🤪🤪🤪

168168

Maoni 61

Penda

Maoni

Katika mawasiliano haya, mwanafunzi huyu anawasilisha ujumbe wake kwa kutumia ikonihisi za kejeli kuonyesha kwamba kando na chuo kikuu cha Kisii kuna vyuo vingine vingi vya hadhi ya juu kuliko chuo kikuu cha Kisii.



Çëë Thëë Çliñtõñ

Kenya Universities Student Organization

17 Aprili saa 08:51 ·



kuna university inajiita steve simple boy (Maseno university) be serious guys 😂

Katika kijelesi hiki cha kimawasiliano, mwanafunzi huyu anawasiliana kwa matumizi ya ikonihisi ili kusisitiza maana lengwa ya usemi wake. Ikonihisi ambazo anatumia hapa ni za furaha ambayo pia ni kejeli.

Mitazamo ya Kipragmatiki Katika Mawasiliano ya Jukwaa la Facebook

2.9 Dhana ya pragmatiki

Utafiti huu unadhamiria kufanya uchanganuzi wa maana ya mawasiliano katika jukwaa la Facebook. Maana kusudiwa katika uchanganuzi wetu ni maana ya kipragmatiki inavyojidokeza katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook. Hata hivyo tumeona kuwa ni vyema kujadili dhana ya pragmatiki kama taaluma mojawapo ya isimu kama ilivyo fafanuliwa na wataalamu mbalimbali kwani, uelewa wa maana ya neno pragmatiki utatuwezesha kupata mwanga katika tafiti zetu.

Pragmatiki ni somo linalotalii maana ya msemaji. Taaluma hii hujishughulisha na maana jinsi ambavyo ujumbe umewasilishwa na mtu anayewasilisha ujumbe huo na kufasiriwa hadi kwa hadhira lengwa. Hivyo basi, pragmatiki huchunguza maana kimuktadha. Yaani ufasiri wa kile wasemaji wanakusudia kumaanisha kulingana na mazingira yaliyopo.

Vilevile jinsi muktadha unavyoathiri maana ya kitu au kitajwa kwani jumbe nyingi huwasilishwa kuliko jumbe zinazotamkwa. Taaluma hii huangazia jinsi ambavyo masuala mengi yasiyosemwa hutambuliwa kama kiungo cha yasiyowasilishwa. Wakati masuala Fulani yakitolewa na mwasilishaji wa ujumbe, msikilizaji hukabiliwa na jukumu la kubainisha maana kusudiwa katika mawasiliano.

Hata hivyo, huenda asipate maana kamilifu ya ujumbe uliyowasilishwa au kusudiwa kimawasiliano endapo hatatumia mchakato mwafaka kutambua ujumbe ambao mnenaji alikusudia kuwasilisha. Masamba (2004), anatoa ufafanuzi kuwa, pragmatiki ni taaluma ya isimi ambayo inajishughulisha na uchunguzi pamoja na uchambuzi wa lugha katika mawasiliano.

Msomu huyu anaendelea kudai kuwa, lengo kuu la taaluma hii ni kuchunguza namna lugha inavyotumiwa na wasemaji wake katika mazingira halisi, kama vile; Ni kwa nini msemaji ameamua kusema hivi badala ya kusema vinginevyo na anakabiliwa na masharti gani ya maamuzi?

Leech (1981), naye anaeleza kuwa pragmatiki ni maana ya matamshi, maumbo pamoja na miundo katika lugha. Mwanazuoni huyu anaendelea kwa kutoa madai kuwa, maana ni sehemu ya umilisi pamoja na ufahamu wa lugha, anasisitiza kuwa, kujifunza lugha ni kukubaliana na dhana za vipengele vyote vilivyopo katika lugha.

Richmond (2011), katika fafanuzi zake kuhusu dhana ya pragmatiki, anasema kuwa, ni tawi la lugha ambalo hushughulikia matumizi ya lugha kwa kuzingatia muktadha wa wazungumzaji wanao husika katika mawasiliano. Hivyo basi, pragmatiki inahusu masuala mawili ambayo ni; matumizi lugha na muktadha.

Yule (1996), kwa upande wake naye, anafafanua dhana ya pragmatiki kwa kusema kuwa, ni taaluma inayohusu mahusiano yaliyopo kati ya maana ya lugha na watumiaji wa mambo hayo.


Blutner (2011) akimrejelea Wilson (2003) na Carson (2002), anasema kuwa lengo la pragmatiki leksika ni kueleza michakato inaotumiwa katika ufasiri wa maana iliyosimbwa katika jumbe na kuleta suluhisho endapo kutakuwa na ugumu wa kimawasiliano. Michakato hii ndiyo hutofautisha dhana iliyowasilishwa na dhana iliyosimbwa kisemantiki. Michakato ambayo mwanaisimu huyu aliangazia katika pragmatiki leksika kimsingi ni kama vile: Kubanika kwa maana ya neno, kukisia kwa maana ya neno na Upanuzi wa maana ya neno.

2.10 Kubanika kwa maana ya neno

Kubanika kwa maana ya neno ni hali ambapo neno huwa linatumika kufafanua maana ambayo ni finyu kuliko dhana ambayo imesimbwa kisemantiki. Maana hiyo ambayo ni finyu lazima iwe ni fahiwa ambayo inahusiana na muktadha wa matumizi ya neno hilo. Wilson (2006), anatoa mfano kwa kutumia matabibu, ‘**Tabibu wote hunywa.**’

Kitendo cha kunywa kinafahamika kwa fahiwa pana. Kitendo hiki kina dhana ya kutia vimimina mdomoni na kupitisha kooni. Tunafahamu kwamba vimimina ni vingi kwa mfano: maji, soda, chai, pombe na sharubati. Lakini katika muktadha huu, ufasiri wa neno kunywa unajibana katika kubugia mvinyo na kufungia maana nyinginezo kama kupitisha chai au maji kooni. Tukirejelea muktadha wa mawasiliano katika jukwaa la Facebook, maana ya neno rafiki inajibana kwa kumaanisha mtu ambaye mnawasiliana naye katika kurasa za Facebook lakini kisemantiki, maana ya neno hilo ni pana kwa mfano, rafiki ni mtu anayekujali katika hali zote za kimaisha, na pia neno rafiki laweza kutumika kumaanisha mpenzi yaani, mtu mnayejamiana kimapenzi.


Kuongezea, wanafunzi ambao hushiriki ibaada ya kikiristo huwa na mazoea ya matumizi ya neno bwana neno ambalo katika muktadha wa ulokole neno hilo hutumiwa kumaanisha mwana wa Mungu ‘Yesu’ kwa hivyo neno bwana katika muktadha linabanwa na kufungia maana nyingine nje kama vile; Bwana kumaanisha mume wa mtu, mwajiri wa mtu, tajiri na maana nyinginezo.



Kukisia kwa maana ya neno

Kukisia kwa maana ya neno, ni hali ambapo neno ambalo lina maana finyu linapanuliwa kimaana ili kuhusisha maana ya kitu ambacho kinahusiana nacho kimaana, tofauti na maana halisi ya neno hilo kiisimu. Suala hili mara nyingi huweza kujidokeza katika matumizi legevu ambayo yanahusu idadi za kijumla. Kwa mfano, mtu akiulizwa kuwa, ni watu wangapi wanawasiliana kupitia jukwaa la Facebook halafu jibu lake liwe kuwa maelfu na maelfu ya watu

kumaanisha kuwa ni watu wengi sana ndio huweza kuwasiliana kupitia kwa jukwaa la Facebook. Tukitazama jibu la usemi kama huu tutabainisha kuwa maana yake ni matokeo ya kukisia kwa maana ya neno hilo.



2.11 Kupanuka kwa maana ya neno

Katika hali hii, neno ambalo lina dhana finyu linatumika kutoa fahiwa ya kijumla. Hivyo basi, maana ya neno hilo huweza kupata upanuzi zaidi kuliko lilivyo katika kategoria ya kisio la maana. Blutner (2011) akimrejelea Sweetser (1990), ambaye anadokeza mifano ya maneno ya kiutambuzi kwa kuangazia kitenzi ona. Neno ambalo lina dhana ya kutazama kitu kwa kutumia macho au kufanya utambuzi.

Kimuktadha, neno ona linaweza kutumika kumaanisha picha anayokuwa nayo mtu kwa akili yake kuhusu suala au masuala Fulani au kutabiri. Kwa mfano katika mawasiliano mtu akiambia mwengine kwamba, ... 'Niliona ukiwa njiani ukielekea hapo ulipo.' kumaanisha mwenzake alijua alichokuwa akifanya kwa nia ya kutimiza malengo yake na mwishowe akapata ufanisi. Hivyo basi, neno ona lenye maana finyu ya kutazama kwa kutumia macho linaweza kutumiwa kutoa maana nyingine kimuktadha kuhusu picha anayokuwa nayo mtu akilini au kutabiri.


Kwa hiyo, nafasi ya ufasiri wa kimaana huweza kupanuliwa zaidi. Sweetser (1990), anaeleza kuwa mambo kama haya yanahusiana na mpangilio wa kiakili katika ruwaza yake.

Tukimrejea Wamitila (2008) katika ufafanuzi wake kuhusu upanuzi wa maana, anatoa madai kuwa, upanuzi wa kimaana hutokea pale ambapo neno linapanuliwa kimaana. Yaani maana mahsusi ya neno inapanuliwa na kuwa maana ya kijumla. Anaendelea kwa kusema kuwa

upanuzi huu unaweza kuchochewa na mandhari ya matumizi ya lugha kijamii, kiuchumi, kisiasa na hata kisaikolojia. Mfano ni neno kupe ambalo zamani lilikuwa na maana ya mdudu anayenyonya damu lakini neno hilo likapanuliwa kimaana kujumlisha mtu anayetegemea kula kwa jasho la wengine. Mfano mwingine ni neno Mburugenge ambalo lilimaanisha aina ya mnyama tu lakini katika muktadha wa mazungumzo, neno hili huweza kujumlishwa na kumaanisha mtu ambaye haelewi mambo akiambiwa au mjinga.

Oiro (2014) akiwarejelea Hock na Joseph (1996) ambao wanadai kuwa, njia moja kuu ambayo kwayo maneno hupata fahiwa mpya na dhana panuzi ni kupitia kwa matumizi ya sitiari. Kwa mfano fahiwa iliyosimbwa kisemantiki ya neno ‘Simba’ ni mnyama wa porini ambaye ni mkubwa na anachukuliwa kama mfalme wa wanyama wengine.

Tukitumia neno hilo kwa mfano; ‘**Barasa ni Simba.**’ Maana ya usemi huu ni kuwa Barasa ambaye ni binadamu ni mkali kwa hivyo maana ya neno hilo imeweza kupata upanuzi wa kimaana.



Kwa ujumla, tunaweza kusema kwamba pragmatiki ni taaluma ambayo inahusiana na matumizi halisi ya lugha katika muktadha tofauti na uelewa wake kama vile; malengo hayo. Kwa mfano, matumizi ya lugha katika muktadha wa vinywaji ambapo mtu anaweza kusema ... ‘leta jinsi tulivyo.’

Usemi huo unaeleweka tu kwa watu ambao wanaburidika kwa vinywaji. Mfano wa vimimina kama vile; sharubati, Soda, Maji, chai na vileo. Iwapo ni muktadha wa mazungumzo mkahawani, basi usemi huo utakuwa unamaanisha kuwa mhudumu alete chai, soda au sharubati lakini katika

mazingira ya mauzo ya vileo, msemaji anasema hivyo kuleta maana ya kuletewa vinywaji vya kulevya.

2.12 Semantiki leksika

Semantiki leksika inashughulikia maana ya neno. Taaluma hii inatupa mwanga kwamba maneno yanaweza kuchukuliwa kuashiria vitu katika ulimwengu wa kisasa kwa utegemezi wa mtazamo mahususi wa kisemantiki leksika. Mmbawanga (2010), anatoa madai kuhusu taaluma ya semantiki leksika kwamba, vitengo vya fahiwa katika semantiki leksika ni vitengo vya kileksika ambavyo kwavyo msemaji anaweza kuongezea kwa mfululizo maishani pamoja na ujifunzaji wa maneno mapya pamoja na fahiwa za maneno hayo.

Kwa mfano: Neno kama vile; Baba ni neno ambalo maana yake kiisimu ni mzazi wa kiume ambapo neno hili limeongezewa fahiwa mpya ya baba wa kisiasa au mkuu wa eneo Fulani.

Katika mazingira ya wanafunzi wa chuo kikuu, wanafuzi huweza kutumia neno baba katika mawasiliano yao kwenye jukwaa la Facebook kumaanisha mkubwa wao katika kitengo cha uongozi wa wanafunzi. Vilevile, neno mchawi kiisimu lina maana ya mshirikina lakini katika muktadha wa mawasiliano ya wanafunzi chuoni, neno mchawi hufasiriwa kuwa ni mtu mashuhuri katika jambo. Mfano katika sentensi;

Chesoli ni mchawi katika somo la hesabati. Hapa panaonyesha kuwa, binadamu wana uwezo wa kuongezea vipashio vipya vya kimaana kwenye maneno kama katika neno, Mbabe wa siasa kuashiria mtu aliye na umarufu katika masuala ya siasa.

2.13 Lugha na mawasiliano

Mawasiliano ni hali ya kuhamisha ujumbe kutoka kwa mnenaji hadi kwa hadhira, kwa matumizi ya lugha.

Haya ni kwa mujibu wa Buliba na wenzake (2006). Wasomi hawa katika ufafanuzi wao kuhusu suala hili, wanaendelea kudai kuwa ujumbe unajumulisha mawazo, taarifa, hisia na mwelekeo wa mwasilishaji kulingana na namna anavyoelewana na walengwa katika mawasiliano.

Mzungumzaji yeyote Yule anapowasiliana kwa matumizi ya lugha yoyote ile huwa na lengo la kuwasiliana kikamilifu na wasikilizaji wake.

Tukimrejelea King'ei (1992), mawasiliano yanaweza kuwa, iwapo maneno yanaotumika ni yenye kueleweka kwa urahisi na binadamu wanaohusika kimawasiliano.

Anaendelea kutoa madai kuwa katika mawasiliano ya lugha ni lazima mtu ambaye anawasilisha ujumbe Fulani aweze kuutoa ujumbe kwa njia ambayo walengwa wataweza kuufasiri bila matatizo yoyote kwani, yule anayeutoa ujumbe huwa na lengo Fulani ambalo hutarajia kuwa anayeupokea ujumbe aweze kuupokea jinsi ulivyo. Katika mawasiliano, kuna mambo ya kuzingatia kama vile: Mtungaji ujumbe, njia ya mwasiliano, mpokeaji wa ujumbe na muktadha au mazingira ya kimawasiliano.

2.13.1 Mtungaji ujumbe

Huyu ni mtoa ujumbe ambao anaulenga kufikia hadhira ambayo inaweza kuwa lengwa na isiyolengwa kimawasiliano pamoja na jinsi ambavyo analenga kumwathiri ama kuwathiri wasikizaji.

2.13.2 Njia ya mawasiliano

Hii ni hali inayoleta athari kwa kujumlisha msimbo, mtindo, mbinu na chombo kinachotumiwa na mwasilishi wa ujumbe kwa ajili ya kukidhi haja ya kimawasiliano.

2.13.3 Mpokeaji ujumbe

Mpokeaji wa ujumbe ni binadamu ambaye anakusudiwa kuupokea ujumbe wa kimawasiliano na jinsi anavyojitambulisha mwenyewe na pia kutambulishwa na mwasilishaji wa ujumbe katika mawasiliano.

2.13.4 Mukadha

Haya ni mandhari ambayo mawasiliano yamechukua hatamu. Mukadha ni maana ya usemi pakubwa. Mawasiliano yoyote yale yanaweza kukamilika au yanaweza kukosa kufanikiwa kwa kwa misingi yoyote ile ambayo inaweza kufanikisha au kuzuia mawasiliano hayo.

2.13.5 Lugha na mukadha

Mukadha wa usemi Fulani unaweza kuathiri maana ya mawasiliano kwa kiasi kikubwa au jinsi maneno katika mawasiliano hayo yatakavyofasiriwa. Mandhari hayo yanaweza kuwa ya kimazungumzo au ya kimapokezi, kwani kuna mandhari pokezi na mandhari asili. Haya ni kwa mujibu wa Romany (2010) akimrejelea Wavriner na Francis (1977) ambao wanataja aina mbili za mukadha kama, mukadha wa kiisimu na mukadha halisi.

2.1.5.1 Muktradha wa kiisimu

Muktradha wa kiisimu ni muktradha ambao unajihusisha na matumizi ya matini au sentensi ambazo neno limetumika. Yule (2004), anatoa tetezi kuwa, mandhari ya kiisimu hudokeza fahiwa za maneno kama yanavyojidokeza kwenye mazingira ya maneno katika kipindi kimoja. Msomi huyu aliwauliza wanafunzi kutunga sentensi kwa minajili ya kubainisha maana tofauti za neno kata kisha akaweza kupata majibu yafuatayo:

1. Mkulima alikata roho.
2. Juma atakata mti wa kuni.
3. Masengeli amekata kauli.
4. Sara amechota maji mtungini kwa kata.

Kulingana na sentensi hizi, inadhihirika kuwa neno kata likitumika pamoja na maneno mengine kama roho, Mti, kauli na mtungi, inakuwa rahisi kubaini maana kusudiwa katika mawasiliano kwani, maana ya neno hupatikana kwa kulihusisha hilo neno na maneno mengine yaliyotajwa. Hata hivyo, katika mawasiliano vijana wanapotumia neno kama kata ambacho ni kitawe, maana zingine za maneno kama haya hubanwa na kufungia maana zingine nje hivyo basi, ufasiri wa maana kusudiwa hutegemea mazingira ambayo mawasiliano yalitokea.

2.13.5.2 Muktradha wa hali halisia

Huu ni muktradha ambao unarejelea mandhari mahsusi ambamo neno linatamkiwa. Inakuwa vigumu kwa mtu asiyekuwa katika mazingira hayo kuelewa suala lilokusudiwa. Hii ndiyo maana katika jukwaa la Facebook, kuna kurasa za makundi mbalimbali ili mawasiliano ya kila kundi yaweze kueleweka kulingana na miktadha mbalimbali. Hali ya kimazingira inamaanisha kuwa ni lazima kushuhudia matendo katika hali halisi ili kuweza kung'amua maana za matendo hayo. Hivyo basi, aina moja ya muktradha wa kipekee haiwezi kutosheleza mahitaji ya kueleweka kwa msamiati kwani, ni sharti aina zingine za muktradha zihusishwe kikamilifu. Lugha mbayo inatumika katika makundi tofauti ya kijamii hutofautiana na ina sifa zake mahsusi.

Nia ya matumizi yoyote ya lugha hiyo ni kukamilisha mawasiliano. Ili mawasiliano yaweze kukamilika, msikilizaji anapaswa kufasiri ujumbe kwa njia inayokusudiwa na mzungumzaji. Jambo ambalo hutegemea uelewa wa muktradha wa mzungumzaji na msikilizaji.

2.14 Hitimisho

Katika sura hii, ni bayana kwamba Facebook ni jukwaa la mawasiliano ambapo watu hukutana na kuweza kujadiliana. Hata hivyo matumizi ya lugha katika Facebook huchukua mtazamo wa michakato ya kipragmatiki. Isitoshe sura hii imeweza kutuonyesha historia ya Facebook na mifumo ya mawasiliano ya jukwaa la Facebook pamoja na mitazamo ya kipragmatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook. Miongoni mwa mifumo ambayo imejadiliwa ni sifa za mawasiliano ya jukwaa la Facebook kama vile; usilabishaji, matumizi ya lugha ya Kiswahili, uchanganyaji msimbo, matumizi ya mkutano duara na matumizi ya picha na ikonihisi.

SURA YA TATU

UPANUZI WA MAANA KATIKA MAWASILIANO YA JUKWAA LA FACEBOOK

3.0 Utangulizi

Katika Sura hii tutajadili jinsi mawasiliano ya Facebook yanavyoibua maana kisemantiki na kipragmatiki kulingana na nadharia ya pragmatiki leksika. Tutatumia nadharia ya pragmatiki leksika katika uhakiki wa sura hii ambayo mwasisi wake ni Reinherd Blutner. Nadharia ambayo iliasisiwa mnamo mwaka wa (1990). Isitoshe, Sura hii itaangazia jinsi ambavyo wanafunzi wa chuo kikuu wanavyoipanua maana ya maneno kwa kutumia mikakati ya kipragmatiki katika mawasiliano yao ya jukwaa la Facebook na kwanini mawasiliano ya Facebook huweza kuchukua mkondo wa upanuzi wa maana. Haya yote yataangaziwa kwa mujibu wa pragmatiki leksika.

Wanafunzi wa chuo kikuu nchini Kenya katika mawasiliano yao ya jukwaa la Facebook, hulenga kukidhi mahitaji yao ya kimawasiliano miongoni mwa wanakikundi katika mawasiliano yao kupitia jukwaa la Facebook .

Matumizi ya usemi kipragmatiki, yanaweza kuleta mafanikio au kuwa kizuizi katika mkabala wa mawasiliano kwa njia moja au nyingine.

Hii ni kutegemea jinsi makundi mbalimbali ya wawasilinaji wanavyofasiri ujumbe katika mawasiliano kwani, wanaweza fasiri maana kusudiwa katika usemi Fulani au wapotoke kimaana.

Maana ya kiisimu kama kawaida hutofautiana na maana ya kipragmatiki yaani, maana inayofasiriwa kulingana na muktadha wa mawasiliano. Hata hivyo, wawasilinaji katika makundi tofauti ya wanafunzi wa chuo kikuu huwasiliana kutumia maneno fulani kimakusudi wakiwa na malengo yao kibinafsi, lakini baadhi yao hujipata wametumia msamiati Fulani kimawasiliano bila kukusudia. Hivyo basi ufasiri wa maana ya ujumbe katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook unabaki kwa hadhira lengwa.

Katika utafiti huu, tunalenga mawasiliano ya jukwaa la Facebook ambako data itakayofanikisha tasnifu hii itatolewa kwa makundi ya wanafunzi wa chuo kikuu. Makundi ambayo tumelenga ni kama yafuatayo: Kenyan university students, Kenya universities organization na K.U. Comrades Forum.

3.1 Upanuzi wa kileksika katika mawasiliano

Huu ni mchakato ambao neno linatumiwa kuonyesha fahiwa ya kijumla zaidi kuliko ile iliyosimbwa kisemantiki, huku ikitoa mfululizo wa upanuzi wa maana mahsusi ya kiisimu. Haya ni kwa mujibu wa Wilson na Carson (2007). Fromkin na Rodman (1978) katika maelezo yao kuhusu suala la upanuzi wa kileksika nao wanadai kuwa, upanuzi wa kileksika ni mchakato wa kileksika ambao kwao maana ya neno hupanuka kwani, neno linamaanisha kila kitu kilichokuwa kikimaanishwa na kuweza kuongezea fahiwa nyingine zaidi kulingana na mazingira ya kimawasiliano. Utafiti huu nao unaongezea kuwa maana ya neno huweza kutambulika kisemantiki lakini maana nyingine zaidi ya maana msingi huweza kuibuliwa au kuchipuka. Katika kuzuru jukwaa la Facebook, tuliweza kubaini kuwa wanafunzi wa chuo kikuu wana lugha yao ya kukidhi haja yao ya kimawasiliano ambayo kwao maana za maneno hupanuliwa ili kuweza kukamilisha mawasiliano kulingana na muktadha wa mazungumzo yao. Kauli tulizonakili kutoka Facebook ni kama zifuatazo;



Christopher Masengeli

9 Machi saa 15:53 .

Walai! , wanasiasa wasomi hujibeba katika mijadala kwenye seneti na parliament jameni? Kumtoa mwenzako rangi Hadi umwambie mwenzako jinzi wewe una shahada ya uzamili na unafundisha chuo kikuu. Ni ukosefu wa mvi, kwani waliyo na mvi hujadili masuala ya ujenzi wa taifa ila si kujipiga kifua Hadi inzi wa chooni kukujua. imagini, going ahead and defining fellow politicians how they graduated posting of upper second you have.

Penda 🤔🤔🤔

Maoni

Shiriki

Katika muktadha wa mawasiliano haya, mwanafunzi huyu anatumia neno ‘**kujibeba**’ kumaanisha kujishaua ama kujisifu ilihali tunafahamu fika kuwa maana ya neno beba kisemantiki ni kunyanyua mzigo au kitu kutoka sehemu moja hadi nyingine. Hivyo basi, maana ya neno beba imepanuliwa kumaanisha kujishaua.

Isitoshe, Maana ya msingi ya kutoa rangi ni kupanguza rangi kutoka mahali au kwa kitu ambacho kimepakwa rangi ili kukinadhifisha lakini katika mazingira ya mawasiliano haya, inabainika kuwa neno hili (kutoa rangi) limepanuliwa kimaana kumaanisha kudunisha.

Simiyu (2016) anatoa maelezo kuhusu upanuzi wa kiistiari kuwa, upanuzi wa kiistiari ni mchakato ambao kwayo fahiwa ya neno haikaribiani na dhana iliyo wazi kiufafanuzi. Yaani, maana ya neno Fulani katika mandhari ya mazungumzo ni tofauti kabisa na dhana ya neno hilo katika mazingira ya kiisimu. Utafiti huu unaunga mkono maelezo ya msomi huyu na kuongezea kuwa, katika upanuzi wa kiistiari, maana ya neno huwa inakuwa mbali na maana halisi ya neno mara nyingi kwa kuhamisha maana ya neno kusudiwa kutoka kiashiria kimoja hadi kiashiria kingine kilicho mbadala.

Katika muktadha wa mawasiliano yayo hayo ya Christopher Masengeli, tunaona matumizi ya neno **Mvi** ambapo kisemantiki neno mvi linatumika kwa maana ya nywele nyeupe iotayo kichwani lakini katika mawasiliano haya maana ya neno hili imepanuliwa na kupata maana ya busara, huu ni upanuzi wa kiistiari. Mara nyingi, wanafunzi hutumia aina hii ya upanuzi kwa lengo la kusetiri ujumbe wao kwa hadhira pana ili ujumbe wao uweze kuifikia hadhira ya wasomi pekee na kuwapa mielekeo miema katika jamii pana. Kwa mfano, katika muktadha huu si kila mtu anaweza pata uelewa wa matumizi ya neno mvi bali himaya ya wasomi.

Pia matumizi ya usemi **kujipiga kifua** hadi inzi wa chooni kukujua ni upanuzi kwa sababu maana halisi ya neno kupiga ni kugonga kitu au mtu kwa nia ya kuumiza lakini katika muktadha wa mawasiliano haya, mwanafunzi huyu ametumia neno hili kumaanisha kujisifu ambapo neno piga limeweza kupanuliwa kimaana.

Kulingana na Carson (2002), katika ufafanuzi wao kuhusu suala la upanuzi, wanatujulisha kwamba, upanuzi wa kileksika unaweza kusababishwa na mabadiliko mengine madogo madogo kama vile chuku na istiari. Matumizi ya neno inzi katika mawasiliano ya Christopher kimuktadha, yanatuonyesha maana panuzi ya neno nzi kwani, ni bayana kuwa maana iliyosimbwa kisemantiki ya neno hili ni mdudu anayepatikana katika mazingira machafu lakini katika usemi(kujipiga kifua hadi inzi wa chooni wakujue), ni upanuzi wa chuku ambao umetumiwa kumaanisha kuwa kujisifu hadi watu wasiyo na hadhi au watu baki wakujue.

Hivyo basi neno inzi kama mdudu linapanuliwa kimaana kumaanisha binadamu wasiyo na hadhi duniani. Aina hii ya upanuzi huweza kutumiwa ili kusisitiza jumbe zilizowasilishwa kwa hadhira lengwa.



Charles Muchika

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)



· 9 Machi saa 12:26 ·

Viongoz wengine ni mbwakoko jameni kwani asubuhi wamevalia tai wako kwa mwenye kiti wa jubilee kisha usiku wametamba kwingine lakini kuona kwake moses kuria kwamba Raila na DP watafanya kazi pamoja kumenistajabisha sana, na iwapo yatawezekana kutimia basi moses ni unju wa kuona matukio mengi yajayo mbeleni. I meant some leaders or other leaders whichever your way of perception

Penda 😂😂😂

Maoni

Shiriki

Katika mawasiliano haya, Mwanafunzi huyu anatumia usemi kwamba viongozi wengine ni **Mbwakoko**. Tunajua bayana kwamba Mbwa ni mnyama na Mbwakoko ni Mbwa mtembezi lakini katika muktadha huu , neno Mbwakoko limeweza kupanuliwa kimaana kutoka kwa maana yake asilia na kumaanisha binadamu asiye na msimamo maishani yaani, mtu anayetapatapa hapa na pale.

Mwandishi wa ujumbe huu ameweza kuwasilisha kwa matumizi ya mchakato wa upanuzi wa kiistiari sababu kuu ikiwa kuusitiri ujumbe huu wa mawasiliano ili uwafikie tu wasilikilizaji au kundi la kimawasiliano analolenga na pia makusudi mengine ni kwa nia ya kukuza lugha na kuzua misamiati mipya yenye maana tofauti na hata katika kuwasilisha ujumbe kwa kusema kuwa, viongozi wengine ni Malaya au makahaba, maneno ambayo yanajulikana wazi kama wanawake ambao hukubali yeyote yule anayetaka kushiriki nao kimapenzi, amefaulu kupunguza makali kwa kutumia sitiari ambayo imeficha maana kwani, bila ufafanuzi huwezi kujua maana kamilifu.

Blutner (2001), akiwarejelea Katz na Fodor (1963) wanatuelemisha kuwa, fahiwa ya neno inategemea mandhari ambayo sentensi hiyo imechipuka. Kulingana na Foder (1963), mandhari yanahusu habari za awali, masuala ya kijamii na ujuzi wa kiisimu. Wanaisimu hawa wanaendelea kwa kusisitiza kuwa, fahiwa kamilifu ya neno inapasa kuhusisha habari zaidi inayomwezesha binadamu wa Maulana kuchanganua maana ya maneno tofauti. Utafiti huu unashadidia mawazo haya kwa kutoa idhibati ya maneno ambayo yanadhihirika katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook kwa mfano;

Katika kijejezi cha mawasiliano ya Muchika hapo juu, kuna usemi “**Moses ni unju wa kuona matukio mengi yajayo mbeleni.**” Ambapo maana ya neno unju linamaanisha mtu ambaye anasemekana kuwa ameishi hapo kale.

Maelezo yake yanapatikana katika makala ya ibaada ya makumbusho ya kaole huko bagamoyo nichini Tanzania. Mojawapo masuala ya kiajabu ya binadamu huyu ni urefu wake yaani kimo, tunaarifiwa kuwa alikuwa na urefu mkubwa ambao uliweza kumfanya atembe baharini na kugusa miguu yake chini. Pia alikuwa akitembea kwa maguu yake kutoka nchi hadi nchi kwa sababu ya urefu wake. Moja kati ya nyayo zake tunaarifiwa kwamba zinapatikana kwenye jiwe ambalo aliweza kuganyaga kule mjini tabora, Tanzania, nyayo ya mguu wa shemali wakati unyayo wa mguu wa kulia nao unasemekana kuwa ulionekana kwenye jiwe ambalo alikuwa ameganyaga huko nchini Congo. Wanahistoria wanatutolea maelezo katika makala ya kihistoria kuwa unju alipofariki dunia aligawanyika vipande kwa vipande kutokana na urefu wake pia, inasemekana kwamba kidole chake kilichokuwa na urefu wa kasoro kilomita moja, ndicho kilichopatikana na kuzikwa pale bagamoyo, hadi sasa haijaleweka wakati alifariki dunia

kiwiliwili cha mwili wake kilichobaki kiliangukia wapi. Aliishi Afrika na endapo alipotaka kula alikuwa akichukua samaki ndani ya bahari kwa kutumia mkono na kuchoma kwa jua kisha anakula.

Kutokana na maelezo haya ya kihistoria, mawazo ya wanaisimu hawa yanapata mashiko kwani matumizi ya neno **unju**, kwa kifungu hiki cha mawasiliano yanaibua maana panuzi ya mtu ambaye ana uwezo wa kuangaza masuala yaliyo mbeleni. Hivyo basi dhana hiyo imetumika kuusetiri ujumbe huo kwa kikundi kilicho lengwa pekee na lazima maana kusudiwa ifasiriwe kimuktadha.

Mfano mwingine katika kifungu hicho cha Charles, ni matumizi ya neno ‘**ona**’ kisemantiki, neno hili linatumika kumaanisha, tambua na kufahamu kwa macho, angalia au tazama lakini katika muktadha wa mawasiliano ya kikundi hiki, mwanafunzi huyu anatumia neno hili kimakusudi kuleta maana mpya ya neno hili kumaanisha tabiri.

Hivyo basi neno **ona** linapata upanuzi wa kimaana ndiposa utafiti huu unaendelea kushadidia mtazamo wa Katz na Foder (1963) kwamba maana ya neno inategemea mandhari ya sentensi hiyo.



Zablon Orangi

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

8 Machi saa 21:00 ·

Janga la korona liliporipotiwa nchini Tanzania na vyombo vya habari, Rais Maghufuli alikuwa simba. Kufuatia madai hayo, mambo ambayo alidai ni upuuzi kwa madai kwamba yeye ni msomi wa Kemia. Leo hii mambo yakoje Tanzania? Kauli yako ni ipi kwa huyu mwalimu wa Kemia? 😞😞😞

11

Penda

Maoni

Shiriki

Katika muktadha wa mawasiliano haya, Orangi anamlinganisha mwendazake Maghufuli na simba. Kisemantiki, Simba ni mnyama ambaye anajulikana kuwa mfalme wa wanyama wengine na pia anajulikana kwa tabia ya ukali.

Katika kifungu hiki neno hili linapata upanuzi wa kimaana kumaanisha binadamu ambaye ni mkali ambapo mwasilianaji analeta maana kimuktadha kuwa, ukali wa mfalme huyu wa Tanzania ulimfanya kupuuza kwamba matangazo kuhusu janga la korona yalikuwa ya ukweli. Huu ni upanuzi wa kiistiari ambao umeweza kupunguza makali ya ujumbe huu na kuusetiri kwa kundi lengwa ambalo ni kundi la wasomi pekee.



Manu Manu

Kenya Universities Student Organization

18 Aprili saa 20:26 ·

Ukitaka kukatia fresher,, Unanza na neno gani?

Katika kijejezi cha mawasiliano haya Manu Manu anawasiliana kwa matumizi ya neno ‘**kukatia**’ maana iliyosimbwa kisemantiki ni hali ya kutenganisha kitu kwa vipande kwa niapa ya mtu fulani. Katika muktadha wa mawasiliano haya, neno hili linapata ufasiri wa maana ya kutongoza msichana kwa ajili ya mahaba au uhusiano wa kimapenzi. Hivyo basi neno kukatia linapata upanuzi wa kimaana. Upanuzi huu unafanyika kwa sababu ya kusetiri ujumbe na kunadhibisha ujumbe huu wa kimawasiliano kwa wanakikundi.



Kennedy Shavanga

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

9 Machi saa 22:23 ·

Mvua ya gharika ni chumo kwa wakulima wa mahindi pamwe na miwa, ambacho ni kinaya kwa wakulima wa nyanya. rasharasha huwafanya wasiopenda kazi kuhema kwa kutafuta mtaji nao wanaopenda vya dezodezo hubaki kikawaida wakijua kwamba wataendelea kuwa kupe kwa mahuluki wenye idili. Ni heri wasomi wavyuo kuwapiga msasa wanagenxi wao ili wasijute maishani na pia wawe dira ya ulimwengu katika siku za mwambo

Penda

Maoni

Shiriki

Katika mawasiliano haya mwandishi ametumia neno **kupe**; dhana iliyosimbwa kisemantiki, neno hili hutumika kumaanisha mdudu ambaye hulaza wanyama damu au watu ambao hutegemea jasho la wengine lakini tukizingatia matumizi ya neno hili kipragmatiki, shavanga anamaanisha kuwa kupe ni mtu anayewategemea kula kwa jasho la wengine.

Isitoshe, mwandishi pia amehimiza wasomi wa vyuo kuwapiga msasa wasomi wao ili wasijute maishani ila wawe dira ya ulimwengu siku za mwambo.

Neno **dira** kisemantiki linatumika kumaanisha kifaa chenye kuonyesha pande za dunia kinachotumiwa na wasafiri hasa wa anga na baharini kuwawezesha kutambua upande wanaelekea, kuondoa nywele kichwani, mawazo anayojiwekea mtu au kikundi kuhusu namna ya kufanya jambo, aina ya nguo. Kipragmatiki neno hili linapata ufafanuzi kimuktadha na kufasiriwa kama kielelezo cha maadili. Hivyo basi, maneno haya **kupe** na **dira** yanapata upanuzi wa kimaana ambao ni upanuzi wa kiistiari.



Naomi Mwendu

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

5 Machi saa 20:16 ·

Uchaguzi mdogo uliofanyika Kabuchai umefanya ubabe wa shingo wa Rais nchini kushuka bei na kuwezesha Weta kupanda kidhamana.

Penda 🤔🤔🤔

Maoni

Shiriki

Lawless (1988) katika tetezi zake anatufahamisha kuwa, makundi ya binadamu wa Mwenyezi Mungu na tamaduni hukuza lugha maalumu zinazoeleweka tu kwa wanakikundi hicho. Lugha hii maalumu huweka mipaka kuwatenga na kuwaweka wanakikundi pamoja. Tukizingatia kauli ya

msomi huyu, matumizi ya neno **ubabe** na **shingo** ni ubunaji wa maana mpya na uundaji wa leksimu ambazo kwao wanakikundi hiki wanapata uelewa wa maana na kuwaweka pamoja wanakikundi hiki.

Kisemantiki, maana ya neno shingo ni sehemu ya mwili ambayo inaunganisha kichwa na mwili lakini kulingana na muktadha wa mawasiliano ya kikundi hiki, neno hili (shingo) limetumika kumaanisha mtu anayefuata mwengine kimamlaka katika daraja ya uongozi. Hivyo basi neno hili linapata upanuzi wa kimaana. Pia, neno **ubabe** limeundwa kutoka kwa neno baba ambalo linamaana ya mkuu au mzazi wa kiume lakini ubabe ni leksimu ambayo imeundwa kuleta maana ya ubingwa kwa hiyo neno hili limeweza kupata upanuzi wa kimaana ili kuusetiri ujumbe wa mawasiliano ya wanakikundi.



Vincent Kasembeli

Saa 7 .

Waziri Wa elimu nchini alifua dafu kwa kudadisi masuala nyeti ambayo yalikuwa mwiba katika uchanjaa Wa elimu. Hata hivyo washikadau Wa wizara hiyo waliweza kutoboa chanzo cha Shule nyingi kupitisha wanafuu wengi katika kategoria ya A' kisha mikakati ya kuzipa mwanya huo ikatekelezwa. Hivi sasa ukicheza Na mitiani ya kitaifa ati unauzia watahiniwa utauma copper kisha utaweza kuiona nchi ya Tisa, Kongole kwa bwana prof.

11

Katika kijejezi cha mawasiliano haya , mwanafunzi huyu anawasiliana kwa matumizi ya neno **'kutoboa'** kimsingi, neno hili hutumiwa kwa maana ya kutia tundu au shimo kwa chombo ili kiweze kupitisha kitu bila kizuizi chochote. Katika muktadha wa mawasiliano haya neno hili limetumika kwa maana ya kufichua siri. Hivyo basi neno kutoboa limepanuliwa kimaana katika mwasiliano haya ya jukwaa la Facebook. Upanuzi huu unafanyika kwa sababu ya kusetiri ujumbe wa kimawasiliano kwa wanakikundi.

Katika mawasiliano haya pia, mwanafunzi huyu anawasiliana kwa matumizi ya maneno, **'yalikuwa mwiba katika uchanjaa wa elimu'** Kimsingi mwiba ni kitu kinachoumiza kinapokukudunga mwilini. Katika muktadha wa mawasiliano haya neno hili limetumika kwa

maana ya kitu chochote ambacho kinaweza leta madhara. Hivyo basi neno hili linapata upanuzi wa kiistiari kwa misingi ya kuusetiri ujumbe kwa wanakikundi na kuwaweka pamoja.



Aligura E.A.

Kenya Universities Student Organization



· **10 Februari** ·

Wale Wenye Principal Aliambia Hawatajoin Campus, Mlitoboa? 😊

152152

Maoni 50

Penda

Maoni

Katika mawasiliano haya kuna matumizi ya neno ‘**kutoboa**’ neno ambalo kisemantiki limesimbwa kwa maana ya kutengeneza tundu au shimo kwenye chombo au mtungi ili kupitisha kilichomo ndani bila kuwa na uwezo wa kujizuia lakini katika muktadha wa mawasiliano haya ya jukwaa la Facebook, neno hili linatiwa chuku ili kuleta maana ya kufaulu kukwepa mateso ambayo yanapatikana katika chuo kikuu. Hivyo basi basi neno kutoboa linapata upanuzi wa kimaana katika mawasiliano haya kimuktadha. Upanuzi huu unafanyika kwa minajili ya kuusetiri ujumbe na kuwezesha kuuficha machungu yaliyomo kwenye ujumbe.



Cleophas Nyongesa

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)



· **5 Machi saa 07:26** ·

Ilikuwa ni mguu niponye, kuchupa, kufokeana na vyombo vya dola kuonyesha ubabe wao katika maeneo yaliyokuwa na chaguzi ndogo. Baadhi ya waheshimiwa walijipata wametiwa nguvuni kwa kucheza ngoma mbaya siku ya kutambua mbivu na mbichi.

Mawasiliano ya Nyongesa pia yanashabikia upanuzi wa maana wa neno baba katika mbinu ya ubunaji wa maana mpya na uundaji wa leksimu ambapo tunaona matumizi ya neno **ubabe** kwa maana ya ubingwa.

Hata hivyo mwasilianaji huyu pia anatumia kifungu **kucheza ngoma mbaya**

Ambapo maana iliyosimbwa kisemantiki ni kuzungusha sehemu za mwili kufuatana na mdundo wa ngozi iliyowambwa (ngoma), lakini maana fasiriwa kulingana na muktadha ni kushiriki katika maovu au machafuko. Hii inaleta upanuzi wa neno kucheza ngoma mbaya kimaana.

Katika mawasiliana haya pia mwandishi wa makala haya anawasilisha ujumbe wake kwa matumizi ya maneno **mbivu** na **mbichi**. Kisemantiki, mbivu ni neno linalotumika kwa maana ya chakula au tunda ambalo limekuwa tayari kuliwa na mbichi ni kinyume cha mbivu lakini katika muktadha wa mwasiliano haya maana inayofasiriwa kizuri na kibaya. Hata hivyo maana ya maneno haya (mbivu na mbichi) yanapata upanuzi wa kimaana.



Cleophas Nyongesa

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)



· **3 Machi saa 07:23** ·

Kumepambazuka ulimwengu kote! Chanjo ya korona sasa ni pumzi na uhai wa lukuki ya watu kote duniani. Waliokuwa wametamaushwa na janga hilo sasa wana nanga ya kushikilia mashua yao isisombwe na mawimbi.

22

Katika chapisho jingine la mawasiliano, Cleophas anawasilisha ujumbe wake kwa matumizi ya kifungu; '**Chanjo ya korona sasa ni pumzi na uhai wa lukuki.**' Kisemantiki, neno pumzi linamaanika ya hewa ya kupumua na uhai ni hali ya kuwa na afya bora lakini maana inayowasilishwa kulingana na muktadha wa mawasiliano haya ni kuwa maisha ya binadamu sasa yamekitwa kwa chanjo ya korona. Nyongesa ametumia wa kimaana wa kiistiari ili kuonyesha umuhimu wa mahuluki kupata chanjo dhidi ya gonjwa hili.

Vilevile, kuna matumizi ya neno **nanga** ambapo maana msingi ya neno hili ni; kifaa kizito kifungwacho katika merikebu na vyombo vingine vya kusafiria majini vinapokuwa bandarini ili visichukuliwe au kusukwasukwa na maji. Lakini kipragmatiki neno hili linafasiriwa kwa maana ya kitu cha kuwapa afya maridhawa kwa hiyo neno hili linapata upanuzi wa kimaana.

Pia matumizi ya neno mashua ambapo maana iliyosimbwa kisemantiki ni chombo cha usafiri wa majini lakini kulingana na muktadha huu; Nyongesa analeta upanuzi wa maana ya neno hili kwa maana ya maisha. Kwa ufupi kifungu kizima kitakuwa: **kumepambazuka ulimwengu kote, chanjo ya korona ni ya muhimu sana kwa binadamu kote duniani. Waliokuwa wametamaushwa na janga hilo sasa wanachakuwalinda maisha yao yasiangamie.** Hii inatufanya kushadidia mawazo ya Ullman (1970) ambaye alitoa fafanuzi kuwa, maneno yanapewa maana moja bunifu au zaidi bila ya maana asilia na maana ya pili zinaishi upande na upande mradi tu pasiwepo na mkinzano.



Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

8 Machi saa 00:59 .

Kusoma ni ibada manake ukishasoma maisha ni asali.

Neno **asali** kisemantiki ni, nta iliyozalishwa na nyuki kwenye masega au uki na huliwa na binadamu au asali ni utamu au uhondo wa kitu. Katika muktadha wa mazungumzo haya, neno hili limepanuliwa kiistari na kuleta maana ya ufanisi au mafanikio maishani. Vilevile, neno ibada limesimbwa kisemantiki kwa maana ya shughuli ya kuabudu Mwenyezi Mungu hasa ndani ya majengo matakatifu pia ibada ni hali ya kuzoea kufanya jambo Fulani kwa hiyo neno kusoma linapanuliwa kimaana kuonyesha shughuli. Katika mawasiliano haya mwasilishi wa ujumbe huu anatomia neno asali ambapo tujuavyo maana ya kufanikiwa maishani.



Jackizo Wa Izoo

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

5 Machi saa 05:56 .

Wanaume watanashati huvaa kiasi Cha nzi wa uchafu kuwatoroka lakini hawatoboki jamani 😂😂
😂

6Virginia Simiyu, Cleophas Nyongesa na Wengine 4

Penda

Maoni

Shiriki

Katika mawasiliano ya Jackzo Wa Izoo, kuna matumizi ya neno **hawatoboki** ambapo sote tanajua kwamba neno kutoboka lina maana ya kupata tundu na kupitisha kilicho ndani ya chombo pasipo na uwezo wa kuzuia. Lakini matumizi ya neno hili katika muktadha huu linatiliwa chumvi kumaanisha kuwa wanaume watanashati hawawezi kutoa pesa. Chuku inatumika hapa kueleza sifa mbaya ya ugumu wa wanaume watanashati wa kutoa pesa.

Jackzo Wa Izoo katika mawasiliano yake anatia chuku mavazi ya wanaume watanashati kwa kusema kuwa, wao huvaa kiasi cha nzi wa uchafu kuwatoroka ambapo kimuktadha , mwasilishi wa ujumbe huu anamaanisha kuwa wanaume hao ni kawaida yao kuvaa mavazi ambayo ni nadhifu kwa kiwango cha kufikiriwa wanamiliki pesa mali mengi na kumbe hawana chochote. Badiliko hili linatumika hapa kwa minajili ya kuusisitiza ujumbe huu.



Steve Juma

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

2 Machi saa 04:19 ·

Watu walimwagika, uhurupark wakifikiria Rayo atatoboka katika huo mkutano hata hapakuwa na nafasi ya inzi kujipenyeza wala kutema mate

Steve Juma pia katika mawasiliano yake ameweza kutumia neno kutoboka kumaanisha hali ya kutoa pesa hivyo basi neno toboka lineweza kupata upanuzi wa kimaana ili kuusifia ujumbe huu, vilevile, anatia chuku kuelezea jinsi watu walikuwa wengi mkutanoni wakitarajia kupata pesa kutoka kwa Rayo.



Steve Juma

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

3 Machi saa 05:02 ·

Korona na karatasi ni homa zinazotishia aghalabu karatasi limethibitiwa na matumizi ya karatasi katika mahaba

Penda

Maoni

Shiriki

Katika mawasiliano haya; mwasilishi wa ujumbe huu ameweza kutumia neno **karatasi** amabapo sote tunaelewa kuwa dhana iliyosimbwa kisemantiki ya neno hili ni kitu laini chenye wembamba kinachotokana na vumbi la miti ambacho hutumiwa kuandikia, kutengeneza vitabu, magazeti na kutengeneza vifaa tofautitofauti. Lakini tukizingatia muktadha huu tutapata kuwa Steve amatumia neno hili kumaanisha ugonjwa wa ukimwi na pia mipira ya kondomu ambayo hutumiwa kama mbinu mojawapo ya kuthibiti Maambukizi ya Marathi ya Ukimwi. Hii ni dhihirisho kuwa maana ya neno hili kisemantiki imejitenga na maana iliyosimbuliwa kimuktadha na kuipa upanuzi wa kimaana.



Jackizo Wa Izoo

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

3 Machi saa 07:21 ·

Mibabe wa siasa wamechangamkia suala la BBI

Hadi vinywa vyao vikapanuka. 😂😂😂

Katika mawasiliano ya mwanafunzi huyu, tunaona matumizi ya neno **Mibabe**, neno ambalo limeundwa kutoka kwa neno ubabe ambalo linatumika kumaanisha; hali ya mtu kutumia nguvu au uwezo wake kudhulumu wengine au hali ya mtu kuwa shujaa. Lakini hapa tunaona ubunaji wa maana na uundaji wa leksimu mpya (mibabe) kuleta maana ya wajuzi wa siasa au watu wilio na ujuzi katika masuala ya kisiasa hivyo basi neno hili linapata upanuzi wa kimaana na kupata leksimu mpya katika lugha ya Kiswahili.

Vilevile; katika mawasiliano haya mwanafunzi huyu anatumia neno vinywa kupanuka ambapo tunajua fika kuwa maana msingi ya neno hili, ni hali ya kupanua midomo au kuufanya mdomo kuwa wazi. Lakini kwa kuzingatia muktadha huu, maana kusudiwa ni kule kuwa na njaa ya pesa yaani kutaka kuhongwa ndiposa waliunge suala la BBI mkono.



Steve Juma

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

3 Machi saa 04:38 .

Wanasiasa wa leo ni mabeberu wao huwa wana teketeke za kula serekalini tu.

Penda

Maoni

Shiriki

Steve juma katika wasilisho lake kwa kikundi , anawasiliana kwa matumizi ya neno **mabeberu** , neno ambalo limetokana na neno beberu lenye maana ya mbuzi dume ila katika muktadha wa mawasiliano haya, mabeberu ni wanyanyasaji kwa hivyo, neno hili linapata upanuzi wa kiistiari.

Isitoshe, Steve anaendelea kwa matumizi ya neno, **teketeke** ambapo teketeke ni leksimu mpya inayotokana na neno teke ambalo limefanyiwa urudiaji kwa kuambatanisha neno lilelile. Maana wazi ya leksimu teke ni pigo la mguu ambalo aghalabu hurushwa kwa kina kirefuhivyo, mtu anapotembea. Katika muktadha wa mawasiliano haya leksimu hii imetumika kumaanisha harakati za wanasiasa kula serekalini.



Steve Juma

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

2 Machi saa 04:22 ·

Kwaya ya KU INA Waridi wengi mno, mafisi waliwamezea sana siku hiyo ya graduation

1Simon Katui

Tia moyo

Maoni

Shiriki

Juma anawasiliana kutumia neno **waridi** maana msingi ya neno hili ni ua yaani sehemu ya mumeza inayo ning'inia. Lakini katika muktadha wa mawasiliano haya, neno hili linapanuliwa kiistiari na kuleta maana ya msichana mrembo anayependeza. Dhana ya kupanuka kwa kiistiari hutumika katika uwasilishaji wa ujumbe kwa sababu ya kuuficha ujumbe ule wa mawasiliano kwa kulenga tu hadhira Fulani.

Pia kuna matumizi ya neno **fisi** Fisi ni mnyama ambaye anajulikana kwa ulafi lakini katika muktadha wa mawasiliano haya neno hili limepanuliwa kiistari na kuleta maana ya mtu ambaye ni mlafi

Isitoshe, Kuna matumizi ya neno **meza** ambapo maana msingi ya neno hili ni kifaa cha kuandalia chakula au kuandikia, na hali ya kupisha chakula kooni. Lakini katika muktadha wa mawasiliano haya, neno hili linapanuliwa kimaana na kuleta maana ya kutamani.



Kimutai Godfrey

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

5 Machi saa 06:56 ·

Omba usikutane na watu ambao ni ndumakuwili in life, because life is not a rehearsal my friends.

Kimutai ametumia neno **Ndumakuwili** katika mawasiliano yake kwa kikundi. Maana iliyosimbwa kisemantiki ya neno hili ni mtu ambaye huchonganisha pande mbili kwa kujifanya mwema kila upande yaani; mnafikiri. Kimuktadha, neno hili linapanuliwa kiistiari kumaanisha binadamu asiye wazi. Kimutai ametumia sutiari hii kwa kuusetiri ujumbe wake kwa wanakikundi ili kuwaonya dhidi ya marafiki wasiojulikana waliko simama.



Christopher Masengeli

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

8 Machi saa 20:42

Kikombe kilitembea katika chaguzi zilizohitimika lakini wanainchi walikuwa tayari wamekata kauli kuwa, silaha zao zitawaendea viongozi waliyo na uwezo katika masuala ya uongozi. Viparaka walikuwa wamekunywa na kumeza unga lakini wembe haukukawia kuwakata.

Upanuzi wa kimaana ambao unaitwa metonimi unajitokeza katika mawasiliano ya Masengeli ambaye anatumia neno **kikombe** linalomaanisha kifaa kinachotumiwa kunywa vitu vya majimaji, aina Fulani ya kufuli linalozuia umeme usitoke, sehemu ya gurudumu la baiskeli au gari, taji lenye linalopewa washindi michezoni. Lakini katika muktadha wa mawasiliano haya, neno hili linatumika kuleta maana ya rushwa au hongo sababu kuu ni kwamba, kikombe kina uhusiano na chai ambayo inaandaliwa kwenye kikombe hivyo basi, kuna uhusiano unaodhihirisha ukaribiano kimaana.

Isitoshe, kuna matumizi ya neno **silaha** ambalo lina maana msingi ya kifaa chochote ambacho kinaweza kutumika kupigania ambacho kinaweza kujeruhi au kua kama vile bunduki, rungu na mkuki. Lakini katika muktadha wa mawasiliano haya, neno **silaha** limepata mageuzi ya kimaana na kuwa kitambulisho cha kura kwani, kitambulisho ni sawa na silaha ya kupiga kura.



Cleophas Nyongesa

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)



· 5 Machi saa 07:40 ·

Ni heri wazalendo kuchonga mizinga yao kuliko kutegemea keki za wanasiasa.

11

Penda

Maoni

Shiriki

Mfano mwingine wa upanuzi wa kimaana wa kimetonimi unapatikana katika mawasiliano ya nyongesa ambaye anatumia neno **keki**, kisemantiki maana ya neno keki ni aina ya mkate unaotengenezwa aghalabu kwa mchanganyiko wa unga wa ngano, mayai na sukari. Lakini matumizi ya neno hili katika muktadha huu ni kwa maana ya pesa ambazo zinapeanwa na wanasiasa.

Vilevile, neno **mzinga** limesimbwa kisemantiki kwa maana ya kitu kilicho na uwazi ndani ambacho aghalabu ni kirefu na tena kina umbo la duara kitumikacho kufugia nyuki, silaha iliyotengenezwa kwa chuma yenye magurudumu na mwanzi utumikao kurushia risasi na marisao kwa nguvu nyingi, na sehemu ya baiskeli ambayo huwekwa vikombe vya baiskeli na marisao. Katika muktadha wa mawasiliano haya mwasilishi wa ujumbe huu anatumia neno kuchonga mzinga kumaanisha kufanya idili na kuwajibika ipasavyo. Hivyo basi, neno hili linapata upanuzi wa kimaana. Mwanafunzi huyu ametumia usemi wa namna hii katika mawasiliano haya ili kuusetiri ujumbe wake kwa himaya ya wanakikundi ambao ni wasomi wa chuo kikuu pekee na kupunguza makali yaliyomo kwenye ujumbe huu.



Naomi Mwende

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

3 Machi saa 18:35 ·



Soon we gonna sing mhadumu ongeza gilasi

Mwanafunzi huyu anatumia neno **glasi** katika kuwasisha ujumbe wake wa kimawasiliano.

Kisemantiki neno glasi lina maana ya kitu cha kunywa vitu vyowevu yaani vimimina lakini katika muktadha huu, neno hili limetumika kumaanisha kinywaji.

Jambo ambalo hatujui ni kuwa, kinywaji hiki ni pombe au ni sharubati? Hata hivyo, neno glasi limeweza kupata upanuzi wa kimetonimi kwa nia ya kuficha ujumbe kusudiwa kwa hadhira nyingineyo isiyo hadhira lengwa.



Christopher Masengeli

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

3 Machi saa 22:43 ·

Masuala ya BBI Ni usiku wa Giza, tunahitaji ufafanuzi through public education Ila tutawaona wenzetu kuwa Ni sungura yosayosa.

Katika mawasiliano haya, Masengeli ametumia neno usiku na giza , maana msingi ya neno usiku ni wakati baada ya jioni na kabla ya asubuhi na maana ya giza ni hali ya kukosekana kwa mwangaza lakini katika muktadha wa mawasiliano haya, maana ya maneno haya inapata upanuzi na kumaanisha kitu kisichoeleweka. Pia, sungura ni aina ya mnyama lakini katika muktadha wa mazungumzo haya neno sungura limetumika kumaanisha binadamu huu ni upanuzi wa kiistiari ambao mwasilishi wa ujumbe huu ametumia ili kuusetiri ujumbe kwa wanakikundi.



Steve Juma

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

5 Machi saa 04:43 ·

Hakuna haja ya kushinda ukilalama maishani, una nafasi ya kufikia upeo wa ufanisi. Hata hivyo, uchunguzi uliofanywa na wadau ni kuwa Kipchoge Keino wa vyuo vikuu kote ulimwenguni scored, average grades at their O level exam

11

Penda

Maoni

Shiriki

Wilson (2003), anatoa maelezo ambayo yanatupa mwanga katika utafiti huu kuwa, upanuzi wa kategoria ni aina ya upanuzi wa fahiwa ambao unajulikana kitabia kwa matumizi ya majina ya rajamu zinazotambulika mno. Kitu ambacho kimetambulika sana cha kategoria Fulani ya jamii hupanuliwa na kutumikizwa kwenye jamii nzima na pana ambayo kitu kicho hicho hupatikana. Mfano wa aina ya upanuzi huu umeonekana katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook ambapo Juma anasema kwamba; Kipchoge Keino wa vyuo vikuu kote ulimwenguni scored, average grades at their O level exam. Kipchoge keino ni gwiji katika uwanja wa riadha kwa hivyo, anapotumiwa kwenye sentensi, hadhira inaweza kufikiria ufasiri ambao unajitenga zaidina dhana iliyosimbwa kumaanisha kipchoge Keino ambaye hushiriki mbio za riadha. Hata hivyo katika muktadha wa mawasiliano haya, Juma anatumia rajamu hii kumaanisha maprofesa wa vyuo vikuu.



Kennedy Shavanga

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

3 Machi saa 21:22 ·

Shakespeare wa Moi kwa wingi ni wakufunzi wa tasnia ya lugha kwani, viziada lugha hujitokeza katika makala yao mara nyingi.

Penda

Maoni

Shiriki

Katika mawasiliano haya, Shavanga anawasiliana kwa matumizi ya rajamu Shakespear Shakespear ni mtu ambaye alikuwa mwandishi shupavu na alitambulika kote ulimwenguni kwa sababu ya uandishi wake, kwa hivyo jina lake linatumika na watu ambao wanapenda kazi yake ya uandishi na uandishi wake kurejelea watu ambao wana ufundi katika uandishi. Kimuktadha, hali mahususi inajumuishwa hadi katika jamii ambayo ile hali mahususi inashiriki.

Hapa rajamu hii inamaanisha kuwa waliobobea katika uandishi katika chuo kikuu cha Moi ni wakufunzi wa tasnia ya lugha. Hivyo basi neno Shakespear linapata upanuzi wa kikategoria. Mwasilianaji huyu ametumia mkakati huu kwa misingi ya kuufumba ujumbe kwa himaya yake ya mawasiliano na pia kuonyesha uelewa wake katika ulingo wa uandishi.



Naomi Mwende

K.U. Comrades Forum

31 Machi saa 12:45 ·

Viongozi wetu wamekuwa Diego Maradona katika masuala ya ujenzi wa taifa hata mbura ya wakenya ni kwamba wengi Wa bunge hawatatuwezesha kuiona ruwaza ya 2030 katika miaka Na mikaka ijayo

11

Penda

Shiriki

Katika mawasiliano haya, mwanafunzi huyu anawasiliana kwa kutumia rajamu Diego Maradona. Jina hili lilijulikana kote ulimwenguni katika uchanjaa wa mpira wa miguu ambapo mchezaji huyu alitamba kwa umarufu wake katika mchezo wa kandanda, watu wanaopenda mchezo wa kandanda hutumia jina la mchezaji huyu (Diego Maradona). Katika muktadha huu wa wamawasiliano ya jukwaa la Facebook, hali mahususi inajumuishwa hadi katika jamii ambayo ile hali mahususi inashiriki ambayo ni masuala ya uongozi. Hivyo basi tunapata upanuzi wa kikadegoria.

3.2 Hitimisho

Katika sura hii, kauli za wawasilianaji katika jukwaa la Facebook kwa makundi husika ambazo zinaonyesha matumizi ya lugha ya kipragmatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook zimeanishwa kwa misingi ya nadharia yetu ya utafiti ya Blutner (1990), Hata hivyo, suala la upanuzi wa maana katika mawasiliano limeweza kujitokeza bayana. Tumeweza kuainisha aina za upanuzi wa kimaana katika mawasiliano ya Jukwaa la Facebook kama vile; upanuzi wa kiistiari, upanuzi wa chuku, upanuzi wa metonimi, ubunaji na uundaji wa leksimu mpya na upanuzi wa maana kikategoria.

Katika upanuzi wa maana kimawasiliano, tumeweza kubaini kwamba wanafunzi wa chuo kikuu huweza kutumia mkakati huu wa upanuzi wa maana katika mawasiliano yao kwa sababu ya kuusetiri ujumbe wao kwa wanakikundi na kwa lengo la kuwaweka wanakikundi pamoja.

Vilevile, tumefanya ugunduzi kwamba mchakato wa upanuzi wa kategoria hutumiwa na wawasilianaji katika jukwaa la Facebook kwa sababu ya kukwepa kujifunga kwa maana inayobainika waziwazi na pia kwa lengo la kujinadhibisha na wanakikundi.

SURA YA NNE

UBANAJI WA MAANA NA KISIO LA MAANA KATIKA MAWASILIANO YA JUKWAA LA FACEBOOK

4.0 Utangulizi

Katika sura hii, tutafanya uchanganuzi wa matumizi ya lugha kipragmatiki kulingana na nadharia yetu ya utafiti ambayo ni; nadharia ya pragmatiki leksika ya Blutner (1990) tukijikita kwa mawasiliano ya wanafunzi wa chuo kikuu katika makundi ambayo tumeweza kuyataja katika sura ya kwanza sehemu ya mbinu za utafiti ya tasnifu hii. Katika uchanganuzi huu wa matumizi ya lugha kipragmatiki, sura hii inajihusisha na michakato ya kipragmatiki ambayo ni mihimili ya nadharia ya pragmatiki leksika. Michakato yenyewe ni: mchakato wa ubanaji wa kileksika na mchakato wa kisio la maana au ukadiriaji wa kimaana katika matumizi lugha.

Vile vile, sura hii inaangazia sababu ambazo zinawafanya wanafunzi wanaowasiliana katika jukwaa la Facebook kubana maana ya usemi na kutumia maneno ambayo yanahitaji kisio la maana.

4.1 Ubanaji wa kileksika na kisio la maana katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook

Blutner (1998) katika ufafanuzi wake anatumia kuwa, ubanaji wa lugha kileksika ni kutumia faridi leksika kwa minajili ya kupitisha fahiwa ambayo imebanwa au dhana iliyo finyu zaidi kuliko fahiwa ambayo imewasilishwa kimsingi. Maana hii finyu ni lazima iwe na uhusiano na mandhari ambayo yanahusika kwani, maana iliyosimbwa inaweza kubanwa katika maana tofauti kutegemea muktadha.

Katika mchakato huu neno linatumiwa kuonyesha dhana/ fahiwa mahususi zaidi kuliko fahiwa iliyosimbwa kisemantiki na hivyo kusababisha kutokea kwa ufinyu wa maana halisi ya kiisimu. Blutner alitoa ufafanuzi kuwa, hali ya muktadha hufungia nje maana nyingine zote na kuruhusu ufasiri mmoja wa neno lililotajwa. Kisio au ukadiriaji wa maana ni aina ya mabadiliko ambayo kwayo leksimu zilizo thabiti kwa njia Fulani hupanuliwa mwishoni na kujumuisha mawanda ya makundi ambayo kwa yakini yanapatikana nje ya maana yake kamili ya kiisimu. Wilson (2003),

anatuweza kuwa mifano mizuri ni kama vile ; matumizi ya kilegevu ya takwimu za kutupa makadirio ya misamiati ya kimaeneo na misamiati ambayo inafafanuliwa kwa njia ya kukanusha.

Kimsingi, dhana ambazo zinapanuliwa ndizo zinawasilishwa na wasemaji katika usemi huku dhana thabiti za leksimu zikiwa ndizo ambazo zimesimbwa kisemantiki na neno lilo hilo. Tazama mifano ya mawasiliano ya wanafunzi wa chuo kikuu katika jukwaa la Facebook.



Naomi Mwende

K.U. Comrades Forum

18 Machi saa 08:08 ·

Taking somebody from the village is easy but kuitoa village yenyewe kutoka kwa mtu ni noma jameni. Wasee wengi huwazia masuala waliyoelemishwa Na Somo wao halafu inakuwa ni Mlima kuachana Na mwiko, hata hivyo. Kutema some of the village issues inakuwa suala ambalo lonahitaji kutadisi kwa siku nyingi.

Uvillage unawafanya wanagenzi wengi kuinamisha Sheria za shule ba kufanya mambo tumbi yasiyohesabika aushini mwa waja.

11

Katika mawasiliano haya, Mwende anawasiliana kwa matumizi ya neno ‘**somo**’ Kisemantiki neno hili hutumika kuamaanisha maarifa ambayo hupangiliwa katika muktadha maalumu na hutolewa au mtu anapojifunza darasani au vyuoni, au mambo mazuri ama mabaya mtu anayapata kwa kuangalia au kupatwa na jambo lilomkabili. Somo pia ni rafiki wa karibu, mwandani au shoga, mtu ambaye jina lake linalandana na lako na pia neno hili linatumiwa kumaanisha mtu anayewapa mafunzo maalumu ya jando na unyago vijana waliobalehe. Tukitazama muktadha wa mawasiliano haya, tunaona kuwa, mwanafunzi huyu amewasiliana kwa kulenga maana ya mtu ambaye huwapatia vijana mafunzo maalumu ya jando na unyago vijana walio komaa kwa hivyo maana ya neno hili imebanwa na kutupa maana zingine.

Isitoshe, katika mawasiliano yaya haya, kuna matumizi ya neno ‘ **mwiko**’ maana msingi ya neno hili ni, kifaa ambacho hutoka kwa mti na hutumika kusonga ugali, kibati chenye mpini kitumiwacho na mjenzi kuchotea udongo na simiti kupigia plasta na kulainisha kuta wakati wa kujenga na pia mwiko ni kitu au jambo au hata neno ambalo mtu anakatazwa kulifanya, kulisema ama kula kwa sababu ya kuogopa kudhurika kiafya au kufedheheka katika jamii ama jambo ambalo mtu hawezi kulifanya kutokana na imani, msimamo wake au mazoea tu.

Katika muktadha wa mawasiliano haya ya Mwende, maana inayolengwa ni kitu au jambo au hata neno ambalo mtu anakatazwa kulifanya, kulisema ama kula kwa sababu ya kuogopa kudhurika kiafya au kufedheheka katika jamii au jambo ambalo mtu hawezi kulifanya kutokana na imani yake. Hivyo basi maana ya neno hili imebanwa na kutupa maana zingine nje. Wanafunzi hawa huweza kutumia mchakato huu wa ubanaji wa kimaana kwa makusudi ya kulenga maana kusudiwa kwa wanakikundi.

Kuongezea, katika mawasiliano haya, mwende anatumia mkakati wa ukadiriaji wa maana kwa kutumia ukadiriaji wa kivumishi cha pekee ‘**ingi**’ anasema kwamba “ Wasee wengi huwazia masuala waliyoelemishwa na somo wao halafu inakuwa ni mlima kuachana na mwiko” hapa mfasiri wa mawasiliano haya anabaki akiduwa kwa kukosa kujua idadi kamili ya wale watu ambao huwazia masuala ambayo walielelemishwa na somo wao kisha anabaki tu kukisia idadi isiyobainika vyema kwa hivyo utafiti huu unayaunga mawazo ya Wilson (2003).

Pia, matumizi ya kifungu **siku nyingi**, ni mfano wa kisio la maana kwani, mfasiri hawezi kubainisha ni siku ngapi ila pasipo kukisia tu idadi ya siku ambazo zinahitaji kudadisi suala hilo. Mkakati huu ni wa muhimu katika mawasiliano kwa sababu unawasaidia wanafunzi hawa kuepuka suala la kujifunga kwa idadi kamili ya watu na wakati.



Naomi Mwende

K.U. Comrades Forum

Jana saa 02:30 ·

Elimu ni nyenzo ya muhimu sana maishani mwa mja. Lakini Mburukenge wengine walionyesha suala hili kisogo pasi kujua kuwa watakuja teseka mwamboni. Jua linapochomoza inafaa kila MTU awajibike ipasavyo. La mno ni kuwa, kwa nini? Watesi huamua kuwa Mburukenge?

11

Penda

Shiriki

Wilson (2012), katika ufafanuzi wake alioutoa kuhusu ubanaji wa dhana kileksika, anatumia kwamba, ubanaji wa kileksika ni mchakato ambao unahusu matumizi ya neno au sehemu ya ama kipande cha sentensi kiitwacho kirai katika kuonyesha fahiwa mahususi kuliko dhana iliyosimbwa kiisimu. Utafiti huu unakubaliana na ufafanuzi huu na kushadidia kuwa maana pana ya neno ndiyo iliyosimbwa kiisimu kwani wakati ubanaji wa maneno kimuundo na kimaana unafanywa tunapata dhana ndogo katika muktadha wa mazungumzo. Maana iliyojitokeza ni sehemu ya maana paana iliyosimbwa. Katika mawasiliano ya Naomi katika jukwaa la Facebook, kuna matumizi ya neno '**jua**' limetumika kwa maana ya kuwa na ufahamu katika sentensi 'pasi kujua kuwa watakuja teseka mwamboni' hivyo basi maana ya neno hili inabanwa na kuiacha maana nyingine nje. Isitoshe katika muktadha huu huu, mwanafunzi huyu anaendelea kuleta maana ya pili ya neno **jua** kama nyota kubwa kuliko zote yenye uwezo wa kutoa mwangaza na kusababisha joto duniani ambayo hutokea wakati wa asubuhi na kuzama wakati wa jioni.

Haya yanadhihirika katika kijejezi '**Jua linapochomoza inafaa kila MTU awajibike.**' Hivyo basi, maana ya neno hili inabanwa na kuacha maana nyingine nje. Hapa mwasilianaji huyu ametumia mkakati huu kwa minajili ya kuonyesha ujuzi wake katika matumizi ya lugha ili kujinadhibisha na wasomi wenzake wakiwa wanakikundi.

Marisya (2017), katika ufafanuzi wake kuhusu ukadiriaji wa fahiwa, anatumia kwamba, ukadiriaji wa dhana ni hali ambapo ufasiri wa neno ambalo lina dhana finyu hupanuliwa ili

kuhusiana na fahiwa ya kitu ambacho kina maana tofauti na maana halisi ya neno hilo kiisimu. Utafiti huu unayaunga mkono maelezo ya mtafiti huyu na kuongezea kuwa majina ya wanyama ambao wanajulikana kwa tabia Fulani yanaweza kutumika katika mchakato huu wa ukadiriaji wa maana kimakusudi. Kwa mfano katika mawasiliano ya Naomi kwenye jukwaa la Facebook, kuna matumizi ya neno Mburugenge ambapo mfasiri wa ujumbe huu sharti awe na ufahamu wa tabia za ujinga wa mnyama huyu ndiposa aweze kufasiri maana ya mawasiliano haya kimuktadha kwani, kwa sababu mburugenge anafahamika kwa ujinga wake basi mwanafunzi huyu anakusudia kuleta maana ya watu wajinga wasiyojua maana ya elimu maishani kwa usemi **‘Mburugenge wengine’**

Hata hivyo, matumizi ya kivumishi **wengine** ni kukisia tu idadi kwani idadi hiyo haibainiki kikamilifu.

Vilevile, kuna matumizi ya neno **kidogo** ambao ni ukadiriaji wa kiasi kisichobainika na pia matumizi ya neno hili (**kidogo**) ni banaji wa kimaana kwani neno hili lina maana ya namna ya kufanya jambo bila kasi na maana ya chini ya idadi inayotarajiwa. Lakini katika muktadha wa mawasiliano haya, maana fasiriwa ni chini ya idadi inayotarajiwa hivyo basi neno hili limebanwa kimaana na kutupa nje maana nyingine. Mwasilianaji huyu anafanya hivi kwa misingi ya kuepuka kujifunga kwa idadi kamili na pia kuweka wanakikundi pamoja.



Boniface Lens Ochieng

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

9 Machi saa 21:54 ·

Maudhui haya hayapatikani kwa sasa

Hili linapofanyika, kwa kawaidi ni kwa sababu miliki aliishiriki tu kwa kikundi kidogo cha watu, kubadilisha anayeweza kuiona au limefutwa.

Penda

Maoni

Shiriki

Katika chapisho hili, Boniface Lens Ochieng anawasiliana kwa matumizi ya neno ‘**miliki**’. Kisemantiki, neno hili lina fahiwa nyingi kama vile: miliki ni mali aliyo nayo mtu au shirika, nchi ambayo mtawala ana mamlaka nayo aghalabu uongozwa na malkia au mfalme na pia miliki ni kuwa na mali au kitu kinachothaminiwa.

Katika muktadha huu wa kimawasiliano, Boniface anatumia neno hili kuleta maana ya kuwa na kitu kinachothaminiwa hivyo basi, neno hili limebanwa kimaana na kutupa nje maana nyinginezo za neno hili.

Hata hivyo, matumizi ya neno hili kwa kubana maana, ni kwa misingi ya kuwahamasisha na kuwaweka wanakikundi pamoja ili waendeleo kuwa pamoja kwa mawasiliano yao ya jukwaa lao la Facebook wasije wakagura jukwaani.



Cleophas Nyongesa

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)



· **3 Machi saa 07:12** ·

Asante kunipa nafasi kuwa sehemu yenu ili tutambe kwenye nyanja za taaluma pamoja.

3Wewe, Jackizo Wa Izoo na Mwingine 1

Katika mawasiliano ya Cleophas, kuna matumizi ya neno ‘**tamba**’. Kisemantiki, neno hili lina fahiwa nyingi kama vile; zunguka huku na kule ukijisifu na kujigamba, elezea au simulia hadithi kwa watu wengine pia neno hili hutumika kumaanisha hali ya kukosa mpinzani kwenye mashindano au kazi Fulani. Katika muktadha wa mawasiliano haya, mwanafunzi huyu anatumia usemi huu: ‘Asante kunipa nafasi kuwa sehemu yenu ili tutambe kwenye Nyanja za taaluma pamoja’ Tunapojikita kwenye muktadha huu wa mawasiliano, tanapata kwamba neno hili limetumika kwa maana ya kuelezea au kusimulia hadhithi kwa watu wengine au kutongoa. Kwa

hivyo neno hili limebanwa kwa maana hii na kutupa maana nyingine nje. Ubanaji wa aina hii ni wa kusudi la kuwaweka wanakikundi pamoja.



Cleophas Nyongesa

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)



· **3 Machi saa 07:40** ·

Ni vyema nyasi kuelewa siasa za kifahari na kuweka ua kuwazuia mafahari kuichochea.

5Cleophas Nyongesa na Wengine 4

Penda

Maoni

Shiriki

Katika mawasiliano haya, mwanafunzi huyu anawasiliana kwa kutumia neno ‘**ua**’ neno ambalo kimsingi lina tumika kwa maana tatu kama vile; kutoa uhai, sehemu ya mmea inayoning’inia na inazalisha mbegu na matunda, uzio au mzunguko wa kuzuia watu au wanyama kuingia kwenye boma au shamba ovyo ovyo. Katika muktadha wa mawasiliano haya, neno hili limetumika kwa maana ya uzio au mzunguko wa kuzuia watu au wanyama kuingia mahali ovyo ovyo. Kwa hivyo neno hili limebanwa kwa maana moja tu na kutupa nje maana nyingine.



Cleophas Nyongesa

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)



· **5 Machi saa 07:26** ·

Ilikuwa ni mguu niponye, kuchupa, kufokeana na vyombo vya dola kuonyesha ubabe wao katika maeneo yaliyokuwa na chaguzi ndogo. Baadhi ya waheshimiwa walijipata wametiwa nguvuni kwa kucheza ngoma mbaya siku ya kutambua mbivu na mbichi.

11

Katika mawasiliano haya, mwanafunzi huyu anawasiliana akitumia neno kuchupa, ambacho ni kitenzi ambacho kimeundwa kutoka kwa na nomino ‘**chupa**’. Kimsingi, neno hili lina fahiwa zifuatazo: ruka kutoka sehemu moja hadi nyingine, chombo cha kuwekea vinywaji na hali ya nguo kuwa fupi. Katika muktadha wa mawasiliano haya, neno hili limetumika kwa maana ya kuruka kutoka sehemu moja hadi nyingine kwani, mwanafunzi huyu katika mawasiliano yake ameweza kubana neno hilo kwa maana moja (kuruka kutoka sehemu moja hadi nyingine), na kutupa nje maana nyingine za neno chupa.

Vilevile, katika mawasiliano haya, kuna matumizi ya neno ‘**dola**’ ambalo kisemantiki lina maana nyingi kama vile; nchi yenye mfumo kamili wa kiutawala, ikiwa na bunge, mahakama na serikali na pesa inayotumika katika baadhi ya nchi kama marekani, Zimbabwe na nyinginezo. Tukizingatia muktadha wa mawasiliano haya, mwanafunzi huyu amewasilisha ujumbe wake katika jukwaa hili la Kenyan university students kwenya Facebook kwa kulenga maana ya nchi yenye mfumo kamili wa kuitawala, ikiwa na bunge, mahakama na serikali. Hivyo basi mawasiliano haya yamebana matumizi ya neno hili kwa maana moja na kutupa maana nyingine ya neno hili nje kwa sababu za kuufumba ujumbe ili uweze kueleweka tu kwa hadhira mahususi ambayo ni hadhira ya wanafunzi wa chuo kuu katika kikundi hiki.

Isitoshe, kuna matumizi ya mkakati wa ukadiriaji wa kimaana katika mawasiliano haya ambapo mwanafunzi huyu anaawasilisha ujumbe wake kwa kukadiria kiasi cha uchaguzi anaposema chaguzi ndogo ambapo kivumishi **dogo** kimetumika kuonyesha kisio la maana. Bila kusita, usemi ‘**kucheza ngoma mbaya**’ pia unahitaji tu kukisiwa kimaana kwani michezo ya ngoma ni mingi na ngoma mbaya ni gani? Inamlazimu mfasiri wa ujumbe huu akisie maana kuwa kucheza ngoma mbaya ni kwenda kinyume na sheria za uchaguzi.



Cleophas Nyongesa

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)



· **10 Machi saa 01:26** ·

Huenda jamii nyingi katika maeneo ya kaskazini mwa Kenya zikakumbwa na baa la njaa kutokana na uvamizi wa nzige na ukame wa muda mrefu.

Penda

Maoni

Shiriki

Mawasiliano haya ya mwanafunzi huyu, kuna matumizi ya neno ‘**baa**’ neno ambalo linatumika kimsingi kwa maana ya janga linalotokea na kuiathiri jamii, mahali kunakouzwa na kunywea pombe haswa bia pia baa ni teke linalopigwa na mtu aliyelala usingizini. Kwa kuzingatia muktadha wa mawasiliano haya, mwasilianaji ametumia neno hili, kwa kulenga maana ya janga linalotokea na kuathiri jamii. Hivyo basi neno baa limeweza kubanwa kwa maana hiyo moja na kutupa maana nyingine nje. Ubanaji huu ni wa kusudi la kuufanya ujumbe wazi kwa wanajamii ili waweze kuepuka kwa hilo janga panapowezekana.



Peter Xuma

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

3 Machi saa 21:47

Thinking ndani ndani ya box ni msingi wa kuzimuni lakini out of the box

Kolaiti na Wilson (2012), katika kufafanua mchakato wa ubanaji wa kileksika, wanatoa tetezi kuwa, ubanaji wa kileksika ni mchakato ambao unahusu matumizi ya neno katika kuwasilisha dhana mahususi kuliko dhana iliyosimbwa kiisimu. Utafiti huu unakubaliana na ufafanuzi huu na kushadidia kuwa maana pana ya neno ndiyo iliyosimbwa kiisimu na kutoa mfano katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook ambapo Peter Xuma anasema, ‘**Thinking ndani ndani ya box ni msingi wa kuzimuni**’ ili kuelewa maana ya ndani ni sharti mfasiri afanye ufasiri wake kwa kutegemea muktadha wa mazungumzo kwa sababu maana ya neno hili ni pana na inaweza kufasiriwa kwa njia tofauti. Maana ya neno hili kimuktadha ni kuwa na mawazo yaliyobanwa. Hata hivyo, mwasiliano haya yanabana maana kwa misingi ya kulenga wanakikundi pekee kimaana.



Peter Xuma

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

10 Machi saa 07:28 ·

Usomi umekua na changamoto kote ulimwenguni kwani mwanafunzi anaweza kujizatiti na kuinama katika harakati za usomi hadi aone chuo kikuu na kufuzu shahada ya degree, lakini inasemekana kua kuna tasnia zingine vyuoni ambapo baada ya kuinama na kuchanika kwenye mpini aushini, kupata mkate wa kila siku ni kuuma chongoo na kwa meno

4Wewe, Zablon Orangi, Peter Xuma na Mwingine 1

Katika mawasiliano haya ya Xuma, kuna matumizi ya neno ‘**chuo**’ kimsingi, neno hili lina fahiwa nyingi kama vile; sehemu ambayo watoto wa kiislamu wanajifunza kurani na mafundisho mengine ya dini, kisu maalumu cha kuchokonelea madafu na nazi, Taasisi za serikali au za binafsi ambazo hutoa elimu kuanzia cheti hadi shahada na pia chuo linatumika kumaanisha idadi ya ndoa alizowahi kufunga mwanamke au mwanaume.

Kwa kuzingatia muktadha wa mawasiliano haya, mawasilishi wa ujumbe huu ametumia neno hili kwa kulenga maana ya taasisi za serikali au za binafsi ambazo hutoa elimu kuanzia cheti hadi shahada. Hivyo basi maana ya neno hili imebanwa kimatumizi na kutupa maana nyingine nje. Isitoshe kuna ukadiriaji wa kimaana ambapo mwasilishi wa ujumbe huu anatoa kauli kuwa ‘**mwanafunzi anaweza kujizatiti na kuinama katika harakati za usomi hadi aone chuo kikuu**’ maana ya kuinama ni ile hali ya kukunja mgongo, lakini katika muktadha wa mawasiliano haya, mfasiri wa ujumbe huu ni sharti awe na kisio la maana kuwa kuinama ni kufanya bidii katika harakati za usomi ndiposa aweze kupata maana kikamilifu.



Naomi Mwende

kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

10 Machi saa 01:32 ·

BBI inasababisha kuinuka kwa mirengo Na miungano ya kisiasa ambapo mirengo ambayo itaibuka kuwa umenolewa vyema kisiasa utaweza kuona peponi ambako mwaniaji Wa uraisi wao atakuwa akiishi kwa miaka mitano lililo Jambo la shani, Na watakao kosa tupa hawataweza kutia upanga wao makali yatacao wawezesha kuukumbatia ufalme lakini je, Vumbi la kisia nchini ni la ghubari au Jua la mti kati? Tafakari ya Babu.

11

Katika mawasiliano haya, tunaona matumizi ya neno ‘ **tupa**’ ambapo kimsingi, neno hili linatumika kwa maana zaidi ya moja kama vile; kifaa cha kunolea kwa kukereza vitu vyenye makali kama vile panga na jembe, kitendo cha kurusha kitu mbali na wewe na vilevile tupa ni kitendo cha kuacha kutunza familia au watu uliopewa jukumu la kuwatunza. Katika muktadha wa mawasiliano haya, neno hili limetumika kwa maana ya kifaa cha kunolea vitu vyenye makali hivyo basi, neno tupa limebanwa kwa maana moja na kutupa nje maana nyingine.

Isitoshe, kuna kukisia kwa maana katika mawasiliano haya ambapo mwandishi anasema kwamba ‘mirengo ambayo itaibuka kuwa umenolewa vyema kisiasa utaweza kuona **peponi** ambako mwaniaji wa uraisi wao atakuwa akiishi kwa miaka mitano lilio jambo la shani’ Kimuktadha, matumizi ya usemi huu unampa mfasiri wa mawasiliano haya kuwa mwasilianaji anatumia neno peponi kumaanisha ikulu maana ambayo inapatikana kwa misingi ya kukisia tu. Pia matumizi ya neno **kuinuka** katika muktadha huu yanaleta kisio la maana ya kuzuka.



Naomi Mwende

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

5 Machi saa 07:49 ·

Muda wa kuhema umefika kwa wanawania kiti Cha MCA. Wengine washakatwa na wembe tayari.

Penda

Maoni

Shiriki

Katika mawasiliano haya, nawasiana kwa matumizi ya neno ‘**hema**’, neno ambalo lina fahiwa nyingi kama vile; kibanda cha turubali, tokwa na pumzi kwa nguvu. Katika muktadha huu wa mawasiliano, neno hili limebanwa kwa maana ya kutokwa na pumzi kwa nguvu kwa hivyo maana nyingine imetupwa nje kwa kusudi la kulenga maana kusudiwa kikamilifu.



Kennedy Shavanga

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

3 Machi saa 21:28 ·

Wanao mtegemea bwana yesu huwa wamejihami kwa neno ambalo huwapigania katika maelfu na maelf ya vita.

2Faith Nekesa na Christopher Masengeli

Penda

Maoni

Shiriki

Katika muktadha wa mawasiliano haya, mwanafunzi huyu anatumia neno ‘**bwana**’ katika kuwasilisha ujumbe wake. Neno bwana lina maana kadhaa kama vile mwajiri wa mtu, mume wa mtu, tajiri na maana nyinginezo. Hata hivyo, katika muktadha wa mawasiliano haya ya Shavanga, neno hili linafasiriwa kwa maana ya Yesu mwana wa Mungu na hivyo, katika muktadha huu neno hili linabanwa kimaana japo lina maana nyingine lakini katika muktadha huu maana nyingine zote zimefungiwa nje ili maana moja pekee itiliwe maanani ambayo ni ‘Yesu’



Steve Juma

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

2 Mac ·



· Sala kwa bwana yesu iliofanywa na askofu chuoni mwaetu (UoN).Iliwafanya watumia unga na wapiga maji kumwona yesu.

11

Katika mawasiliano haya, mwanafunzi huyu ameweza kutumia neno bwana kwa kubana maana kama ilivyoelezwa hapo juu katika mawasiliano ya shavanga, vilevile, kuna matumizi ya neno ‘**unga**’, neno unga lina maana ya kitu kilichosagwa na kuwa vumbivumbi. Katika muktadha wa kawaida, neno unga linajumuisha vitu vingi vya unga kama vile, unga wa mahindi, unga wa wimbi, unga wa mawele na kadhalika. Hata hivyo, katika muktadha wa mawasiliano haya, neno hili limeweza kubanwa kumaanisha mihadarati kama kokeini dawa ya kulevya ambayo ni ungaunga na kwa hivyo maana nyingine zimeweza kuachwa nje.

Isitoshe, kuna matumizi ya neno ‘**maji**’. Neno maji linatumika kwa maana ya vitu viowevu kama vile, sharubati, pombe, maji ya kunywa na nyinginezo. Katika muktadha wa mawasiliano haya, neno hili limebanwa kwa maana ya pombe na kutupa maana nyingine nje. Ubanaji huu umeweza kufanyika kwa sababu ya kuusetiri ujumbe huu kwa wanakikundi pekee na kuwaweka pamoja.



Kennedy Shavanga

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

4 Machi saa 22:49 ·

Radio ikikosa kaa huwaacha wazee wakishida wakilalama 🙋

1Jackizo Wa Izoo

Katika mawasiliano haya, mwanafunzi huyu anawasiliana kwa matumizi ya neno ‘**kaa**’ Kimsingi, neno hili lina fahiwa nyingi kama vile; kipande chochote cha ukuni kilichochoameka na kubakia kabla ya kuwa jivu, mnyama mwenye miguu sita ambaye ana gamba mwilini na magando mawili akaaye majini, kipande cha mti kwenye nyumba za kiasili kinachokuwa kama nguzo kunakokomezwa paa, ishi katika eneo Fulani, kitendo cha kutia makalio chini, kuwa mahali kwa kipindi Fulani aidha kifupi au kirefu na jinsi kitu kinavyoonekana au kilivyo kwa mtazamo wan je. Katika muktadha wa mawasiliano haya, neno hili limebanwa kwa maana ya kitu kinachobeba nguvu za umeme kitumikacho katika vyombe vinavyotumia umeme kama vile Radio na tochi hivyo basi maana nyingine za neno hili zimeweza kutupwa nje.



Kennedy Shavanga

Kenyan university students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

9 Machi saa 22:23 ·

Mvua ya gharika ni chumo kwa wakulima wa mahindi pamwe na miwa, ambacho ni kinaya kwa wakulima wa nyanya .rasharasha huwafanya wasiopenda kazi kuhema kwa kutafuta mtaji nao wanaopenda bya dezodezo hubaki kikawaida wakijua kwamba wataendelea kuwa kupe kwa mahuluki wenye idili.Ni heri wasomi wavyuo kuwapiga msasa wanagenxi wao ili wasijute maishani na pia wawe dira ya ulimwengu katika siku za mambo.

Penda

Maoni

Shiriki

Katika mawasiliano haya ya Facebook, mwanafunzi huyu anawasiliano kwa matumizi ya neno ‘nyanya’ Kimsingi, neno hili hutumika kwa maana mbili ambazo ni; mamaye wazazi wangu na aina ya mboga lakini katika muktadha huu wa mawasiliano ya jukwaa la Facebook, neno hili limebanwa kwa maana ya aina ya mboga na kutupa maana nyingine ya neno nyanya nje.

Isitoshe, kuna matumizi ya neno ‘dira’ ambapo kiisimu neno hili lina fahiwa nyingi kama vile; kifaa chenye kuonyesha pande za dunia kinachotumiwa na wasafiri hasa wa anga na baharini kuwawezesha kutambua upande ambao wanaelekea, mawazo anayojiwekea mtu au kikundi cha watu kuhusu namna ya kutekeleza jambo Fulani, nguo ndefu inayofanana na kanzu ivaliwayo na wanawake ambayo haikugawanywa katika eneo kati ya kifua na kiuno , dira pia ni hali ya kuondoa nywele kichwani kwa kutumia kifaa kama mkasi au wembe. Katika muktadha wa mawasiliano haya, neno hili limebanwa kwa maana ya mawazo anayojiwekea au kikundi cha watu kuhusu namna ya kutekeleza jambo Fulani kwa hivyo maana nyingine imetupwa nje. Ubanaji huu unatumika hapa kwa misingi ya kuhimiza na kuweka wanakikundi pamoja.



Kennedy Shavanga

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

3 Machi saa 00:36 ·

Giza la kaniki lilitanda pindi malaika was kitivo cha uhandisi alitangazwa kuaga Dunia chuoni

3Jackizo Wa Izoo na Wengine 2

Tukitazama mawasiliano haya ya Kennedy, tunaona matumizi ya neno ‘malaika’ ambapo kimsingi, neno malaika lina maana za kiisimu kama vile; kitoto kichangacha binadamu, nywele zinazoota mwilini mwa binadamu na kiumbe cha mbinguni chenye umbo la kibinadamu na kina mabawa. Katika muktadha huu, maana nyingine za neno hili zinafungiwa nje ili maana moja itiliwe maanani ambayo katika muktadha huu ni kiumbe kichanga cha binadamu. Ubanaji huu umetumika kimakusudi kuonyesha jinsi ambavyo mwanafunzi aliyeaga dunia hakuwa na dosari wala hatia.

Katika mawasiliano haya pia matumizi ya neno giza la kaniki yanaleta kukisia kwa maana ya huzuni giza na rangi jeusi ni ishara ya tukio la huzuni bin simanzi.Hata hivyo matumizi ya usemi huu yanaleta mwanga jinsi wanafunzi wa chuo hicho walikuwa wamehuzunika wakati huo.



Zablon Orangi

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)

10 Machi saa 17:04

Mabilioni ya kina mama walishabikia Siku kuu ya wanawake duniani ambapo kima cha fulusi kisioweza kujulikana kilitumiwa kwa nakshi ya mapambo miongoni mwa minofu ya mapochopocho. Isitoshe koo walitumika kama mboga kwani hawakuitikia jimbi wala mtetea kuandaliwa maadamu ilikuwa siku ya jinsia ya kike pekee.

Penda

Maoni

Shiriki

Katika mawasiliano haya ya Orangi, kuna matumizi ya neno ‘mabilioni’ kimuktadha, neno hili limetumika kuonyesha ukadiriaji wa idadi ya kina mama ambao walishabikia siku ya kina mama. Matumizi ya neno hili ni ya kuonyesha kuwa kina mama ambao walishabikia siku hiyo walikuwa wengi kiasi cha kuesabika mabilioni.

Vilevile, kuna matumizi ya neno ‘**Kima**’ kimsingi neno hili linatumika kwa maana nyingi kama: nyama iliyosagwa ikawa vipande vidogo kabisa kama changarawe, kiasi cha kitu kama vile wema, ubaya, au hata bei ya bidhaa na pia neno kima hutumika kwa maana ya mnyama mdogo wa jamii ya nyani, tumbili au sokwe aliye na rangi ya kijivu na tabia za kibinadamu kama vile uwezo wa kuambua ndizi na kuila. Katika muktadha wa mawasiliano haya, neno kima limebanwa kwa maana ya kiasi cha kitu. Hivyo basi, maana nyingine za neno hili zinafungiwa nje ili maana moja tu itiliwe maanani ambayo ni kiasi cha fulusi kilichotumika kuadhimisha siku kuu ya wanawake ulimwenguni.

Bila kusita, katika mawasiliano yaya haya, mwasilianaji anatumia neno ‘**koo**’ kiisimu neno hili lina fahiwa nyingi kama vile; kuku jike anayetaga mayai, maradhi yanayomfika mtu na yanayoathiri mtu kooni pia koo ni sehemu ya mwili iliyo baada ya kinywa iliyo na uwazi na umbo la mwanzi na hutumiwa kupitisha chakula na hewa. Katika muktadha wa mawasiliano haya, neno hili limebanwa kwa maana ya kuku jike anayetaga mayai. Hivyo basi, maana nyingine zimetupwa nje kwa minajili ya kulenga ujumbe kwa wanakikundi.



Zablon Orangi

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

8 Machi saa 20:51 ·

Pana haja ya kuwa na tai katika mazingira haya. Neno "tai" katika sentensi hii lina maana gani?

33

Maoni 1

Penda

Maoni

Shiriki

Katika mawasiliano haya, kuna matumizi ya neno ‘tai’ neno ambalo kiisimu lina fahiwa nyingi kama: Ndege mla msoga, ukosi wa blausi au shati na aina ya vazi.

Katika muktadha huu, mfasiri wa mawasiliano haya anabaki kukisia maana kusudiwa tu kwani, tai kama aina ya ndege mlamsoga anapatikana katika mazingira yam situ na tai kama vazi au ukosi wa blausi ama wa shati hupatikana katika mazingira yanaohitaji mavazi. Hata hivyo hatujui mwasilianaji anazungumzia mazingira yapi ndiposa maana kusudiwa inabaki jambo la kisio tu.



Zablon Orangi

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

8 Machi saa 20:43 ·

Tembe zinazotumiwa kuthibiti makali ya karatasi zinawafanya waathiriwa wa gonjwa hili kupata matumaini aushini hata hivyo, vidonge hivi vina athari hadi pia kwani mamilioni ya watu kariani huambukizwa virusi bila kujua kwa kushiriki densi ya Papa tuandamane maadamu huwezi kubaini kuwa yule ana uele na huyu ni buheri wa hamza.

Utapata kuwa makahaba wengi hufaulu kujiepusha na ugonjwa huu kwa sababu wao mara nyingi hucheza mchezo wa nipe utafurahi kwa matumizi ya karatasi.

Marisya (2017), katika kufafanua ukadiriaji wa maana anatumia kwamba, ukadiriaji wa maana ni hali ambapo ufasiri wa neno ambalo lina fahiwa finyu hupanuliwa kifahiwa ili kuleta uhusiano wa karibu na maana ya kitu ambacho kina maana tofauti na dhana halisi ya neno hilo kiisimu. Kwa mfano, neno **karatasi** kama linavyotumiwa kurejelea gonjwa la ukosefu wa kinga mwilini katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook na Zablon Orangi, ni kwa kulinganisha jinsi karatasi linavyokuwa nyororo na nyepesi ambapo mtu anayeugua uwele wa ukimwi ana konda mithili ya ng'onda na kuwa mwepesi kama karatasi.

Katika mawasiliano haya, mwanafunzi huyu anaendelea kuwasilisha jumbe zake kwa matumizi ya neno **karatasi** ambayo kimuktadha inaibua maana ya kukisia ambayo ni mipira ya kufanyia mahaba. Hata hivyo, mchezo anaodai kuwa ni wa nipe utafurahi, panahitaji ufasiri wa maana ambao ni wa kukisia tu.

Isitoshe, kuna ukadiriaji wa idadi ambapo mwanafunzi huyu anawasiliana kwa kutumia kivumishi cha idadi mamilioni. Hapa pana maana ya kukisia kuwa wanao ambukizwa virusi vya ukimwi ni watu wengi sana.

Katika mawasiliano ya mwanafunzi huyu, kuna matumizi ya neno, **'tembe'** kiisimu, neno hili lina fahiwa nyingi kama vile; kuku aliyefikia umri wa kutaga mara ya kwanza kabisa, kidonge cha dawa, vijumba vidogo vinavyojengwa kwa udongo na miti kuanzia chini hadi juu ya paa. Katika muktadha wa mawasiliano haya ya jukwaa la Facebook, mwanafunzi huyu (Orangi) anawasilisha ujumbe wake kwa matumizi ya neno hili kwa kubana maana ya vidonge vya dawa na kutupa maana nyingine za neno hili nje.

Vilevile, kuna matumizi ya neno **'pia'** kiisimu neno hili linatumika kumaanisha fahiwa nyingi kama vile; kitu chenye umbo la mviringo kilichochongoka kwa mbele kama koni au umbo la piramidi ambacho huwa kinatumika na watoto kucheza, kwa kukizungusha ncha yake kali ikiwa chini, mfupa ambao upo kwenye mbele ya maungo ya goti ambao huchezacheza, sehemu ya mbele ya chombo cha majini yenye umbo la duara, kadhalika, tena au pamoja na.

Katika muktadha wa mawasiliano haya, neno hili limebanwa kwa maana ya tena au pamoja na. Hivyo basi, fahiwa nyingine zimeachwa nje kwa kusudi la kulenga maana ya jumbe kikamilifu na kufanya ubainike waziwazi kwa wanakikundi.

Ubanaji huu na kisio la maana katika mawasiliano haya umefanywa sababu ya kuuficha ujumbe na kulenga hadhira ya wanakikundi pekee.



Vincent Kasembeli

K.U. - Comrades Forum

Saa 1 ·

Hatihati za mamia ya wanasiasa kuwatayarisha baadhi ya wanamgambo Na panga pamoja Na rungu ili kuzua rabsha katika uchaguzi zinaitenga dimokrasia katika nchi nyingi. This is not required in a civilised nation jameni...!

Katika mawasiliano ya Kasembeli katika jukwaa la Facebook, kuna matumizi ya neno ‘**panga**’ kiisimu neno hili lina fahiwa nyingi kama vile; eneo maalumu ambalo limeteuliwa kwa minajili ya kufanyiwa shughuli za matambiko, kifaa cha kukatia vitu aghalabu miti na ambacho kinafanana na kisu kikubwa kilicho na makali upande mmoja, mahali ambapo panaaminiwa kuwa pana mizimu na watu hupatumia kufanya matambiko aghalabu pangoni, mtoni, milimani au chini ya mti mkubwa, kiumbe mdogo wa baharini ambaye ana umbo la bapa na anapenda kujificha kwenye mchanga, kifaa ambacho kinatumika kukinga tope kwenye gari, baiskeli au pikipiki ili mpandaji asichafuke, shimo katika ardhi lenye maji ambayo hayakauki, ishi katika nyumba au chumba cha mtu kwa makubaliano maalumu ambayo ni ya kumlipa kodi kwa mwezi ama kipindi fulani, weka vitu ama kitu kwa mpangilio na utaratibu ambao unatakikana, kukubaliana kwa jambo fulani kwa ajili ya kulitekeleza, kaa katika hali ya upweke au ukiwa, ishi na mwanamke au mwanamme bila kuwa na ndoa na pia panga ni hali ya kushikilia mtoto vizuri ili aweze kujisaidia.

Katika muktadha wa mawasiliano haya, neno hili limebanwa kwa maana ya kifaa cha kukatia vitu aghalabu miti na ambacho kinafanana na kisu kikubwa chenye makali.

Vilevile, katika mawasiliano haya mwanafunzi huyu amewasilisha ujumbe wake kwa matumizi ya neno ‘**tenga**’ kisemantiki neno hili lina fahiwa nyingi kama vile; aina ya kapu ambalo linatengenezwa kwa mianzi aumiyaa, hali ya kuweka pembeni au kando, bagua mtu, andaa vitu kama chakula na samaki mkubwa jamii ya papa ambaye ana mwiba mkubwa na umbo la bapa ambaye anaishi baharini. Katika muktadha wa mawasiliano haya, neno hili limebanwa kwa maana ya kuweka pembeni au kando masuala ya kidimokrasia. Ubanaji huu unafanywa

kimaksudi kwa sababu ya kulenga ujumbe wakimawasiliano na kuuweka wazi kwa wanakikundi na kuwahamasisha kwa lengo la kuwaweka wawasilianaji wa jukwaa la Facebook pamoja.

Kuongezea, mwanafunzi huyu anawasiliana kwa matumizi ya mkakati wa kisio la maana ambapo katika mawasiliano yake kuna matumizi ya neno ‘**mamia ya wanasiasa**’ hata hivyo linabaki jukumu la mfasiri wa maana ya ujumbe huu kukisia tu idadi iliokusudiwa kimawasiliano pasipo kuwa na idadi bainifu. Mkakati huu wa kisio la maana unatumika kwa ajili ya kukwepa masuala ya kujifunga kwa idadi kamili ambayo huenda ikiwa na dosari katika upande wa kiwango.



Vincent Kasembeli K.U. - Comrades Forum

Saa 23 ·

🗨️ · Ujio Wa gonjwa la Korona ulisababisha mganda kusikika kote ulimwenguni hata hivyo kulingana Na tangazo hilo maalumu inabainika kuwa hata kuukaribia mfuo ni hatari kwa usalama katika maisha ya mahuluki mafungu Na mafungu ya mabilioni.

11

Katika mawasiliano haya ya jukwaa la Facebook, mwanafunzi huyu ana wasilisha ujumbe wake wa kimawasiliano kwa matumizi ya neno ‘**mganda**’ kisemantiki, neno hili limesimbwa kwa fahiwa nyingi kama vile; ngoma ya wanyasa na wazaramo, fungu la mashuke ya fanaka ambayo yamevunwa, kundi la watu ambao wanatembea kwa miguu na baragumu ambalo hupulizwa kutoa ujumbe maalumu. Katika muktadha wa mawasiliano haya ya jukwaa la Facebook, neno mganda limebanwa kwa maana ya baragumu ambalo hupulizwa kutoa ujumbe maalumu.

Vilevile, katika mawasiliano haya, Vincent anawasiliana kwa matumizi ya neno ‘**mfuo**’ kimsingi neno mfuo limesimbwa kwa maana nyingi kama vile; namna ya kuosha nguo, chombo ambacho kinatumiwa na seremala kutoboa mbao, namna mapambo yatengenezwavyo kwa kutumia madini

mahususi, mstari unaochorwa ardhini ilimradi kufuatisha wakati wa kupanda mbegu, mfereji mwembamba kulia na kushoto mwa kila kidole unaotenganisha kucha na nyama ya kidole pembeni mwa ukucha na pia neno mfuio hutumika kwa maana ya kishimo kidogo kinachofanana na mwanandani wa kaburi kinachochimbwa kwenye mvungu wa kitanda cha mwakisu ili kuelekezea maji yanayooshewa maiti kuingia ndani. Katika muktadha wa mawasiliano haya ya jukwaa la Facebook, neno mfuio limebanwa kwa maana ya kishimo kidogo kinachofanana na mwanandani wa kaburi kinachochimbwa kwenye mvungu wa kitanda cha mwakisu ili kuelekezea maji yanayooshewa maiti kuingia ndani. Ubanaji wa maana katika mawasiliano haya ya Vincent unafanywa kwa sababu ya kuwezesha mawasiliano haya kulenga maana na kubainisha waziwazi kwa wawasilianaji wa kundi hili la jukwaa la Facebook.

Isitoshe, katika mawasiliano haya, mwanafunzi huyu ana tumia mkakati wa ukadiriji wa kimaana ambapo tunaona matumizi ya maneno **‘mahuluki mafungu na mafungu ya mabilioni’** Katika muktadha wa mawasiliano haya mfasiri wa maana ya ujumbe huu anabaki kuikadiria maana kuwa ni watu wengi idadi ya mabilioni ambayo haiwezi kubainika kikamilifu. Ukadiriaji huu unafanyika kwa sababu ya kukwepa kujifunga kwa idadi kamilifu ambayo huenda ni ya juu zaidi au hata ya chini. Hata hivyo, hatuwezi tukabaini idadi ya mafungu mwasilianaji anamaanisha katika usemi huu kumaanisha kuwa ukadiriaji wa maana katika mawasiliano haya ni wa sababu ya kuusetiri ujumbe huu kwa wanakikundi ambao ni wanafunzi wa chuo kikuu wanaowasiliana kupitia jukwaa la Facebook.



Vincent Kasembeli

Saa 7 .

Waziri Wa elimu nchini alifua dafu kwa kudadisi masuala nyeti ambayo yalikuwa mwiba katika uchanjaa Wa elimu. Hata hivyo washikadau Wa wizara hiyo waliweza kutoboa chanzo cha Shule nyingi kupitisha wanafuu wengi katika kategoria ya A' kisha mikakati ya kuzipa mwanya huo ikatekelezwa. Hivi sasa ukicheza Na mitiani ya kitaifa ati unauzia watahiniwa utauma copper kisha utaweza kuiona nchi ya Tisa, Kongole kwa bwana prof.

Katika mawasiliano haya, mwanafunzi huyu anawasiliana kwa matumizi ya maneno ‘ **shule nyingi kupitisha wanafuu wengi**’ matumizi ya vivumishi hivi vya pekee yanafanya idadi ya shule na wanafunzi ambao hupita mtihani kwa alama ya juu kukosa kubainika waziwazi. Hata hivyo linabaki jukumu la mfasiri wa ujumbe huu wa kimawasiliano kukisia tu. Matumizi ya mchakato huu ni ya kusudi la kukwepa kujifunga kwa idadi kamilifu ambayo huenda isiwe ya ukweli.

Isitoshe, katika matumizi ya neno ‘**copper na nchi ya tisa**’ linabaki jambo la kukisia maana yake pia kwani copper ni neno la kiingereza ambalo hutumika kumaanisha madini ya dhahabu na nchi ya tisa haijulikani hapa ulimwenguni.

Hata hivyo katika mawasiliano haya mfasiri anabaki kukisia maana ya neno copper kuwa ni risasi na nchi ya tisa ni ahera ambapo ukipigwa risasi unakufa na kwenda ahera. Mchakato huu wa kisio la maana unatumika hapa kwa sababu ya kuusetiri ujumbe kwa wanakikundi na pia kuwalenga tu wanafunzi ambao huwasiliana kwenye jukwaa la Facebook na kuwaweka pamoja.



Steve Juma

Kenyan University Students (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT and Egerton)

2 Mac ·



Watu walimwagika, uhurupark wakifikiria Rayo atatoboka katika huo mkutano hats hapakuwa na nafasi ya inzi kujipenyeza wala kutema mate hats hivyo karibu uwanja huo utabike takrbani mamilioni

Katika mawasiliano haya ya Steve Juma, kuna ukadiriaji wa kimaana ambapo mwanafunzi huyu badala ya kutoa idadi kamili ambayo iliudhuria mkutano, anachia mfasiri wa maana ya ujumbe kukisia idadi kwa usemi ‘takrbani mamilioni’. Mchakato huu unatumika na wanafunzi katika mawasiliano kwa kusudi la kuepuka kujifunga kwa idadi Fulani kwani huenda hesabu ikawa ilimchenga.



Naomi Mwende

K.U. Comrades Forum

20 Machi saa 23:55 ·

Uongozi Wa nchi ya Kenya unapigana vita vyake dhidi ya ubwana Wa Korona kwa kuweka Sheria za kuzingatiwa Na mahuluki lukuki .Isitoshe, miongoni mwa Sheria hizo matumizi ya kompyuta katika shughuli za Taasisi ni suala ambalo linatosheleza huduma za taifa zima kwani, serikali hii yetu ni Swara kwa kuangaza yaliyombeleni. Hata hivyo, Mbulia wengine walijaribu kuleta ukasuku wao katika masuala haya lakini wakapata kuwa Wizara ya afya ni mwamba ambao hautetereki katika kuthibiti baa hili nchini.

Penda

Shiriki

Katika mawasiliano haya, mwanafunzi huyu nawasiliana kutumia kivumishi cha kutilia mkazo, (mahuluki lukuki), maneno haya yanatumika kuonyesha idadi ya watu. Hivyo basi linabaki jukumu la mfasiri wa ujumbe huu kubashiri idadi kusudiwa. Kisio hili la maana ni la kusudi la kuepuka kujifunga kwa idadi kamili.

Isitoshe, kuna matumizi ya neno ‘baa’ katika mawasiliano haya. Kimsingi, neno hili linatumika kumaanisha; eneo la kuuzia pombe na janga au dhiki. Katika mawasiliano haya, neno hili limetumika kimuktadha kwa maana ya janga au dhiki.

Hivyo basi neno hili limeweza kupata ubanaji wa maana ya janga na kutupa nje maana ya eneo la kuuzia pombe. Ubanaji huu umetumika hapa na mwanafunzi huyu kwa sababu za kulenga wanakikundi na kuifanya maana kusudiwa kubainika waziwazi.



Eddy Gar

Kenya Universities Student Organization

11 Aprili saa 12:42 ·

Natafuta bibi. Nipewe number pliz

3232


Maoni 16

Penda

Maoni

Katika mawasiliano haya, mwanafunzi huyu anawasiliana kwa matumizi ya neno ‘**bibi**’ neno ambalo kimsingi lina fahiwa nyingi kama vile; mzazi wa kike aliyemzaa baba au mama yaani nyanya na pia ni jina la heshima linalotumiwa kumwita mwanamke.

Katika muktadha wa mawasiliano haya, neno hili limebanwa kwa maana ya jina la heshima la kumwita mwanamke. Ubanaji huu unafanyika hapa kwa sababu ya kulenga ujumbe kusudiwa kwa wanakikundi.



Loice Wasike

Kenya Universities Student Organization

16 Machi saa 11:00 ·

Comrade aliyepigwa katika chaguzi ndogo zilizohitimika matungu ni wa Kata ya Harambee maeneo ya matungu Mumias, picha ya kwanza alikuwa afisa wa iebc katika huo uchaguzi mdogo, pia alipeleka uchiriku wake huko kisha malaika wa watu akakumbana na Kofi kutoka kwa aliyekuwa waziri wa spoti mbabe. Rashid Echesa.

1010

Katika mawasiliano haya ya jukwaa la Facebook, Wasike anawasiliana kwa matumizi ya neno ‘kata’ kimsingi neno kata lina fahiwa nyingi kama vile; chombo cha kuchotea maji ndani ya mtungi, eneo la utawala au lokesheni, tunganisha sehemu moja ya kitu kwa kisu au kitu chenye makali, kitambaa au pamba inayobandikwa mahali penye kidonda au uvimbe na kitu ambacho hutengenezwa kwa majani au kitambaa na kuviringwa ambacho huwekwa kichwani au begani wakati wa kubeba mzigo ili kupunguza mbinyo au uzi mnene uliosukwa. Katika muktadha wa mawasiliano haya, neno hili limebanwa kwa maana ya eneo la utawala kwa minajili ya kulenga ujumbe uliokusudiwa kimawasiliano.

Vilevile, kuna matumizi ya neno ‘**malaika**’ neno ambalo kimsingi linamaana nyingi kama vile; mtoto mchanga, nywele ambazo huota mwilini, na viumbe wa mbinguni au hurulaini.

Katika mawasiliano haya kimuktadha, neno hili limebanwa kwa maana ya mtoto mchanga kwa sababu ya kulenga ujumbe kusudiwa kimawasiliano.

Isitoshe, kuna ukadiriaji wa kimaana katika mawasilano haya ambapo mwanafunzi huyu anawasiliana kwa matumizi ya neno ‘**ndogo**’ kuonyesha kiasi cha uchaguzi uliofanyika. Hata hivyo ukadiriaji huu wa kimaana ni wa kusudi la kuonyesha aina ya uchaguzi kwa wanakikundi.



Aligura E.A.

Kenya Universities Student Organization



· **11 Aprili saa 21:48** ·

Sai Apa Yunivasithy Bei Ya Nyanya Inacompete Na Unga. Uhuru Fungua 🤔

7373

Maoni 16

Penda

Maoni

Katika mawasiliano haya ya Facebook, mwanafunzi huyu anawasiliano kwa matumizi ya neno ‘**nyanya**’ Kimsingi, neno hili hutumika kwa maana mbili ambazo ni; mamaye wazazi wangu na aina ya mboga lakini katika muktadha huu wa mawasiliano ya jukwaa la Facebook, neno hili limebanwa kwa maana ya aina ya mboga na kutupa maana nyingine ya neno nyanya nje.

Isitoshe, katika mawasiliano haya kuna matumizi ya neno ‘**unga**’ ambalo lina maana ya kitu kilichosagwa na kuwa vumbivumbi. Katika muktadha wa kawaida, neno hili linatumika kujumuisha vitu vingi ambavyo vimesagwa kama vile; unga wa mahindi, unga wa wimbi na kadhalika. Hata hivyo neno unga limeweza kubanwa katika muktadha wa mawasiliano haya ya jukwaa la Facebook kumaanisha mahindi yaliyosagwa na kuwa vumbivumbi yaani chakula.

Ubanaji huu ni wa kimaksudi kwani, umelenga kuusetiri ujumbe kwa maana moja kusudiwa kwa wanakikundi.

4.2 Hitimisho

Katika sehemu hii, michakato ya ubanaji wa maana na kisio la maana katika mawasiliano na jinsi ambavyo inatumiwa na wanafunzi katika mawasiliano yao ya jukwaa la Facebook imejadiliwa na kutolewa mifano mwafaka kutoka kwa jukwaa la Facebook kwa makundi yaliyoteuliwa kufanyiwa uchunguzi. Isitoshe sababu ambazo zinawafanya wawasilianaji wa Facebook wakiwasiliana kwa kutumia mikakati ya ubanaji wa maana na kisio la maana katika mawasiliano pia zimeweza kujadiliwa. Hata hivyo, imebainika katika sura hii kwamba, wanafunzi huwasilisha ujumbe wao kwa matumizi ya mkakati wa ubanaji wa maana katika lugha zaidi ikilinganishwa na jinsi wanavyotumia mkakati wa ukadiriaji wa maana. Sababu kuu ikiwa ni kuuweka ujumbe wa kimawasiliano wazi kimaana na ukadiriaji wa kimaana kimatumizi ni kwa minajili ya kukwepa kujifunga kwa idadi kamilifu ambayo si bainifu na kuusetiri ujumbe wa kimawasiliano kwa wanakikundi pekee.

SURA YA TANO

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.0 Utangulizi

Katika sura hii matokeo ya uchanganuzi wa maana ya kipragmatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook yatajadiliwa na kutathiminiwa kama malengo ya utafiti yameafikiwa au la, kisha katika sura hii pia, tutatoa mapendekezo kuhusu tafiti zingine zinazofaa kufanywa kuhusu suala la maana ya kipragmatiki katika mawasiliano na tafiti nyinginezo katika mitandao ya kimawasiliano.

5.1 Kutathmini Ufanisi wa Malengo ya Utafiti

Katika utafiti huu, tuliongozwa na maswali ya utafiti haya;

1. Je, lugha inayotumika katika jukwaa la Facebook inatumika kwa maana gani kipragmatiki?
2. Je, mikakati ya ubanaji hudhihirika vipi?
3. Mikakati ya upanuzi hudhihirika vipi?

Katika utafiti huu, tulikusanya data kutoka kwenye mtandao wa intaneti. Data hii tuliitoka kutoka kwa mawasiliano ya jukwaa la Facebook ambapo tulitumia makundi matatu ya jukwaa la Facebook ambayo wanafunzi wa chuo kikuu hutumia kutimiza haja zao za kimawasiliano. Makundi ambayo tuliyatumia katika kufanikisha malengo ya utafiti huu ni; Kenyan university students Facebook, K.U. comrades forum Facebook na Kenya universities organization.

Utafiti huu ulikusudia kuafikia malengo matatu ambayo ni; Kubainisha maana ya kipragmatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook, kujadili mikakati ya usimbwaji na upanuzi wa maana na mwisho, kujadili mikakati ya ubanaji wa lugha inavyotumika katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook.

Sura ya kwanza ya utafiti huu imejadili utangulizi ambao umetoa maelezo kuhusu tafiti zilizofanywa katika mitandao ya kijamii tukiwemo na jukwaa la Facebook, sura hii pia imebainisha tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, upeo na mipaka, umuhimu wa utafiti, msingi wa nadharia ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti, mbinu za utafiti, mbinu zilizotumika katika utafiti huu, mbinu zilizotumika kukusanya data katika utafiti, uteuzi wa sampuli, uchanganuzi na uwasilishaji wa data.

Sura ya pili ya utafiti huu imeweza kujadili historia ya jukwaa la Facebook na mifumo ya mawasiliano ya jukwaa la Facebook, Sifa za lugha ya kimawasiliano katika jukwaa la Facebook ambapo tumeangalia usilabishaji, matumizi ya lugha ya Kiswahili, matumizi ya mkutano duara, na matumizi ya ikonihisi na picha, dhana ya pragmatiki, muktadha, na mawasiliano katika jukwaa la Facebook. Isitoshe tumejadili mitazamo ya kipragmatiki na jinsi ambavyo lugha huhusiana na mawasiliano. Vilevile, tumeweza kutoa maelezo kuhusu dhana ya maana kwa kuzingatia nadharia yetu ya utafiti ambayo ni pragmatiki leksika ya Blutner(1990), ambapo tumeonyesha michakato ya kileksika kama vile: Ubanaji wa maana, upanuzi wa maana na kisio la maana katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook ambapo utafiti huu unahusika. Mawazo ambayo yametolewa ni kulingana na mchango wa wataalamu mbalimbali wa lugha na matumizi yake kwa minajili ya kukidhi haja ya kimawasiliano.

Katika sura ya tatu tuliweza kuwasilisha data ya mawasiliano ya wanafunzi wa chuo kikuu ambao huwasiliana kwa kutumia lugha ya Kiswahili kutoka kwenye jukwaa la Facebook kisha tukaifanyia uchanganuzi wa kipragmatiki ili kubainisha jinsi maana ya mawasiliano huweza kubainika kipragmatiki. Sura hii haswa ilijikita katika kuangazia suala la upanuzi wa kimaana katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook ambapo tuliweza kufanya ugunduzi kuwa, katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook, maneno hupata upanuzi wa maana kulingana na muktadha wa matumizi, bila shaka aina za upanuzi uliodhihirika hapa ni; upanuzi wa kiistiari, upanuzi wa chuku, upanuzi wa kategoria, upanuzi wa aina ya ubunaji wa maana mpya na uundaji wa leksimu na upanuzi wa aina ya Metonimi ambapo utafiti huu uliweza kubainisha kuwa wanafunzi wengi hutumia upanuzi wa kiistiari kwa mawasiliano yao katika mchakato wa upanuzi wa maana katika mawasiliano.

Vilevile, tuliweza kugundua kuwa, wawasilianaji wa jukwaa la Facebook huwasiliana kwa matumizi ya mchakato wa upanuzi wa maana kwa sababu ya kuusetiri ujumbe wao wa kimawasiliano, kuuficha ukali ambao unaweza bainika katika usemi wa kimawasiliano kwa mfano katika matumizi ya maneno ya kiidikati na maneno mwiko na pia matumizi ya mkakati wa upanuzi wa maana katika mawasiliano ni wa kusudi la kuwalenga wanakikundi pekee katika mawasiliano na kuwaweka pamoja wawasilianaji wa kikundi kicho hicho cha mawasiliano ya jukwaa la Facebook.

Katika sura ya nne, tuliwasilisha data kutoka kwenye jukwaa la Facebook ambayo tuliifanyia uchanganuzi wa maana ya kipragmatiki kwa kuangazia michakato ya ubanaji wa maana na kisio la maana katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook. Sura hii iliweza kubainisha kuwa wanafunzi wengi hutumia mchakato wa ubanaji katika mawasiliano yao ya jukwaa la Facebook ikilinganishwa na mchakato wa ukadiriaji wa maana au kisio la maana.

Isitoshe, katika utafiti huu, tuliweza kufanya ugunduzi kuwa matumizi ya mkakati wa ubanaji wa maana katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook ni wa kimakusudi kwa sababu wawasilianaji ambao hutumia jukwaa la Facebook kama nyenzo ya kimawasiliano mara nyingi huwasilisha ujumbe wao kwa lengo la kuuweka ujumbe wa kimawasiliano wazi kwa wanakikundi.

Mchakato wa pragmatiki leksika wa ubanaji wa maana katika mawasiliano pia hutumiwa na wanafunzi wa vyuo vikuu nchini katika mawasiliano yao ya jukwaa la Facebook kwa lengo la kuhamasisha na kuwaunganisha wanachama wa kundi hilo la kimawasiliano au wanakikundi wa jukwaa la Facebook na mwisho tuligundua pia kuwa ubanaji wa maana katika mawasiliano ya wanafunzi wa vyuo vikuu ambao huwasiliana kupitia makundi yetu ya utafiti huwasiliana katika jukwaa la Facebook ni wa sababu ya kusisitiza, kuwaonya na kuwahimiza wanakikundi kuhusu masuala ibuka duniani.

Katika matumizi ya mkakati wa kisio au ukadiriaji wa maana, tuliweza kufanya ugunduzi kuwa, sababu ya matumizi ya mkakati huu wa pragmatiki leksika ni kuwa, wanafunzi wa chuo kikuu ambao tuliweza kuzuru mawasiliano yao katika jukwaa la Facebook huwasiliana kwa matumizi ya kisio la maana kwa nia ya kukwepa kujifunga kwa idadi kamilifu ambayo huenda ikawa ni ya urongo.

Vilevile, maneno mengine kimawasiliano ni mwiko kuyawasilisha jinsi yalivyo kikamilifu kwa hivyo inawalazimu wawasilianaji kuwasiliana kutumia ukadiriaji wa maana ya maneno katika mawasiliano kwa minajili ya kuuficha ukali wa maneno hayo na kuusetiri ujumbe wa kimawasiliano kwa wanakikundi.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya pragmatiki leksika ya Blutner (1990) ambapo nadharia hii ilikusudia kutufanikisha katika suala la uchanganuzi wa kipragmatiki wa maana ya kipragmatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook. Utafiti huu umedhihirisha kuwa nadharia ya pragmatiki leksika ni faafu katika harakati za uchanganuzi wa maana ya kipragmatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook kikamilifu kwani, imetuwezesha kupata utambuzi kuwa mwasilianaji ana uhuru wa kutumia maneno kwa namna mbalimbali kulingana na mikakati ya pragmatiki leksika, mwasilianaji anaweza kuusetiri ujumbe wake wa kimawasiliano ili uweze kuwafikia tu wasikilizaji anaowalenga, kuficha ukali wa maneno kama vile matumizi ya maneno mwiko na pia ukuzaji wa lugha kwa kutumia misamiati mipya yenye maana tofauti. Katika utafiti huu tumeweza kufanya ugunduzi kwamba mchakato wa upanuzi wa kimaana katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook hutumika kwa asilimia kubwa kuliko mchakato ya pragmatiki leksika mingine, ukifuatiwa na mchakato wa ubanaji wa kimaana kisha kwa uchache kabisa mchakato wa kisio la maana.

Utafiti huu pia umetuwezesha kugundua kwamba ni vigumu kwa msikilizaji ambaye hayuko katika mazingira ya mawasiliano au msikilizaji ambaye hakushirika katika shughuli husika kuweza kubainisha maana iliyokusudiwa kikamilifu kwa kuwa lugha ni kitu chenye uchangamano mkubwa katika suala la ufasiri wa kimaana.

Kwa ujumla, imedhihirika kuwa malengo ya utafiti huu yametimilika. Kwanza, tumeweza kubainisha maana ya kipragmatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook na kujadili mikakati na usimbwaji na upanuzi wa maana katika mawasiliano ya Facebook, kisha tukaweza kujadili mikakati ya ubanaji wa maana ya lugha inavyotumika na wanafunzi wa vyuo vikuu, katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook.

5.2 Changamoto za Utafiti

Changamoto zilizokumba utafiti huu ni ugumu wa kupata vijelezi vya mawasiliano ambayo wawasilianaji wamewasiliana kwa matumizi ya mikakati ya kipragmatiki. Isitoshe, halijakuwa jambo rahisi kuwapata wanafunzi wanaoegemea lugha ya Kiswahili kimawasiliano kwani wengi wa wanafunzi wa chuo kikuu wana mazoea ya kuwasiliana kutumia lugha ya kiingereza na wengine wao huwasiliana kwa kuchanganya lugha ya Kiswahili na kiingereza.

Hata hivyo baada ya kudadisi zaidi, tulifanikiwa kupata vijelezi vya mawasiliano ambayo yaliweza kufanikisha malengo yetu ya utafiti.

Mtandao wa intaneti pia uliweza kutuchenga kwa sababu mawimbi ya kunasa kurasa za jukwaa la Facebook hayakuwa wakati wowote tulipokuwa na hitaji la kuzuru jukwaa la Facebook.

5.3 Mapendekezo

Utafiti huu, umeweza kuangazia suala la uchanganuzi wa maana ya kipragmatiki katika mawasiliano ya jukwaa la Facebook kwa matumizi ya nadharia ya pragmatiki leksika ya Blutner (1990). Hata hivyo kuna haja ya utafiti mwingine kama huu kufanywa katika Instagram kwa kutumia nadharia hii ya pragmatiki leksika au nadharia ya uhusiano.

Isitoshe, mtafiti anapendekeza utafiti mwingine kufanywa kuhusu miundo ya sentensi katika jumbe za jukwaa la Facebook kwa kufidia uwanja wa sintaksia. Pia pana haja ya watafiti wanaokuja mbeleni kuangazia miundo ya maneno kimofolojia katika jumbe za mitandao ya kijamii kama suala la utafiti kwa matumizi ya nadharia nyingine zinazoweza kutoa maelezo kikamilifu kuhusu mawasiliano.

MAREJELEO

- Atlas, J. D and Levinson (1981). *Itclefts, informativeness and logical form; in p.cole* (ed) Radical pragmatics, New York Press.
- Atlas, J.D (2005). *Logic, Meaning and conversation: Semantical underdeterminacy, Implicature, and their interface*, Oxford: Oxford University Press.
- Austine J.L. (1962). *How to do things with words*. Cambridge: Harvard University Press.
- Beaugrande, Robert de (1991). *Linguistics theory: The Discourse of fundamental works*. London. Longman.
- Beaugrande, Robert de, & Wolfgang Dressler (1981). *Introduction to text Linguistics*. London. Longman.
- Blommaert, J. (2005). *Discourse*. Cambridge University Press.
- Blutner, R. (1998) *Lexical pragmatics journal of semantics*, 15:115-62.
- Blutner, R. (2000). Some aspects of optimality in natural language interpretation. *Journal of Semantics* 17:189-216.
- Blutner, R. (2004), *Pragmatics and the lexicon in L*, Horn & G. Ward (eds) Hand book of pragmatics, Oxford: Blackwell.
- Blutner, R (2011), *Some perspectives on lexical pragmatics readers*: Routledge. London.
- Brown, G. & George Yule (1983). *Discourse analysis*. Cambridge University press.
- Brundage, Sundry (February 8, 2011) Facebook Moving headquarters to menlo park: social networking giant to move into former sun/oracle campus the Almenac menlo park, CA. katika. <http://www.almananews.com/new/show-story.phpid=8270>.
- Carson, R. (2002). *Thoughts and utterances: The pragmatics of explicit communication*, Oxford lackwell.
- Carter, R. (1997). *Investigating English Discourse*. London: Routledge.
- Chomsky, N (1965). *Aspects of the Theory of Syntax*. MIT: Massachusetts, Cambridge.
- Cook, G (1989). *Discourse*. Oxford. Oxford University Press.
- Eckard, R (2002). Semantic change in grammaticalization: in G.katz, S. of the sixth Annual meeting of the Gesellschaft fur semantic sinn & Bedeutung VI, Osnabruck: University of Osnabruck.
- Grice, P. (1967). *Logic and Conversation*, William James Lectures, Havard University, typescript, reprinted in H.P. Grice (1989) *studies in the way of words*, Cambridge, MA: Harvard University press.
- Habwe, J. (1999). "Discourse Analysis of Swahili Political Speeches". Tasnifu ya PhD ambayo haijachapishwa, chuo kikuu cha Nairobi.
- Habwe J & Karanja, P. (2004). *Misingi ya sarufi ya Kiswahili*. Nairobi Phoenix Publishers Ltd.

- Horn, L. (1984). Towards a new taxonomy of pragmatics inference Q-based and R-based Implicature; in D. Schiffrin (ed) *Meaning, form and use in context: Linguistic applications*. Washington, Georgetown University Press.
- Horn, L. (2005). *Current issues in neo-Gricean pragmatics*; *Intercultural pragmatics*, 2:191-204.
- Kiunga, M.T. (2016). “Maana ya usemi na mazungumzo katika mitandao ya kijamii hususani Facebook na Twita”. *Tasnifu ambayo haichachapishwa chuo kikuu cha Nairobi*.
- Langacker, R. (1995). *Language and structure: Some fundamental linguistic concepts*. Cambridge. Harvard University Press.
- Laserson, P.C. (1999). *The dynamic lexicon*, Texas: Princeton University.
- Leech, G. (1981[1974]), *Semantics the study of meaning*, 2nd edn. Harmondsworth: Penguin.
- Leech, G. (1983). *Principles of pragmatics*. London and New York. Longman.
- Levinson, C.S. (1981). *Pragmatics*. Cambridge: C.U.P.
- Lobner, S. (2002). *Understanding semantics*, New York: Oxford.
- Maccvittie, C. & Maekinlay, A. (2008). *Social psychology and Discourse*. London: Willey, Blackwell.
- Massamba et al (2004). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu (FOKISA) Sekondari na Vyujo*. Dar-es-salaam: TUKI.
- Massamba et al (2012). *Sarufi Miundo Ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA) Sekondari na Vyujo*. Dar-es-salaam: TUKI.
- McCawley, J.D. (1978). *Conversational Implicature and the lexicon*: in P. Cole (ed) *Syntax and semantics: pragmatics*, New York: Academic Press.
- McMahon, A. (1994). *Understanding language change*, New York: Cambridge University press.
- Mdee, J.S. (1986). *Kiswahili muundo na Matumizi yake*. Intercontinental Publishers: Nairobi.
- Meillet, A. (1905). *The search for the perfect language*, Paris: Bouillon.
- Mmbwanga, K.F. (2010). “New words and meaning on facebook: Alexical pragmatics Analysis”, Unpublished MA thesis University of Nairobi.
- Mohammed, M. A. (2001). *Modern Swahili Grammar Nairobi*: East African Educational Publishers
- Morgan, J.L. (1978). *Two types of convention in indirect speech acts in P. Cole's syntax and semantics: pragmatics*. New York academics press.
- Murphy, L. (2003). *Semantic relations and the lexicon*. Cambridge: C.U.P.
- Muyuku, J.A. (2009). *Language mixing in the language of advertising: A case study of commercial banks and mobile Telecommunications in Kenya*. Unpublished MA thesis: University of Nairobi.
- Mwaringa, D. K. (2009). “Globalization and cultural impact of the media, A web analysis of the facebook social network”, MA thesis unpublished University of Nairobi.

- Okuku, W.M.(2010). “Uchanganuzi wa kiisimu wa baadhi ya matini za Kiswahili: Mtazamo wa pragmatiki leksika”. Unpublished MA thesis university of Nairobi, Kenya.
- Palmer, F.K. (1981). *Semantics*. Cambridge C.U.P.
- Raymond, H.(2003). *Motives for language change*. Cambridge university press.
- Recananti, F. (2004). *Literal Meaning*. Cambridge. Cambridge University press.
- Saeed, J.(1997). *Semantics*. Oxford: Blackwell.
- Wamitila, K.W. (2008). *Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*, Vide-Muwa Publishers, Kenya.
- Wangui, Z.N. (2010). “Manifestation of stereotype through Gikuyu figurative language: Alexical pragmatic perspective”, unpublished MA thesis, University of Nairobi Kenya.
- Wilson, D. & Carson, R. (2007). *A unitary approach to lexical pragmatics: Relevance influence and ad hoc concepts*.
- Wilson & Sperber, D. (2002). *Truthfulness and Relevance, Mind and language*, 111:583-632.
- Wilson, D. (2003). *Relevance and Lexical Pragmatics Journal of Linguistics*, Italy.

VIAMBATANISHO

Kiambatanisho cha kwanza

Data ya Kenyan university students



Charles Muchika

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)



· 9 Machi saa 12:26 ·

Viongoz wengine ni mbwakoko jameni kwani asubuhi wamevalia tai wako kwa mwenye kiti wa jubilee kisha usiku wametamba kwingine lakini kuona kwake moses kuria kwamba Raila na DP watafanya kazi pamoja kumenistajabisha sana, na iwapo yatawezekana kutimia basi moses ni unju wa kuona matukio mengi yajayo mbeleni. I meant some leaders or other leaders whichever your way of perception

Penda 🤔🤔🤔

Maoni

Shiriki



Christopher Masengeli

9 Machi saa 15:53 ·

Walai! , wanasiasa wasomi hujibeba katika mijadala kwenye seneti na parliament jameni? Kumtoa mwenzako rangi Hadi umwambie mwenzako jinzi wewe una shahada ya uzamili na unafundisha chuo kikuu.Ni ukosefu wa mvi, kwani waliyo na mvi hujadili masuala ya ujenzi wa taifa ila si kujipiga kifua Hadi inzi wa chooni kukujua.imagini, going ahead and defining fellow politicians how they graduated posting of upper second you have.

Penda 🤔🤔🤔

Maoni

Shiriki



Zablon Orangi

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)

8 Machi saa 21:00 ·

Janga la korona liliporipotiwa nchini Tanzania na vyombo vya habari, Rais Maghufuli alikuwa simba. Kufuatia madai hayo, mambo ambayo alidai ni upuuzi kwa madai kwamba yeye ni msomi wa Kemia. Leo hii mambo yakoje Tanzania? Kauli yako ni ipi kwa huyu mwalimu wa Kemia? 🤔🤔🤔

11

Penda

Maoni

Shiriki



Kennedy Shavanga

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)

9 Machi saa 22:23 ·

Mvua ya gharika ni chumo kwa wakulima wa mahindi pamwe na miwa, ambacho ni kinaya kwa wakulima wa nyanya. rasharasha huwafanya wasiopenda kazi kuhema kwa kutafuta mtaji nao wanaopenda vya dezodezo hubaki kikawaida wakijua kwamba wataendelea kuwa kupe kwa mahuluki wenye idili. Ni heri wasomi wavyuo kuwapiga msasa wanagenxi wao ili wasijute maishani na pia wawe dira ya ulimwengu katika siku za mwambo

Penda

Maoni

Shiriki



Naomi Mwende

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)

5 Machi saa 20:16 ·

Uchaguzi mdogo uliofanyika Kabuchai umefanya ubabe wa shingo wa Rais nchini kushuka bei na kuwezesha Weta kupanda kidhamana.

Penda 🤔🤔🤔

Maoni

Shiriki



Cleophas Nyongesa

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)



5 Machi saa 07:26 ·

Ilikuwa ni mguu niponye, kuchupa, kufokeana na vyombo vya dola kuonyesha ubabe wao katika maeneo yaliyokuwa na chaguzi ndogo. Baadhi ya waheshimiwa walijipata wametiwa nguvuni kwa kucheza ngoma mbaya siku ya kutambua mbivu na mbichi.



Cleophas Nyongesa

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)



· 3 Machi saa 07:23 ·

Kumepambazuka ulimwengu kote! Chanjo ya korona sasa ni pumzi na uhai wa lukuki ya watu kote duniani. Waliokuwa wametamaushwa na janga hilo sasa wana nanga ya kushikilia mashua yao isisombwe na mawimbi.



Cleophas Nyongesa

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)



· 3 Machi saa 07:23 ·

Kumepambazuka ulimwengu kote! Chanjo ya korona sasa ni pumzi na uhai wa lukuki ya watu kote duniani. Waliokuwa wametamaushwa na janga hilo sasa wana nanga ya kushikilia mashua yao isisombwe na mawimbi.



Jackizo Wa Izoo

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)

5 Machi saa 05:56 ·

Wanaume watanashati huvaa kiasi Cha nzi wa uchafu kuwatoroka lakini hawatoboki jamani 😂😂



6Virginia Simiyu, Cleophas Nyongesa na Wengine 4

Penda

Maoni

Shiriki



Steve Juma

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)

2 Machi saa 04:19 ·

Watu walimwagika, uhurupark wakifikiria Rayo atatoboka katika huo mkutano hata hapakuwa na nafasi ya inzi kujipenyeza wala kutema mate



Steve Juma

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)

3 Machi saa 05:02 ·

Korona na karatasi ni homa zinazotishia aghalabu karatasi limethibitiwa na matumizi ya karatasi katika mahaba

Penda

Maoni

Shiriki



Jackizo Wa Izoo

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)

3 Machi saa 07:21 ·

Mibabe wa siasa wamechangamkia suala la BBI

Hadi vinywa vyao vikapanuka. 🤔🤔🤔



Steve Juma

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)

3 Machi saa 04:38 .

Wanasiasa wa leo ni mabeberu wao huwa wana teketeke za kula serekalini tu.

Penda

Maoni

Shiriki



Steve Juma

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)

2 Machi saa 04:22 .

Kwaya ya KU INA Waridi wengi mno, mafisi waliwamezea sana siku hiyo ya graduation

1Simon Katui

Tia moyo

Maoni

Shiriki



Kimutai Godfrey

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)

5 Machi saa 06:56 .

Omba usikutane na watu ambao ni ndumakuwili in life, because life is not a rehearsal my friends.

11



Christopher Masengeli

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)

8 Machi saa 20:42 ·

Kikombe kilitembea katika chaguzi zilizohitimika lakini wanainchi walikuwa tayari wamekata kauli kuwa, silaha zao zitawaendea viongozi waliyo na uwezo katika masuala ya uongozi. Viparaka walikuwa wamekunywa na kumeza unga lakini wembe haukukawia kuwakata.



Cleophas Nyongesa

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)



· 5 Machi saa 07:40 ·

Ni heri wazalendo kuchonga mizinga yao kuliko kutegemea keki za wanasiasa.

11

Penda

Maoni

Shiriki



Naomi Mwende

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)

3 Machi saa 18:35 ·



Soon we gonna sing mhudumu ongeza gilasi



Christopher Masengeli

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)

3 Machi saa 22:43 ·

Masuala ya BBI Ni usiku wa Giza, tunahitaji ufafanuzi through public education Ila tutawaona wenzetu kuwa Ni sungura yosayosa.



Steve Juma

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)

5 Machi saa 04:43 ·

Hakuna haja ya kushinda ukilalama maishani, una nafasi ya kufikia upeo wa ufanisi. Hata hivyo, uchunguzi uliofanywa na wadau ni kuwa Kipchoge Keino wa vyuo vikuu kote ulimwenguni scored, average grades at their O level exam

11

Penda

Maoni

Shiriki



Kennedy Shavanga

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)

3 Machi saa 21:22 ·

Shakespeare wa Moi kwa wingi ni wakufunzi wa tasnia ya lugha kwani, viziada lugha hujitokeza katika makala yao mara nyingi.

Penda

Maoni

Shiriki

11

Penda

Shiriki



Kennedy Shavanga

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)

3 Machi saa 00:36 ·

Giza la kaniki lilitanda pindi malaika was kitivo cha uhandisi alitangazwa kuaga Dunia chuoni

3Jackizo Wa Izoo na Wengine 2



Boniface Lens Ochieng

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)

9 Machi saa 21:54 ·

Maudhui haya hayapatikani kwa sasa

Hili linapofanyika, kwa kawaidi ni kwa sababu miliki aliishiriki tu kwa kikundi kidogo cha watu, kubadilisha anayeweza kuiona au limefutwa.

Penda

Maoni



Cleophas Nyongesa

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)



· 3 Machi saa 07:12 ·

Asante kunipa nafasi kuwa sehemu yenu ili tutambe kwenye nyanja za taaluma pamoja.

3Wewe, Jackizo Wa Izoo na Mwingine 1



Cleophas Nyongesa

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)



· 3 Machi saa 07:40 ·

Ni vyema nyasi kuelewa siasa za kifahari na kuweka ua kuwazuia mafahari kuichochea.

5Cleophas Nyongesa na Wengine 4

Penda

Maoni

Shiriki



Cleophas Nyongesa

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)



· 5 Machi saa 07:26 ·

Ilikuwa ni mguu niponye, kuchupa, kufokeana na vyombo vya dola kuonyesha ubabe wao katika maeneo yaliyokuwa na chaguzi ndogo. Baadhi ya waheshimiwa walijipata wametiwa nguvuni kwa kucheza ngoma mbaya siku ya kutambua mbivu na mbichi.

11



Cleophas Nyongesa

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)



· 10 Machi saa 01:26 ·

Huenda jamii nyingi katika maeneo ya kaskazini mwa Kenya zikakumbwa na baa la njaa kutokana na uvamizi wa nzige na ukame wa muda mrefu.

2Cleophas Nyongesa na Mwingine 1

Penda

Maoni

Shiriki



Peter Xuma

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)

3 Machi saa 21:47 ·

Thinking ndani ndani ya box ni msingi wa kuzimuni lakini out of the box



Peter Xuma

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)

10 Machi saa 07:28 ·

Usomi umekua na changamoto kote ulimwenguni kwani mwanafunzi anaweza kujizatiti na kuinama katika harakati za usomi hadi aone chuo kikuu na kufuzu shahada ya degree, lakini inasemekana kua kuna tasnia zingine vyuoni ambapo baada ya kuinama na kuchanika kwenye mpini aushini, kupata mkate wa kila siku ni kuuma chongoo na kwa meno

4Wewe, Zablon Orangi, Peter Xuma na Mwingine 1



Naomi Mwende

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)

10 Machi saa 01:32 ·

BBI inasababisha kuinuka kwa mirengo Na miungano ya kisiasa ambapo mirengo ambayo itaibuka kuwa umenolewa vyema kisiasa utaweza kuona peponi ambako mwaniaji Wa uraisi wao atakuwa akiishi kwa miaka mitano lililo Jambo la shani, Na watakao kosa tupa hawataweza kutia upanga wao makali yatacao wawezesha kuukumbatia ufalme lakini je, Vumbi la kisia nchini ni la ghubari au Jua la mti kati? Tafakari ya Babu.

11



Naomi Mwendu

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)

5 Machi saa 07:49 ·

Muda wa kuhema umefika kwa wanawania kiti Cha MCA. Wengine washakatwa na wembe tayari.

Penda

Maoni

Shiriki



Kennedy Shavanga

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)

3 Machi saa 21:28 ·

Wanao mtegemea bwana yesu huwa wamejihami kwa neno ambalo huwapigania katika maelfu na maelf ya vita.

2Faith Nekesa na Christopher Masengeli

Penda

Maoni

Shiriki



Boniface Lens Ochieng

KENYAN UNIVERSITY STUDENTS (UON, SEKU, MU, MMUST, KU, JKUAT AND EGERTON)

9 Machi saa 21:54 ·

Maudhui haya hayapatikani kwa sasa

Hili linapofanyika, kwa kawaidi ni kwa sababu miliki aliishiriki tu kwa kikundi kidogo cha watu, kubadilisha anayeweza kuiona au limefutwa.

Penda




Maoni

Shiriki

2.8 Msimulizi wa hadithi Anayeonekana

· Saa 1 ·



unapiga luku na uko na sura personal ad unakaa black market.    anyway

sijacum kwa ubaya.   

3232

Maoni 15

Penda

Maoni

Kiambatanisho cha pili

Data Kutoka K.U. Forum



Naomi Mwende

K.U. COMRADES FORUM

18 Machi saa 08:08 ·

Taking somebody from the village is easy but kuitoa village yenyewe kutoka kwa mtu ni noma jameni. Wasee wengi huwazia masuala waliyoelemishwa Na Somo wao halafu inakuwa ni Mlima kuachana Na mwiko, hata hivyo. Kutema some of the village issues inakuwa suala ambalo lonahitaji kutadisi kwa siku nyingi.

Uvillage unawafanya wanagenzi wengi kuinamisha Sheria za shule ba kufanya mambo tumbi yasiyohesabika aushini mwa waja.

11



Naomi Mwende

K.U. COMRADES FORUM

31 Machi saa 12:45 ·

Viongozi wetu wamekuwa Diego Maradona katika masuala ya ujenzi wa taifa hata mbura ya wakenya ni kwamba wengi Wa bunge hawatatuwezesha kuiona ruwaza ya 2030 katika miaka Na mikaka ijayo

11

Penda

Shiriki



Vincent Kasembeli

K.U. - COMRADES FORUM

Saa 1 ·

Hatihati za mamia ya wanasiasa kuwatayarisha baadhi ya wanamgambo Na panga pamoja Na rungu ili kuzua rabsha katika uchaguzi zinaitenga dimokrasia katika nchi nyingi. This is not required in a civilised nation jameni...!



Vincent Kasembeli**K.U. - COMRADES FORUM**

Saa 23 ·



· Ujio Wa gonjwa la Korona ulisababisha mganda kusikika kote ulimwenguni hata hivyo kulingana Na tangazo hilo maalumu inabainika kuwa hata kuukaribia mfuo ni hatari kwa usalama katika maisha ya mahuluki mafungu Na mafungu ya mabilioni.

11



Vincent Kasembeli

Saa 7 ·

Waziri Wa elimu nchini alifua dafu kwa kudadisi masuala nyeti ambayo yalikuwa mwiba katika uchanjaa Wa elimu. Hata hivyo washikadau Wa wizara hiyo waliweza kutoboa chanzo cha Shule nyingi kupitisha wanafuu wengi katika kategoria ya A' kisha mikakati ya kuzipa mwanya huo ikatekelezwa. Hivi sasa ukicheza Na mitiani ya kitaifa ati unauzia watahiniwa utauma copper kisha utaweza kuiona nchi ya Tisa, Kongole kwa bwana prof.

11



Naomi Mwende

K.U. COMRADES FORUM

20 Machi saa 23:55 ·

Uongozi Wa nchi ya Kenya unapigana vita vyake dhidi ya ubwana Wa Korona kwa kuweka Sheria za kuzingatiwa Na mahuluki lukuki .Isitoshe, miongoni mwa Sheria hizo matumizi ya kompyuta katika shughuli za Taasisi ni suala ambalo linatosheleza huduma za taifa zima kwani, serikali hii yetu ni Swara kwa kuangaza yaliyombeleni. Hata hivyo, Mbulia wengine walijaribu kuleta ukasuku wao katika masuala haya lakini wakapata kuwa Wizara ya afya ni mwamba ambao hautetereki katika kuthibiti baa hili nchini.

Penda

Shiriki

Kiambatanisho cha tatu

Data kutoka KENYA UNIVERSITIES ORGANIZATION



Eddy Gar

KENYA UNIVERSITIES STUDENT ORGANIZATION

11 Aprili saa 12:42 ·

Natafuta bibi. Nipewe number pliz

3232

Maoni 16

Penda

Maoni



Loice Wasike

KENYA UNIVERSITIES STUDENT ORGANIZATION

16 Machi saa 11:00 ·

Comrade aliyepigwa katika chaguzi ndogo zilizohitimika matungu ni wa Kata ya Harambee maeneo ya matungu Mumias, picha ya kwanza alikuwa afisa wa iebc katika huo uchaguzi mdogo, pi akipeleka uchiriku wake huko kisha malaika wa watu akakumbana na Kofi kutoka kwa aliyekuwa waziri wa spoti mbabe .Rashid Echesa

1010



Aligura E.A.

KENYA UNIVERSITIES STUDENT ORGANIZATION



· 10 Februari ·

Wale Wenye Principal Aliambia Hawatajoin Campus, Mlitoboa? 😊

152152

Maoni 50

Penda

Maoni

Maasai Lekishon

Imagine it's only 100 bob guys na hutawai kosa kamaziwa kamtoi 😊😊😊 on this platform I earn between 400-600 daily 😊😊 si mambo ya kuchochana ati 10k daily zii!! Hii ni legit kapunch kako na unasonga 😊😊 join smartpay today. You earn in 5 ways

1. Watch videos for 30 seconds only and get paid 50 bob 😊
2. Easy questions survey questions. 5 questions @ 50 😊
3. Lucky spin win upto 4000 🎉
4. Clicking ads and you get paid 😊
5. Referral (optional) 50 bob for every referral made 🎉
6. Welcome spin free for all new users. 🎉

Minimum withdrawal ni 200 paid directly to your mpesa number. With these utakosaje kapunch (500) daily 🧑 hio ni enough, considering unalipa tu Soo (100) kujoin alafu hutawai lipa dooh ingine tena 😊😊 it's a lifetime investment 😊😊 tafuta kamia tuomoke kimoja na Mia moja 🙌

<https://www.smartpaykenya.com/signup.php?ref=Eagle>

SMARTPAYKENYA.COM

Register to Smartpay

Prince Johnty
ameshiriki chapisho lake la kwanza.



· 16 Aprili saa 09:30 ·

Kirinyaga

university watuu wa financial engineering mko wapii,,,,,,course inawapeka aje 🤔🤔



Cêë Thêë Clĩntõñ

KENYA UNIVERSITIES STUDENT ORGANIZATION

15 Aprili saa 23:24 ·

unaringa na uko Embarambara university (kisii university) 😂😂😂

168168

Maoni 61

Penda

Maoni



Cêë Thêë Clĩntõñ

KENYA UNIVERSITIES STUDENT ORGANIZATION

17 Aprili saa 08:51 ·



kuna university inajiita steve simple boy (Maseno university) be serious guys 😂